**OORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR**

**MHE. PANDU AMEIR KIFICHO - SPIKA**

| | |
|---|---|
| 1. Mhe. Ali Abdalla Ali | Naibu Spika/Jimbo la Mfenesini. |
| 2. Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa | Mwenyekiti wa Baraza Jimbo la Kikwajuni. |
| 3. Mhe. Mgeni Hassan Juma | Mwenyekiti wa Baraza/ Nafasi za Wanawake. |
| 4. Mhe. Balozi Seif Ali Iddi | MBM/Makamu wa Pili wa Rais/Kiongozi wa Shughuli za Serikali/Kuteuliwa na Rais. |
| 5. Mhe. Dr. Mwinyihaji Makame Mwadini | MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Ikulu na Utawala Bora/ Jimbo la Dimani. |
| 6. Mhe. Omar Yussuf Mzee | MBM/Waziri wa Fedha/ Kuteuliwa na Rais. |
| 7. Mhe. Haji Omar Kheri | MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ/Jimbo la Tumbatu. |
| 8. Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji | MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais/Kuteuliwa na Rais. |
| 9. Mhe. Mohammed Aboud Mohammed | MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais/ Kuteuliwa na Rais. |
| 10.Mhe. Abubakar Khamis Bakary | MBM/Waziri wa Katiba na Sheria/Jimbo la Mgogoni. |
| 11. Mhe. Rashid Seif Suleiman | MBM/ Waziri wa Afya/ /Jimbo la Ziwani. |
| 12.Mhe. Ramadhan Abdalla Shaaban | MBM/Waziri wa Ardhi, Maakazi, Maji na Nishati/ Kuteuliwa na Rais. |
| 13.Mhe. Juma Duni Haji | MBM/Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Kuteuliwa na Rais. |
| 14.Mhe. Zainab Omar Mohammed | MBM/Waziri wa Uwezeshaji, Ustawi wa Jamii, Vijana, Wanawake na Watoto/Kuteuliwa na Rais. |
| 15.Mhe. Abdillah Jihad Hassan | MBM/Waziri wa Mifugo na Uvuvi/Jimbo la Magogoni. |
| 16.Mhe. Ali Juma Shamuhuna | MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Donge. |
| 17.Mhe Dr. Sira Ubwa Mamboya | MBM/Waziri wa Kilimo na Maliasili/Kuteuliwa na Rais. |
| 18.Mhe. Nassor Ahmed Mazrui | MBM/Waziri wa Biashara,Viwanda na Masoko/Jimbo la Mtoni. |
| 19.Mhe. Said Ali Mbarouk | MBM/Waziri wa Habari, Utamaduni Utalii na Michezo/Jimbo la Gando. |
| 20.Mhe. Haroun Ali Suleiman | MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi Ya Rais, Kazi na Utumishi wa Umma/Jimbo la Makunduchi. |
| 21.Mhe. Haji Faki Shaali | MBM/ Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Mkanyageni. |
| 22.Mhe. Machano Othman Said | MBM/Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Chumbuni. |

| | |
|---|---|
| 23. Mhe. Shawana Bukheit Hassan | MBM/Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Dole. |
| 24. Mhe. Issa Haji Ussi (Gavu) | Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Chwaka. |
| 25. Mhe. Zahra Ali Hamad | Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Nafasi za Wanawake. |
| 26.Mhe.Mahmoud Thabit Kombo | Naibu Waziri wa Afya/ Jimbo la Kiembesamaki |
| 27.Mhe. Bihindi Hamad Khamis | Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni,Utalii na Michezo/ Nafasi za Wanawake. |
| 28.Mhe. Haji Mwadini Makame | Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/ Jimbo la Nungwi. |
| 29.Mhe. Thuwaybah Edington Kissasi | Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Fuoni. |
| 30.Mhe. Mohammed Said Mohammed | Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi/Jimbo la Mpendae. |
| 31.Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak | Naibu Waziri wa Kilimo na Maliasili/Nafasi za Wanawake. |
| 32.Mhe. Said Hassan Said | Mwanasheria Mkuu. |
| 33.Mhe. Abdalla Juma Abdalla | Jimbo la Chonga |
| 34.Mhe. Abdalla Moh'd Ali | Jimbo la Mkoani |
| 35.Mhe. Abdi Mosi Kombo | Jimbo la Matemwe |
| 36.Mhe. Ali Mzee Ali | Kuteuliwa na Rais |
| 37.Mhe. Ali Salum Haji | Jimbo la Kwahani |
| 38.Mhe. Amina Iddi Mabrouk | Nafasi za Wanawake |
| 39.Mhe. Asaa Othman Hamad | Jimbo la Wete |
| 40.Mhe. Asha Abdu Haji | Nafasi za Wanawake |
| 41.Mhe. Asha Bakari Makame | Nafasi za Wanawake |
| 42.Mhe. Ashura Sharif Ali | Nafasi za Wanawake |
| 43.Mhe. Bikame Yussuf Hamad | Nafasi za Wanawake |
| 44.Mhe. Farida Amour Mohammed | Nafasi za Wanawake |
| 45.Mhe. Fatma Mbarouk Said | Jimbo la Amani |
| 46.Mhe. Hamad Masoud Hamad | Jimbo la Ole |
| 47.Mhe. Hamza Hassan Juma | Jimbo la Kwamtipura |
| 48.Mhe. Hassan Hamad Omar | Jimbo la Kojani |
| 49.Mhe. Hija Hassan Hija | Jimbo la Kiwani |
| 50.Mhe. Hussein Ibrahim Makungu | Jimbo la Bububu |
| 51.Mhe. Ismail Jussa Ladhu | Jimbo la Mji Mkongwe |
| 52.Mhe. Jaku Hashim Ayoub | Jimbo la Muyuni |

| | |
|---|---|
| 53.Mhe. Kazija Khamis Kona | Nafasi za Wanawake |
| 54.Mhe. Makame Mshimba Mbarouk | Jimbo la Kitope |
| 55.Mhe. Marina Joel Thomas | Kuteuliwa na Rais |
| 56.Mhe. Mbarouk Wadi Mussa (Mtando) | Jimbo la Mkwajuni |
| 57.Mhe. Mlinde Mabrouk Juma | Jimbo la Bumbwini |
| 58.Mhe. Mohammed Haji Khalid | Jimbo la Mtambile |
| 59.Mhe. Mohamedraza Hassanali Mohamedali | Jimbo la Uzini |
| 60.Mhe. Mohammed Mbwana Hamadi | Jimbo la Chambani |
| 61.Mhe. Mussa Ali Hassan | Jimbo la Koani |
| 62.Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa | Nafasi za Wanawake |
| 63.Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi | Nafasi za Wanawake |
| 64.Mhe. Nassor Salim Ali | Jimbo la Rahaleo |
| 65.Mhe. Omar Ali Shehe | Jimbo la Chake-Chake |
| 66.Mhe. Panya Ali Abdalla | Nafasi za Wanawake |
| 67.Mhe. Rufai Said Rufai | Jimbo la Tumbe |
| 68.Mhe. Raya Suleiman Hamad | Nafasi za Wanawake |
| 69.Mhe. Saleh Nassor Juma | Jimbo la Wawi |
| 70.Mhe. Salim Abdalla Hamad | Jimbo la Mtambwe |
| 71.Mhe. Salma Mohammed Ali | Nafasi za Wanawake |
| 72.Mhe. Salma Mussa Bilali | Nafasi za Wanawake |
| 73.Mhe. Salmin Awadh Salmin | Jimbo la Magomeni |
| 74.Mhe. Shadya Mohamed Suleiman | Nafasi za Wanawake |
| 75.Mhe. Shamsi Vuai Nahodha | Jimbo la Mwanakwerekwe |
| 76.Mhe. Subeit Khamis Faki | Jimbo la Micheweni |
| 77.Mhe. Suleiman Hemed Khamis | Jimbo la Konde |
| 78.Mhe. Suleiman Othman Nyanga | Jimbo la Jang'ombe |
| 79.Mhe. Ussi Jecha Simai | Jimbo la Chaani |
| 80.Mhe. Viwe Khamis Abdalla | Nafasi za Wanawake |
| 81.Mhe. Wanu Hafidh Ameir | Nafasi za Wanawake |

**Ndugu Yahya Khamis Hamad** **Katibu wa Baraza la Wawakilishi**

**Kikao cha Tatu - Tarehe 23 Januari, 2015**

*(Kikao kilianza saa 3.00 asubuhi)*

**DUA**

*Mhe. Naibu Spika (Ali Abdulla Ali) alisoma dua*

**HATI ZA KUWASILISHWA MEZANI:**

**Mhe. Ussi Jecha Simai (Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba na Sheria):** Mhe. Naibu Spika, ahsane kwa ruhusa yako naomba kuwasilisha Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala kuhusu Mswada wa Sheria ya Kuanzisha Taasisi ya Ulinzi ya Jeshi la Kujenga Uchumi Zanzibar 2015 pamoja na Mambo yanayohusiana na hayo. Naomba kuwasilisha.

**MASWALI NA MAJIBU**

**Nam. 47**

**Ruzuku kwa *"Sobber House"***

**Mhe. Saleh Nassor Juma** - Aliuliza:-

*(Mhe. Mjumbe ameliondoa)*

**Nam.78**

**Muhimili wa Mahakama Kuteua Kiongozi wake**

**Mhe. Jaku Hashim Ayoub** - Aliuliza:-

Kwa kuwa Zanzibar ina nguzo tatu za utawala zinazojitegemea kwa mujibu wa Katiba yaani Serikali, Baraza la Wawakilishi na Mahakama.

a) Je, kwa nini Rais huapishwa na Jaji Mkuu ambaye kwa nafasi yake huteuliwa na Rais.

b) Je, kwa nini Rais humteua Jaji Mkuu na hamteuwi Spika.

c) Je, kwa nini Mahakama nayo isingetengenezwa utaratibu wa kwake wenyewe wa kuteuwa Jaji Mkuu kama ilivyo Baraza la Wawakilishi linavyomteua Spika na je, hali ilivyo sasa haiwezi kusababisha ukosefu wa utawala bora.

**Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria** - Alijibu:-

Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Na.78 kama ifuatavyo.

Mhe. Naibu Spika, ni kweli kwamba Zanzibar ina nguzo tatu za kiutawala zinazojitegemea kwa mujibu wa Katiba ya Zanzibar 1984, lakini mamlaka hizo katika kutekeleza majukumu yake lazima zitegemeane na haziwezi kutenganishwa moja na nyengine. Kwa kuzingatia suala la Utawala Bora.

a) Mhe. Naibu Spika, kutokana na hayo basi ni utaratibu wa uendeshaji ambapo sheria na utaratibu uliowekwa utaheshimiwa na kufuatwa katika utendaji wa shughuli hizo. Kifungu cha 3(2) cha Katiba ya Zanzibar pamoja na kifungu cha 4 cha sheria ya Kiapo cha Uaminifu na barua ya uteuzi Na. 1 ya 1986 ambapo vyote vimempa uwezo Jaji Mkuu kumuapisha Rais. Hii ndio maana ni kwa nini Rais

huapishwa na Jaji Mkuu. Kufanya na kufuata utaratibu huu ndio kutekeleza suala la utawala bora kwa sababu tunatekeleza vifungu vya Katiba na vifungu vya sheria.

b) Ni kweli kwamba Rais humteuwa Jaji Mkuu na hamteuwi Spika. Hii ni kutokana na masharti ya Katiba vile vile. Katiba yetu ya 1984 ambayo imeeleza bayana na kumpa uwezo Rais kumteuwa Jaji Mkuu na Majaji wengine baada ya kushauriana na Tume ya Utumishi ya Mahakama (Kifungu Na.94(1) na (2) na Spika kwa mujibu wa Katiba hiyo hiyo kuchaguliwa na Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi chini ya kifungu Na.73 (1) cha Katiba.

c) Ili Mahakama itengeneze utaratibu wake kuteuwa Jaji Mkuu ni lazima kurekebisha Katiba yetu ya 1984 ili isiwe kwenye mamlaka ya Rais. Lakini mfumo ulipo sasa hauwezi kusababisha ukosefu wa utawala bora kwani kisheria moja wapo ya nguzo ya dhana ya utawala bora ni utawala wa sheria *(Rule of Law).* Hivyo, uwepo wa Katiba na Sheria na kutekelezwa kwa masharti ya sheria tulizojiwekea ni kukua kwa utawala bora. Lakini zaidi ni kuwa Katiba yetu imeweka wazi suala la mgawanyo wa madaraka *(Seperation of Powers)* chini ya kifungu 5(a) (1), (2) na (3).

**Mhe. Jaku Hashim Ayoub:** Mhe. Naibu Spika, pamoja na majibu ya Mhe. Waziri kujibu swali hili kwa nguvu ya hoja, naomba kumuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza.

**Mhe. Naibu Spika:** Inamia *speaker,* hasikii Mhe. Waziri kwa utaratibu.

**Mhe. Jaku Hashim Ayoub:** Pamoja na majibu ya Mhe. Waziri kujibu swali hili kwa nguvu ya hoja ya Kikatiba, haoni wakati umefika wa Katiba yetu tuangalie upya ili Jaji Mkuu wa Zanzibar uteuzi wake utokane na Majaji wenyewe badala ya mfumo unaotumika hivi sasa. Hilo la kwanza.

La pili, kutokana na kwa kuwa Katiba siyo Msahafu utaratibu wa sasa Spika wa kuchaguliwa na Wajumbe wa Baraza na muhimili mwengine wa Dola kiongozi mkuu, haoni Rais hivi sasa wakati umefika kwa suala zima hili kuangaliwa upya.

**Mhe. Naibu Spika:** Swali la pili rejea.

**Mhe. Jaku Hashim Ayoub:** Mhe. Naibu Spika, swali la pili lilikuwa hivi, kwa kuwa Katiba siyo Msahafu utaratibu wa sasa wa Spika kuchaguliwa na Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi na muhimili mwengine kuchaguliwa Dola na kiongozi wake mkuu, Rais haoni usawa unakosekana katika suala zima la utawala bora.

**Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria:** Mhe. Naibu Spika, naomba nimjibu Mhe. Mjumbe maswali yake mawili ya nyongeza kama ifuatavyo.

Jaji Mkuu wa Zanzibar kwa mujibu wa Katiba na Sheria anateuliwa na Rais baada ya kupendekezwa na Tume ya Uajiri ya Mahakama. Tume ya Uajiri ya Mahakama ndiyo inayopendekeza majina ya matatu kwa mfano ya nani awe Jaji Mkuu na pia ndiyo inayopendekeza majina ya Majaji. Sasa inapopendekezwa kule, kwa hivyo, kwa kushauriana na Tume hiyo ndiyo Jaji Mkuu anateuliwa na Rais.

Suala hili la uteuzi wa Jaji Mkuu takriban katika nchi nyingi ndiyo utaratibu huu unavyofanywa, kuna Tume ya Uajiri ya Mahakama inapendekeza na halafu mkuu wa nchi ndiye anateuwa, inategemea kuna nchi nyengine baada ya uteuzi huo au baada ya mapendekezo hayo lazima ithibitishwe na Bunge, lakini kuna nchi ambazo siyo lazima, kwa mfano Kenya lazima ithibitishwe na Bunge kwa Jaji Mkuu, lakini Afrika Kusini kwa mfano na Uganda siyo lazima kuthibitishwa katika utaratibu huo.

Lakini suala la Spika kwa mujibu wa Katiba yetu, Spika anateuliwa na Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi na hii ni utaratibu uliopo katika nchi takriban zote; Kenya, Uganda, Tanzania na nchi nyengine kama hizo. Sasa huu ni utaratibu umewekwa na nchi hizo zina *separation of powers* au zina ile mihimili mitatu ya kinchi.

Kwa hivyo, ukifanya moja kwa mujibu wa Katiba siyo kwamba unavunja ule wa *separation of powers,* lakini kama sisi tunahitaji kwamba Spika kwa mfano ateuliwe na Rais ateuliwe kwa utaratibu ambao utapangwa au Jaji Mkuu ateuliwe na Rais kwa utaratibu uliopangwa, huo ni utaratibu ambao sisi wananchi wa Zanzibar tutautaka, kama tutaka hivyo ni kweli Katiba siyo Msahafu pale pana haja ya kurekebisha Katiba inaweza ikarekebishwa, lakini hiyo

itarekebishwa baada ya makubaliana ya wananchi pamoja na makubaliano ya utaratibu huo huo wa Kikatiba ulivyowekwa namna ya kurekebisha Katiba hiyo.

**Mhe. Saleh Nassor Juma:** Mhe. Naibu Spika, ahsante kwa kuwa Mhe. Waziri amesema wazi kwamba kuna *separation of powers* na Katiba zetu zote, kwa maana ya hii ya Jamhuri na ya Zanzibar inaonesha hivyo. Lakini kwa kuwa amesema Mhe. Waziri kwamba Jaji Mkuu pamoja na kwamba lazima apate mapendekezo ya jopo la Majaji ndiyo ateuliwe na Rais, lakini haoni kwamba kwa nchi zinazotekeleza demokrasia na utawala bora kama sisi, haoni kwamba Rais ku-*nominate* huyo Jaji Mkuu ni *executive,* yaani kuingilia muhimili mwengine wa Dola au wa nchi. Hilo la kwanza.

La pili, kwa kuwa Jaji Mkuu ameteuliwa na Rais, haoni kwamba kwa sababu huyu Jaji Mkuu ni binadamu, kuna siku Rais atafika Mahakama pengine kwa bahati yoyote anaweza akapelekwa Mahakamani, inaweza ikatokezea na nchi nyingi zimeshatokezea. Sasa ikiwa Rais atapelekwa Mahakamani, je, huyu Jaji Mkuu ikiwa ni miongoni mwa majopo la Majaji wanaosimamia hii kesi ya Rais.

Haoni kwamba anaweza akalipa fadhila kwa mteule wake, *that's (b) and (c)* ni sababu gani za msingi ambazo zimesababisha hadi leo hii Katiba hii ya Zanzibar kutorekebishwa na hatimaye *Legislatures* wakajitegemea wenyewe katika kupata kiongozi wao mkuu.

**Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria:** Mhe. Naibu Spika, naomba nimjibu Mhe. Saleh Nassor Juma, maswali yake ya matatu ya nyongeza kama inavyofuata.

a) Rais anapomteuwa Jaji Mkuu haiingilii muhimili mwengine wa utawala. Katiba imesema hivyo na Mhe. Naibu Spika, naomba Mjumbe atizame kwa mfano uteuzi wa Majaji uliopo katika nchi nyengine kama Marekani na Uingereza, ambao Marekani kwa mfano kule wanasema kule *two separation of powers;* yaani yale ile *separation of powers, executive, judiciary* na *legislature* haziingiliani kabisa, lakini *still* Rais ndiye anamteuwa Jaji Mkuu wa Marekani na hii kwa sababu Rais ndiye kiongozi wa nchi, hata kama kuna *separation of powers*, kwa mujibu wa Katiba Rais wa nchi ndiye kiongozi mkuu.

Kwa hivyo, lazima kuwe na nguvu nyengine ambazo lazima apewe yeye, lakini Rais anapomteuwa Jaji Mkuu, ukishamteuwa sasa pale ndiyo inapoanza ile *separation of powers*. Jaji Mkuu anaapishwa akishakuapishwa kiapo chake ni kulinda Katiba na kulinda sheria ambazo yeye ameshakula kiapo. Kwa hivyo, hakuna *interference* baina ya *executive*, yaani Rais na Jaji Mkuu.

b) Hivyo, sioni kwamba kuna maingiliano aina hiyo, lakini pale ambapo kwa kufano Rais atapelekwa Mahakamani, Jaji hatolipa fadhila ikiwa kweli ni Jaji Mkuu na aliyekula kiapo chake na imeshatokea mwahala chungu nzima ambapo Rais ameshatakiwa baada ya kufanya mambo ni kinyume, lakini kwa mujibu wa Katiba yetu na kwa mujibu wa Kanuni za Baraza la Wawakilishi, Rais anapofanya matatizo yoyote yale kinyume na Katina kuna *impeachment of procedure* ambayo ipo katika Kanuni za Baraza la Wawakilishi.

Kwa hivyo, Jaji Mkuu hahusiani kabisa, inafanywa shughuli zile kwa mujibu wa utaratibu uliopo katika Kanuni za Baraza la Wawakilishi, halafu baadae tena ndiyo inakuja ile *valid* kwamba kama Rais amekiuka Kanuni au hakukiuka Kanuni.

c) Suala jengine ambalo amelizungumza Mhe. Saleh Nassor, ni kwamba Katiba, kama nilivyosema mwanzo unaweza kuirekebisha, lakini utaratibu wa kurekebisha Katiba umewekwa pia katika kifungu cha 80 cha Katiba yenyewe. Kwa hivyo, kama tuna haja yoyote ya kurekebisha Katiba, *whether* tuseme kwamba Spika asiteuliwe na Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi, tutamuasisi ateuliwe kwa utaratibu gani au Rais asimteuwe Jaji Mkuu tutamuasisi wenyewe tu ateuliwe kwa namna gani. Pindi ikikubalika na ikawekwa katika Katiba, basi hiyo itakuwa ni Katiba na itabidi lazima tufuate.

Lakini kwamba kipindi hichi wakati sisi tunafuata *Rule of Law* na utawala wa sheria, Rais ndiye mwenye majukumu ya kufanya mambo haya kwa mujibu wa Katiba na kwa mujibu wa wa sheria za viapo kama tulivyosema hapo awali.

**Mhe. Wanu Hafidh Ameir:** Mhe. Naibu Spika, kwa kunipa nafasi hii kumuuliza Mhe. Waziri swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa Mhe. Waziri amekiri kuwa Zanzibar ina nguzo tatu za utawala ambazo zinajitegemea na kwa kuwa katika Katiba ya Zanzibar inaelekeza kuwa Mawaziri wa SMZ wanatokana na Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi ambapo Mawaziri hawa kwa upande mmoja huwa ni *executive* na kwa upande mwengine huwa ni *legislature*. Je, Mhe. Waziri atakubaliana na mimi kuwa Mawaziri wa SMZ kuwa katika pande zote mbili ni kuwa kuna muingiliano wa Katiba na kwamba kunahitajika mabadiliko ya Katiba.

**Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria:** Mhe. Naibu Spika, naomba kumjibu swali lake la nyongeza Mhe. Mjumbe kama ifuatavyo.

Sikubaliani naye kwa sababu *separation of powers*; kuna aina mbili ya *separation of powers*; Kuna *true separation* ambapo *executive, legisture* na *judiciary* haziingiliani kabisa kabisa. Kwa mfano kama Marekani na ndiyo maana utaona Marekani Mawaziri siyo Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi, hiyo ndiyo *two separations*.

Lakini kuna hii iliyokuwa *separation of powers,* lakini imechanganyika changanyika kidogo takriban katika nchi zote za *Commonwealth* pamoja na Uingereza, kwa mfano Wajumbe wa Bunge wanakuwa ni Majaji ndiyo wale *House of Lords* wanapokaa kwenye *chamber* yao, wale baadhi yao ni Wajumbe ambao wapo katika Bunge.

Kwa hivyo, ni *fused*, lakini haina maana kwamba ushakuwa katika *branch* moja na ukawa *branch* nyengine ni kwamba hakuna *separation of powers*. *Separation of powers* inajulikana kwa ule utaratibu wa utekelezaji wa *seperation of powers.* Uingereza na nchi nyingi za *Commonwealth*, *separation of powers* zimekuwa *fused* kwa misingi hiyo, lakini Marekani na baadhi ya nchi *separation of powers* zao ni *two separations, Legisture* hawaingiliani na *executive* na *executive* hawaingiliani na *judiciary*.

Kwa hivyo, hivi sasa sisi tunafuata *separation of powers* katika misingi hiyo. Kama sisi wenyewe tutahisi kwamba mawaziri wasiwe ni wajumbe wa Baraza la Wawakilishi, ni jukumu la bunge lako au Baraza lako tukufu kuamua hivyo na tukiamua hivyo, itabidi tubadilishe Katiba, tukishakubadilisha Katiba basi waziri hatokwenda kugombea kule, waziri itategemea atakavyoteuliwa na itakuwa ile *executive* haiingiliani kabisa na *legislature*. Nakushukuru Mhe. Naibu Spika.

**Nam. 21**

**"E-Learning" Katika Masomo ya Sayansi**

**Mhe. Saleh Nassor Juma** - Aliuliza:-

Tatizo la ukosefu wa walimu wa masomo ya sayansi katika skuli za Zanzibar bado linaendelea kuleta usumbufu katika tasnia ya Taaluma hapa nchini. Kwa kuwa katika miaka ya hivi karibuni Serikali ilifikia maamuzi ya kuajiri walimu wa kigeni kutoka Nigeria, jambo ambalo limepelekea gharama kubwa kwa Serikali yetu.

Je, ni lini Wizara ya Elimu itafanya utaratibu wa kuunganisha mtandao wa kielimu walau kwa shule za Sekondari za juu (*Advance Level Secondary Schools*) za Unguja na Pemba ili wanafunzi wote wa "*A-Level*" hapa Zanzibar waweze kusoma masomo ya sayansi kupitia "*E-learning*".

**Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali** - Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 21. Kwanza Mhe. Naibu Spikia, naomba nitowe utangulizi.

Mhe. Naibu Spika, ni kweli kuwa skuli za Zanzibar zina upungufu wa walimu wa masomo ya Sayansi na Hesabati. Upungufu huu umetokana na uchache wa wanafunzi wanaohitimu mafunzo ya ualimu wa Sayansi na Hesabu katika vyuo Vikuu na Vyuo vya Ualimu. Katika kukabiliana na tatizo hili, serikali imekuwa kitumia mbinu mbali mbali kuongeza idadi ya walimu wa masomo ya Sayansi na Hesabati, ikiwemo kuomba msaada wa walimu wa kujitolea kutoka mataifa na mashirika ya kujitolea yakiwemo Shirika la *VSO* la Uingereza, *Peace Corps* la Marekani, *JICA* la

Japan, Koica la Korea na Serikali ya Nigeria kupitia *"Technical Aids Corps*" ambalo lilikubali kuleta nchini walimu 14 wa kufundisha masomo ya Sayansi na Hesabati katika skuli zetu za Sekondari za vijijini kwa mkataba wa miaka miwili.

Walimu hao hivi sasa wamemaliza mkataba wao wa miaka miwili na wmesharejea makwao na tunatarajia kupokea walimu wengine 36 hivi karibuni. Walimu hao wanalipwa mishahara na Serikali ya Nigeria na kwa upande wetu tunawajibika kuwagharamia huduma za umeme, maji, nyumba na matibabu. Hivyo, gharama zilizotumika kwa ajili ya kuwalipa walimu hao sio kubwa kama Mhe. Mwakilishi alivyodhania.

Pia, faida kubwa imepatikana kutokana na walimu hawa kubadilishana uzoefu na ujuzi katika ufundishaji wa masomo ya Sayansi na Hesabati. Pia, ni kweli kuwa utaratibu wa kufundisha walimu wetu kwa njia ya mtandao au kwa njia nyengine au kwa jina jengine ni *E-learning* utasaidia sana katika kuongeza idadi ya walimu wenye sifa za kufundisha masomo ya sayansi.

Mhe. Naibu Spika, baada ya maelezo hayo naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi kama hivi ifuatavyo:-

Mhe. Naibu Spika, wizara inakusudia kutumia huduma za mtandao wa mawasiliano katika kusomeshea na kufundishia masomo mbali mbali kwa kutumia uwezo mkubwa wa mkongo wa Taifa wa mawasiliano wa simu uliopo hapa Zanzibar. Hata hivyo, kwa hivi sasa ni taasisi chache tu za elimu ndizo zilizounganishwa na mkongo huo wa mawasiliano. Nazo ni Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar, Chuo cha Kiislamu Mazizini, Taasisi ya Karume ya Sayansi na Skuli ya Kiembe Samaki ambayo imeunganishwa hivi karibuni.

Pia, kwa kupitia mradi wa TZ21, unaogharamiwa na Shirika la Kimataifa la Maendeleo la Marekani *(USAID*) skuli za msingi 248, zimepatiwa kompyuta aina ya *Laptop* na kuunganishwa na mtandao kwa ajili ya kusaidia ufundishaji wa masomo ya lugha. Skuli hizi zimeunganishwa na mtandao kupitia kampuni ya Simu ya *Zantel*.

Pia, Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar kwa ufadhili wa Benki ya Dunia imepata fedha kwa ajili ya kuandaa maabara ya kurikodia vipindi mbali mbali vya masomo ya Sayansi na Hisabati. Hivi sasa vipindi hivi vitatumika kutolea mafunzo kwa walimu wa masomo ya sayansi na hisabati kupitia vituo vya walimu. Hata hivyo, kutasaidia katika kuongeza idadi na uwezo wa walimu wa Sayansi na Hisabati. Wizara yangu itaendelea na juhudi za kuzipatia skuli zetu kompyuta na kuunganishwa na mtandao wa mawasiliano kwa kutumia mkongo wa Taifa wa mawasiliano.

**Mhe. Saleh Nassor Juma:** Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri sana ya Mhe. Naibu Waziri, mdogo wangu hapa Mhe. Zahara, naomba kwa heshima kubwa niulize swali dogo la nyongeza kama ifuatavyo. Kwa kuwa Mhe. Naibu Waziri amekiri kwamba ni shule chache zilizounganishwa na huo mkongo wa mawasiliano wa taifa ambao wanapata hii huduma ya *E-learning* na kwa hivyo, asilimia kubwa ya shule bado zinaendelea ku-*suffer* na tatizo la walimu wa sayansi. Kwa kuwa inaonekana hawa Wanaigeria mnaowapendelea sana kuwachukua hawasaidii sana katika mashule yetu.

Je, ni lini serikali itafanya utaratibu wa kuwanasihi walimu wazuri wa sayansi ambao wako katika mawizara na wengine wameshastaafu, ili waweze kupata ule kufanyakazi kupitia ule utaratibu wa *part-time employee,* ambapo hata humu kwenye Baraza walimu wazuri wapo wa sayansi kina mwalimu Salum pale, ni lini mtaanzisha ule utaratibu wa *part-time employee* na vile vile, kuwanasihi na kuwashauri hawa Makatibu Wakuu, ambapo wengine wana nafasi kubwa Makatibu Wakuu, Manaibu Makatibu Wakuu ni walimu wazuri wa masomo ya sayansi. Je, ni lini mtawaomba na wao wakipata nafasi waje hapa mashuleni, wateremke kusomesha *PCM* kama ilivyokuwa siku za nyuma.

**Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:** Mhe. Naibu Spika, kwanza mimi sitaki nikubaliane na Mhe. Saleh Nassor kwa kusema hawa walimu wa Nigeria ambao tunawaleta hawasaidii sana. Mhe. Naibu Spika, walimu hawa ambao tuliwapata kwa awamu ya kwanza, walisaidia sana tena sana katika skuli zetu za Sekondari za mashamba. Kwa mara ya kwanza kuna skuli zilikuwa zikipasisha watoto kuingia Kidato cha Tano, lakini walikuwa hawana sifa kubwa. Lakini kutokana na ile kubadilishana uzoefu kati ya uzoefu walionao walimu wa Nigeria na hapa kwetu, basi imepelekea skuli zile kwa mara ya kwanza wanafunzi kupata *division one*.

Kwa mfano Skuli ya Uzini kwa mara ya kwanza tumepata wanafunzi ambao wamepata *division one* na hii imetokana na msaada mkubwa wa walimu hawa wa Nigeria.

Mhe. Naibu Spika, kwa niaba ya wizara nawashukuru sana hawa walimu, pamoja na Serikali ya Nigeria kwa kutupatia msaada huu.

Lakini jengine alisema tunaonaje kuwachukua hawa walimu wazoefu wa sayansi kutusaidia kufundisha *part-time* katika skuli zetu.

Mhe. Naibu Spika, hilo sidhani kama ni ombi, kwa sababu sio mimi wala waziri wangu hata katika bajeti ya mwaka jana, nilisema kwamba kama kuna walimu wazoefu wa sayansi, basi tunawaomba watusaidie na wapo wengi katika maskuli yetu, wanawasomesha wanafunzi wetu na wanawasaidia sana mheshimiwa.

Kwa hivyo, kama kuna wengine ambao wanaweza kutusaidia bado wizara inasisitiza waje kutusaidia na hata wale ambao wako katika skuli za wenzetu za Bara, basi Mhe. Naibu Spika, ni vizuri kuweka uzalendo mbele, kwa sababu kimshahara kweli kuna tofauti, lakini sio tofauti kubwa. Tofauti Mhe. Naibu Spika, ya 70,000 ikufanye uhame katika mji wako, ikufanye uhame katika nchi yako ambayo imekusomesha. Kwa kweli tunahitaji kuweka uzalendo mbele zaidi Mhe. Naibu Spika.

**Mhe. Subeit Khamis Faki:** Nakushukuru sana Mhe. Naibu Spika, kwa kunipa fursa na mimi kumuuliza Mhe. Naibu Waziri kumuuliza swali moja la nyongeza. Kwanza namshukuru sana Mhe. Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri aliyojibu, na ametueleza kwamba kuna baadhi ya skuli ambazo zimeunganishwa mtandao na watasomeshwa kwa njia ya mtandao. Sasa namuuliza Mhe. Naibu Waziri, kwa kuwa kusomesha kwa njia ya mtandao ni nzuri lakini wanafunzi wakisoma wanataka kusoma kwa vitendo na wakati mwengine wanasoma kwa kuona, yaani *theory* na *practical.*

Sasa namuuliza Mhe. Naibu Waziri Je, katika kusomesha kwa huu mtandao watasomesha kwa njia kama redio au wataweka *TV*, ili wanafunzi wote wawe wanaona kwa vitendo na kwa kusikia?

**Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:** Mhe. Naibu Spika, katika kusomesha kwa njia ya mtandao, tunasomesha na kwa vitendo pia. Mhe. Subeit Khamis kama ungebahatika kuona huu mradi wa *TZ*11 namna wanafunzi wetu wanavyojifunza, basi kwa kweli ungeburudika na ungeona serikali imefanya kazi kubwa.

Pia, Chuo chetu Kikuu cha *SUZA*, kimeanzisha programmu ya *SUZA TV*, kwa hivyo nikisema *SUZA TV* ni kwamba yale mafunzo yake yatakuwa wakati unajifunza na huku unaona kwa vitendo kile ambacho kinafundishwa. Nakushukuru sana Mhe. Naibu Spika.

**Mhe. Salma Mohamme Ali:** Mhe. Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi, baada ya majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri naomba nimuulize swali dogo la nyongeza lenye kifungu (a) na (b). Kwa kuwa katika majibu yake katueleza kuwa bado tatizo la walimu wa sayansi lipo, na kwa kuwa katika Skuli ya Fidel Castro palikuwa na walimu wawili wa sayansi ambao walikuwa wakifundisha vizuri sana masomo haya na kwa kuwa walimu hao mmoja alihamishiwa Chuo cha Amali Vitongoji na mwengine alipelekwa skuli ya kawaida na akapewa nafasi ya Ualimu Mkuu.

Je, kuwaondosha walimu hawa wa sayansi wazalendo katika Skuli ya Sekondari inayotegemewa Pemba na kuwatawanya katika skuli ambazo utaalamu wao hautumiki vizuri. Je, huko Mhe. Naibu Waziri, si kuongeza uhaba wa walimu wa sayansi.

Je, hivi sasa Skuli ya Fidel Castro upungufu wa walimu wa sayansi na hesabu uko kwa kiwango gani?

**Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:** Mhe. Naibu Spika, ni kweli Skuli ya Fidel Castro ni skuli ambayo ni tegemezi kwa Pemba, lakini kama alivyosema yeye mwenyewe kuwa nimekiri kuwa tunaukosefu wa walimu wa hesabu na sayansi. Kwa hivyo, kuwaondosha walimu pale na kwenda kuongeza nguvu katika skuli nyengine, Mheshimiwa sidhani kama ni tatizo. Fidel Castro tuna walimu wa sayansi kuliko skuli nyengine na kuna skuli nyengine tulikuwa hatuna kabisa.

Kwa hivyo, hilo zoezi limefanywa kutokana na angalau na kufidia kidogo katika skuli nyengine. Lakini kama ambavyo nilizungumza awali kwamba tuna walimu 36 ambao tumeshatiliana nao mikataba na kipindi cha karibuni

tu watafika. Kwa hivyo, hao watakapofika tutawaeneza katika skuli zetu mbali mbali za sekondari pale ambapo patakuwa tunahisi pana upungufu mkubwa.

**Nam. 36**

**Zanzibar Kutokuwa na Chuo Cha Ubaharia**

**Mhe. Saleh Nassor Juma** - Aliuliza:-

Zanzibar ni Nchi ambayo eneo la mipaka yake ni eneo lote la Visiwa vya Unguja na Pemba pamoja na Visiwa vidogo vilivyozungukwa na Bahari. Kwa kuwa usafiri wa baharini ni muhimu sana kwa nchi za visiwa na kwa kuwa Zanzibar hutegemea sana usafiri huu huku ikiwa haina hata chuo cha kufundishia mabaharia na hivyo kutegemea zaidi chuo kilichopo Tanzania Bara na kwa kuwa Serikali ya Awamu ya Pili ya Mzee Aboud Jumbe iliona umuhimu wa suala la usafiri wa baharini na kuanzisha chuo chake cha mchepuo wa Sayansi ya Baharini katika shule ya Sekondari ya Lumumba ambayo ilisaidia sana kutoa manahodha (*captains*) na maafisa wakuu (*chief officers*) wengi, ambapo sasa mchepuo huo haupo tena.

Je, ni lini Serikali itaona tena umuhimu wa usafiri wa baharini kwa kuweza kuanzisha chuo chake cha ubaharia.

**Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali** - Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 36 kama ifuatavyo:-

Mhe. Naibu Spika, usafiri wa baharini ni muhimu sana kwa nchi za visiwa kama vile Zanzibar na ni kweli kuwa kwa sasa Zanzibar haina Chuo chake cha kufundisha mabaharia. Baadhi ya mabaharia na manahodha wa meli za Zanzibar wamesomea katika chuo cha Dar-es-Salaam *Maritime Institute* kilichopo Dar-es-Salaam, ambacho ndio chuo pekee kwa nchi za Afrika ya Mashariki.

Pili, ni kweli kuwa katika kipindi cha uongozi wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ya awamu wa pili, Serikali ya awamu ya pili ilianzisha mchepuo wa uvuvi katika Skuli ya Sekondari ya Lumumba. Mchepuo huo ulikuwa na madhumuni ya kuandaa wanafunzi ambao baadae watasomea fani mbali mbali za uvuvi katika ngazi ya elimu ya juu.

Mchepuo huo haukukusudiwa kutoa manahodha (*Captains*) au maafisa wakuu (*Chief Officers*) wa meli. Hata hivyo, wanafunzi waliohitimu skuli hiyo na skuli nyengine za sekondari waliofaulu vizuri masomo ya Fizikia, Hesabati na Jiografia walikuwa na sifa za kuwawezesha kujiunga na vyuo vinavyofundisha masomo ya ubaharia.

Baada ya maeleo hayo, napenda kumjibu Mhe. Mwakilishi kuwa wizara yangu haina lengo la kuanzisha Chuo cha kufundishia ubaharia. Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano ndio wizara inayohusika na masuala ya mafunzo katika fani hiyo.

**Mhe. Saleh Nassor Juma:** Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri, naomba niulize swali moja dogo kama ifuatavyo. Kwa kuwa amekiri kwamba mchepuo uliokuwepo pale Lumumba Sekondari ulitoa vijana wazuri sana katika fani ya sayansi. Kwa mfano *Mathermatic* na *Physics* na hata *Geography* walipasi vizuri. Lakini asisahau kwamba kulikuwa na somo la *Marine* na *Nevigation,* ambapo vile vile walifanya vizuri kwa kupitia mifuko hiyo kuanzia *Form I* mpaka *Form VI* na hatimae wakajiendeleza kupitia hiyo *Marine Sciences* tukatoa Ma-*captaines* wazuri akina marehemu Ali Yassin Juma na kadhalika, ambao walisaidia sana katika kutuendeshea meli zetu hapa pamoja na hizi boti na wengine walikuwa makamanda wazuri kule KMKM.

Je, huoni Mhe. Naibu Waziri pamoja na kwamba wenye kutoa taaluma hiyo ya mambo ya mabaharia, yaani wataalamu katika mambo ya bahari ni Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi, lakini huoni kwamba msingi uliopatikana katika ile awamu ya pili ya Marehemu Mzee Aboud Jumbe pale Lumumba. *No,* aah! Mwenyezi Mungu amzidishie maisha. Haoni kuwa msingi uliowekwa na Rais wa Pili Mzee Aboud Jumbe pale ulisaidia sana kutoa wataalamu wa fani ya bahari, haoni kuna haja ya kuuendeleza badala ya kuwaachia watu wa mawasiliano tu waanzishe mambo hayo, badala ya kuwajengea nyinyi msingi?

**Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:** Mhe. Naibu Spika, nataka nikubaliane na yeye lakini niseme kama wizara ilibidi kuuvunja mchipuo ule kwa wakati ule kwa sababu nyingi tu, lakini moja tukumbuke kama mchipuo ule ulikuwa ni darasa la nane mpaka kumia na mbili, hatukuwa na *Form V* wala *Form VI*. Kwa hivyo, ile *link* ya kuweza wanafunzi wale kuingia Chuo Kikuu ilikuwa haiopo, kwa hivyo, hiyo ilikuwa ni sababu moja haidhuru walikuwa wakitoka pale *Form IV* wanaweza kujiunga na fani nyengine au vyuo vyengine.

Lakini jengine ambalo lilisababisha ni ukosefu wa bajeti, unajua Mheshimiwa Muwakilishi bajeti ya Wizara ya elimu namna ilivyo na mambo ya uvuvi yanahitaji vifaa, mwisho wa siku inahitaji bodi, mashine, nyavu kwa bajeti ambayo tulikuwa nayo kwa Wizara ya Elimu kwa wakati ule basi isingekidhi haja ilikuwa haiwezekani wanafunzi wale kuweza kufikia lengo hasa.

Lakini bado Wizara ya Elimu iko katika kulifikiria suala hilo kwa sababu nchi yetu ni nchi ya visiwa na uvuvi ni sehemu kubwa ya uchumi wa nchi yetu. Nakushukuru sana Mheshimiwa.

**Mhe. Naibu Spika**, Mhe. Ismail Jussa Ladhu, una taarifa au utaratibu au kitu gani? Naona umesimama sijui una nini.

**Mhe. Ismail Jussa Ladhu:** Suala la nyongeza Mheshimiwa au?

**Mhe. Naibu Spika:** Yameshamalizika masuala.

**Mhe. Ismail Jussa Ladhu:** Ahsante bwana.

**Nam. 25**

**Umbali wa Vituo vya Daladala na Kuchelewa kwa Wanafunzi Kufika Skuli**

**Mhe. Jaku Hashim Ayoub** **-** Aliuliza:-

Mhe. Naibu Spika, kabla ya Serikali kutoa majibu ya Namba 25, naomba uniruhusu kutumia ilani ya uchaguzi Mkuu ya mwaka 2010, ukurasa wa 212 kifungu cha 171 (b) kinasema;

"Kuendelea kupiga vita kudhibiti na kutoruhusu vitendo vya ubaguzi wa aina yoyote ile kujitokeza katika sehemu za utoaji wa huduma au fursa mbali mbali za kiuchumi na kijamii miongoni mwa wananchi".

Mhe. Naibu Spika, naomba Serikali itoe jibu la suala hili hivi sasa.

Hivi karibuni Serikali imefanya uamuzi wa kuhamisha kituo cha daladala cha Darajani, tokea uamuzi huo kufanyika, kumekuwa na athari nyingi zimejitokeza ambazo bado ufumbuzi wake ni mgumu. Miongoni mwa athari hizo ni shida wanazopata wanafunzi kushuka kwenye vituo ambavyo vipo mbali na maeneo ya skuli. Hivyo, kuwalazimu kutembea masafa marefu, pamoja na kupishana na misongamano ya watu na dalalada mpaka hufika skuli wakiwa wamechelewa na kuchoka.

(a) Je, lini Serikali itasaidia kuondosha usumbufu huo kwa wanafunzi kwa kuruhusu daladala kupakia wanafunzi na kushusha kituo cha Darajani na kuondoka.

(b) Kuna mpango gani mbadala wa kusaidia wanafunzi wawe na vyombo vya usafiri vya umma kwa ajili yao tu.

**Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano** **-** Alijibu:-

Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 25 lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mhe. Naibu Spika, ni kweli Serikali imeondosha kituo kikuu cha Darajani, kutokana na msongomano na bughudha kubwa kwa wananchi wanaofuata huduma eneo la Darajani pamoja na wanafunzi wanaosoma maeneo ya karibu na hapo.

a) Serikali imeandaa "Mpango mkuu" wa upangaji mji wa Zanzibar, *(Zanzibar Master Plan)* ambao utaingiza sehemu mbali mbali za huduma za jamii kikiwemo kituo kikuu cha daladada ili kuwaondolea usumbufu wanafunzi na wananchi kwa ujumla. Serikali inatafuta kituo muafaka kwa ajili ya kuondoshea usumbufu unaojitokeza.

b) Kwa hivi sasa Serikali haina mpango wa kutoa gari maalum kwa kuwahudumia wanafunzi, lakini wameandaa utaratibu kwa wanafunzi kutozwa nusu nauli, hivyo naomba Waheshimiwa Wawakilishi wajitolee kuwasaidia wanafunzi kadri hali itakavyoruhusu pamoja na wamiliki na watumiaji kwa maana kwamba mmiliki na waendeshaji magari ya daladala na magari mengine ya kibiashara.

**Mhe. Jaku Hassan Ayoub**: Mhe. Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri naomba kuuliza suala moja la nyongeza.

Mhe. Naibu Spika, ndio maana nikaitumia hii ilani makusudi ili kupiga vita ubaguzi, hivi sasa pale tukenda tayari magari yamejazana mwanzo mpaka mwisho, ndio ule ubaguzi uliosemwa katika ilani, hakuna sababu za msingi za kuondosha kituo kile kwa nini asiweke kwa dharura mpaka hiyo *Master plan* ya mji itakavyokamilika baadae wakaondosha.

Huoni Mheshimiwa Waziri ni kuwanyanyasa wananchi wa visiwa hivi vya Unguja na Pemba, huduma pale hivi sasa zinatolewa ndio ule ubaguzi ulio kwenye ilani ya Chama cha Mapinduzi ukienda sasa hivi magari yapo yanalipishwa shilingi mia tano yanapakiwa, wakati kuondosha kituo kile kinasaidia madaktari kutoka Mnazi Mmoja na wanafunzi kufika skuli kwa wakati, huoni ndio ubaguzi wenyewe tunaofanya huo Mhe. Waziri.

Na kama msongamano wizara yako ndio inayoongoza kuleta msongamano katika Mji wa Zanzibar, ukizingatia mnatoa makontena bandarini mchana njia ya kituo cha Malindi pale magari hayapiti mpaka Kinazini, kwa hivyo, Wizara yako inaendelea kuwasumbua wananchi wa Zanzibar.

Mhe. Naibu Spika, naomba jibu.

**Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano:** Mhe. Naibu Spika, la kwanza ningemuomba tu Mheshimiwa Jaku Hassan Ayoub, atambue na aweke uzito wa chombo hiki anachokitumia, kwa maana kwamba anapozungumza ana *address* jamii na wananchi wote na kutaka kujua anachokisema ili watu wakipe uzito na Serikali ikipe uzito kwa ajili ya kuchukua tahadhari ama hatua za utekelezaji.

Serikali imekiondosha kituo cha daladala Darajani, huduma zinazofanyika hivi sasa Darajani ni wanaoegesha magari ya taxi na magari mengineyo, madhumuni ya kuondosha ilikuwa ni msongamano, wote tunakiri kwamba ukiweka daladala ulikuwa ni mkubwa sana, matumizi yanayotumika hivi sasa ni kwa ajili ya kuegesha taxi na gari nyengine.

Nimuombe tu Mheshimiwa Jaku Hassan Ayoub, kwamba kama suala la uondoshaji wa makontena kupelekea msongamano, haya alete kwa utaratibu wake, Serikali sisi tupo tutamueleza nini ambacho tunakikusudia. Madhumuni ya Serikali kwamba kuona tunatafuta eneo muafaka kwa ajili ya kuondoa tatizo la msongamano wa daladala kwa mji wetu wa Zanzibar na ndio maana tukasema kwamba kwa kuliona hilo Serikali hatutaki tufanye kitu kimoja kesho tufanye chengine, tumeona kwamba Serikali iandae utaratibu mzuri wa Mpango Mji wa Mji mzima wa Zanzibar kwa ajili ya kupata maeneo yote yanayostahiki kwa ajili ya maegesho ya magari ya daladala na kwa ajili ya mfumo mzima wa usafiri katika Mji wa Zanzibar.

**Mhe. Salmin Awadh Salmin:** Mhe. Naibu Spika, kwa kunipa nafasi hii kuuliza suala moja la nyongeza.

Mhe. Naibu Spika, suala la kuondosha msongomano katika eneo la Darajani ni suala muhimu na kwanza tuipongeze Serikali kwa kuondosha msongamano katika eneo lile muhimu, lakini eneo ambalo sasa hivi magari wanafuatilia eneo lile la majengo yale ya Michenzani ni eneo ambalo halifai na inaonekana au ilivyoonekana eneo lile kama la

muda, lakini sasa inaonekana eneo lile limeshakuwa la kudumu, lakini ni eneo ambalo halifai na limeleta usumbufu mkubwa sana kwa wananchi.

Namuuliza Mhe. Waziri, pamoja na uamuzi wa kuwaondosha wananchi pale Darajani kupanda magari, Je, muda wote huo Serikali ina mpango gani sasa wa kulitafuta eneo mbadala ili wananchi wasipate usumbufu hasa pale anapotaka huduma katika maeneo yale ya Darajani na maeneo mengine ukizingatia kwamba eneo lile halifai, Serikali ina mpango gani kwa sababu muda unaonekana sasa umeshakuwa mrefu na hakuna juhudi yoyote inayochukuliwa, mbali na majibu ya Mheshimiwa Waziri kwamba wanaweka *master plan. Master plan* hiyo mpaka lini itamalizika?

**Mhe. Naibu Waziri wa Miuondombinu na Mawasiliano:** Mhe. Naibu Spika, ni kweli kwamba kumekuwa kuna kituo katika maeneo ya Michenzani mpaka Afisi kuu ya Chama cha Mapinduzi na eneo hili limetolewa kwa ajili ya kipindi cha muda, sisi kama Serikali tumeunda kama Tume ama Kamati ambapo imeongozwa na usimamizi wa bodi ya usafiri na usalama barabarani, bodi hii imewaalika wahusika wengi wakiwemo watu wa mipango miji, Tawala za Mikoa baadhi ya Madiwani na watu wengine wanaohusiana na masuala mazima ya upangaji wa Mji. Katika maamuzi yetu ambayo tumeamua ambayo yanakuja Serikalini sasa hivi ni kwamba lazima tuende kwa hatua mbili.

Hatua ya kwanza tuwe tuna jambo la muda mfupi ambapo si muda mrefu Serikali itatangaza maeneo ya vituo mbali mbali kuondosha huo usumbufu na hatua ya pili ni hiyo ambayo tunazungumzia ya kwenda katika *Master plan*, ambapo tutalazimika kama Serikali tuwe tuna eneo ambalo tunaita kama *pull*, magari yote yanaishia hapo baadae unachukua gari jengine kutoka hapo kwenda katika maeneo ya mjini kwa ajili ya kupata huduma, kwa kipindi hiki cha mpito Serikali karibu si muda mrefu tutatangaza maeneo maalum kwa ajili ya maegesho ya daladala katika upande wa Mji wa Zanzibar na maeneo yote yanayozunguruka mji wetu.

**Mhe. Mohammed Mbwana Hamad:** Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwa kunipa nafasi ya kumuuliza Mhe. Naibu Waziri suala la nyongeza kama ifuatavyo.

Kwa kuwa kimeondolewa kituo cha daladala cha Darajani kwa kutokana na msongamano mkubwa wa magari pamoja na watu, lakini kuna maeneo mbali mbali Mheshimiwa kwa mujibu wa *nature* yake yanakuwa na msongamano wa magari na watu kwa wakati mwingi, kama vile Darajani, Mwanakwerekwe na kwengineko.

Je, Wizara yako ina mpango gani wa kujenga daraja la juu kwa juu ili kupunguza msongamano huo wa mkato wa watu kwenda katika upande wa pili wa barabara?

**Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano:** Mhe. Naibu Spika, suala la Mheshimiwa Muwakilishi amejielekeza katika suala zima la mrundikano ama msongamano wa magari na wananchi katika maeneo kadhaa, ametoa mfano wa Mwanakwerekwe na maeneo ya Mombasa. Tunaamini kwamba utaratibu mzuri kwamba la kwanza madereva wetu kubaki katika utaratibu wa kisheria unaoongoza matumizi mazuri ya barabara, lakini la pili, kuna maeneo ambayo tayari tumeanza kwa kuweka utaratibu wa muongozo wa mataa kwa ajili ya kuongoza safari tumeanza maeneo ya Mkunazini, tunakwenda eneo la Malindi, baadae tunakuja eneo la Mombasa.

Tunaamini kwamba kama madereva watasimamia vizuri taratibu za usafiri barabarani kwa maana ya kwamba sheria, wenzetu askari wa barabarani wakiwasimamia vizuri madereva hawa na muongozo wa mataa tutaona kwamba matumizi ya barabara kwa msongamano yatapungua. Lakini kwa eneo la Mwanakwerekwe tunaamini kwamba ilikuwepo *conjection* kubwa tumejitahidi kama Serikali kuongeza laini ya pili kwa maana ya kwamba barabara zimekuwa mbili sasa katika eneo lile na kama kuna tatizo tunaamini kwamba tatizo hili linasababishwa na uzembe wa madereva sio ufinyu wa miuondombinu ya barabara.

Kwa hivyo, sisi kama Serikali tunawaomba wenzetu wa Jeshi la Polisi waengeze kasi ya kusimamia eneo lile ili kuondoa msongamano huo ambao unajitokeza.

**Nam. 29**

**Ahadi ya Mhe. Rais Kupeleka Umeme.**

(*Mhe.Mjumbe aliyetaka kuuliza swala hilo ameliondoa*)

**Nam. 81**

**Uchakavu wa Majengo ya Sebleni na Limbani**

**Mhe. Jaku Hashim Ayoub** **-** Aliuliza:-

Majengo ya maendeleo ya wananchi yaliyoko Sebleni na Limbani kule Pemba yamechakaa sana au yamechoka na kuhatarisha maisha ya wazee wetu wanyonge.

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kukarabati majengo hayo ili kuepusha madhara yanayoweza kutokea.

(b) Je, ni lini Serikali itatoa usafiri katika nyumba hizo kwa wale watumishi wanaosaidia wazee hao japo vespa.

**Mhe.Waziri wa Uwezeshaji,Ustawi wa Jamii, Vijana, Wanawake na Watoto -** Alijibu:-

Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 81 lenye sehemu (a) na (b). Kabla ya kujibu napenda kurekebisha maelezo yaliyo katika swala lake, ili kuweka usahihi wa hali halisi kama hivi ifuatavyo:-

Mhe. Spika, kwanza napenda kumfahamisha Mhe. Mwakilishi kwamba majengo ya maendeleo ya wananchi yaliyopo Sebleni Unguja na Limbani hayapo chini ya Wizara yetu sisi, isipokuwa majumba ya wazee yaliyoko Sebleni na Jumba la Wazee liliopo Limbani ndio liko chini ya Wizara ya Uwezeshaji Ustawi wa Jamii Wanawake na Watoto.

(a) Mhe. Spika, Serikali katika kipindi chote cha utekelezaji wa Awamu ya Saba imejipanga vizuri katika suala zima la kukarabati na kuzifanyia matengenezo makubwa nyumba za wazee zilizopo Sebleni kwa Unguja na Limbani kwa Pemba.

Sebleni–Unguja, Serikali kupitia Wizara ya Uwezeshaji, Ustawi wa Jamii, Vijana, Wanawake na Watoto, tayari imeshazifanyia matengenezo makubwa nyumba mbili, kubwa, ukumbi, msikiti, vibanda vya ulinzi, ukuta uliozunguka eneo lote la nyumba ya wazee. Aidha Serikali imefanya ukarabati mkubwa wa miundombinu ya maji na umeme ili kuhakikisha kuwa wazee wanapata huduma hiyo bila ya matatizo yoyote.

Pia, kwa wazee hao, Serikali imeamua kuwapatia milo mitatu kwa siku yaani asubuhi, mchana na usiku na kuwapatia posho la Shilingi Arubaini Elfu (40,000/=) kwa ajili ya matumizi yao madogo madogo ya mkononi.

Kwa upande wa nyumba za wazee za Limbani–Pemba, tayari wizara imeshachukua hatua ya kuandaa makisio ya matengenezo yote yanayohitajika ikiwemo kujenga uzio pamoja na kukarabati nyumba na kujenga miundombinu mipya ya maji na umeme.

Kinachosubiriwa hivi sasa ni kupata fedha kwa ajili ya mradi huo. Nia ya Serikali ni kuzifanyia ukarabati nyumba zote za Sebleni na Limbani ili kuwaweka wazee wetu katika mazingira yaliyo bora zaidi na kujenga ustawi wao kwa jumla.

Kwa hatua hiyo tuliyofikia, sikubaliani na maelezo ya Mhe. Mwakilishi aliesema kwamba “Majengo ya maendeleo ya wananchi yaliyoko Sebleni na Limbani kule Pemba yamechakaa sana au yamechoka na kuhatarisha maisha ya wazee wetu wanyonge.

(b) Mhe. Naibu Spika, suala la kuwapatia vipando watumishi wetu ikiwemo vespa na baskeli viko katika bajeti ya wizara yangu na wakati wowote tukipata fedha suala hilo litatekelezwa kwa kila anaestahiki kupatiwa usafiri wa aina hiyo ili kuleta ufanisi wa kazi na utekelezaji.

Mhe. Naibu Spika, ningeomba kutoa wito kwa Waheshimiwa wote Wajumbe wa Baraza lako Tukufu watenge siku maalum ya kuwatembelea wazee wa Sebleni, Welezo na Limbani ili waone jinsi wanavyoishi na wanavyohudumiwa pamoja na kuona kwa macho yao wenyewe mazingira mazuri wanayoishi kutokana na jitihada zinazofanywa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar chini ya Uongozi wa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dkt. Ali Mohammed Shein. *(Makofi)*

**Mhe. Jaku Hashim Ayoub:** Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, pamoja na majibu ya Mhe. Waziri, kutokufananisha kijiko na upawa naomba kumuuliza suala dogo tu la nyongeza.

Mimi sikuuliza nyumba ya Kariakoo wala Muyuni yeye moja kwa moja alishafahamu nyumba za Sebleni ndio kunakokaa wazee na hiyo mbali mbali ndio huko kwa wazee. Sasa sijui hili jawabu alilokuja kujibu hapa kati ya tofauti ya kijiko na upawa.

Kamati yangu nilipokuwa nayo ikiongozwa na Makamu Mwenyekiti, Mhe. Hija Hassan Hija na Mwenyekiti Amina Iddi Mabrouk, walishuhudia nyumba ya Limbani wakilia na usafiri angalau vespa moja tu na huu karibu mwaka wa tatu. Je, suala hilo mpaka leo linasubiri bajeti ya usafiri wa vespa kuwahudumia wananchi wale. Ni lini watatafuta njia ya kutafuta vespa hiyo moja kumkabidhi mtu anaewalea wazee wale.

**Mhe. Waziri wa Uwezeshaji, Ustawi wa Jamii, Vijana, Wanawake na Watoto:** Mhe. Naibu Spika, hapa hapana mwiko wala kijiko, siku yoyote tutakayopata tutawanunulia wale wahuduma wa nyumba ya wazee Sebleni na Limbani na Waziri wa Fedha kwa bahati nzuri analisikia hilo, wakati wowote tukipata pesa tutafanya kazi hizo.

**Mhe. Subeit Khamis Faki:** Nakukushukuru sana Mhe. Naibu Spika, kwa kunipa fursa nimuulize Mhe. Waziri swali la nyongeza.

Kwanza namshukuru sana kwa majibu yake mazuri anayojibu. Lakini namuuliza Mhe. Waziri kwa kuwa amesema kama wazee wetu waliokuwepo Sebleni, Limbani na waliokuwepo sehemu nyengine wanashughulikiwa vizuri sana na Serikali ya Mapinduzi ya Ummoja wa Kitaifa iliyokuwepo madarakani. Sasa napenda nimuulize Mheshimiwa. Kwa kuwa wakati umefika sasa wa kuwashughulikia wazee wetu na kila siku tunapitisha sera na sheria za kuwasaidia wazee wetu, kuna wazee wengi ambao wamo katika mitaa na hali yao sio nzuri sana hawajiwezi.

Mhe. Naibu Spika, ni lini serikali kupitia wizara yake itawaratibu wazee hawa ili kuongeza tena wazee wengine ambao watasaidiwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kupitia Wizara yake iliyokuwepo madarakani.

**Mhe. Waziri wa Uwezeshaji, Ustawi wa Jamii, Vijana, Wanawake na Watoto:** Nashukuru Mhe. Naibu Spika, kwa suala zuri na la maana sana la Mhe. Subeit aliloniuliza. Mhe. Naibu Spika, sasa hivi tunawahakiki wazee wote waliokuwepo katika Wilaya zote za Unguja na Pemba, ili tujue wapi kuna mzee aliyekuwa hana mtu wa kumsaidia wa kumshughulikia.

Lakini suala kubwa tunasema siku zote tushughulike na wazee wetu ndio waliotuzaa, wakatulea, wakahangaika, njaa, tabu, jua, mvua mpaka tukafikia hapa, tusiingojee serikali tu. Lakini tumo katika utaratibu na *Inshallah* Mungu akipenda pengine kabla ya kumaliza kipindi hichi cha mwaka 2015 mambo yetu yatakuwa mazuri tutawasaidia wazee.

**Nam. 16**
**Kutoweka Kwa Magazeti na Viwanda vya**
**Uchapishaji Zanzibar**

**Mhe. Salim Abdalla Hamad (Kny/Mhe. Saleh Nassor Juma) -** Aliuliza:-

Katika miaka ya mwishoni mwa 1950s na mwanzoni mwa 1960s, Zanzibar ilikuwa na magazeti mengi yakiwemo, KWELI IKIDHIHIRI UONGO HUJITENGA, ZANZIBAR KWETU na kadhalika. Kwa kuwa magazeti yote haya wahariri wake wakuu walikuwa ni wazalendo wa nchi hii akiwemo marehemu Mtoro Rehani Kingo na magazeti haya yalikuwa yakichapishwa hapa hapa Zanzibar.

(a) Kwa nini magazeti hayo yalipotea na hivi sasa Zanzibar haina magazeti mengi kama ilivyokuwa hapo zamani.

(b) Je, ni sababu gani za msingi zilizopelekea kuwepo kwa gazeti moja tu ambalo kwa sasa linamilikiwa na SMZ lichapishwe Tanzania Bara, huku Zanzibar tukiwa na kiwanda cha kisasa cha Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali ukilinganisha na hicho cha miaka ya nyuma.

**Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo -** Alijibu:-

Mhe. Naibu Spika, nakushukuru na naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 16 lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, kwanza nataka kuweka kumbukumbu sawa kwa kufahamisha kwamba gazeti la **"Kweli Ikidhihiri Uwongo Hujitenga"** lilianza kuchapishwa 24 Oktoba 1970 na lilisita kuchapishwa mnamo mwaka 1974. Gazeti hili lilikuwa linamilikiwa na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar na gazeti la **"Afrika Kwetu"** na sio **"Zanzibar kwetu"** lilianza kuchapishwa 1948 na mhariri wake alikuwa marehemu mstahiki Mtoro Rehani Kingo. Baada ya Mapinduzi marehemu mstahiki Mtoro Rehani Kingo alikuwa Meya wa Mji wa Zanzibar. Baada ya kutoa maelezo hayo sasa naomba kujibu swali lake Nam. 16 lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo.

(a) Mhe. Naibu Spika, magazeti mengi yaliyokuwepo katika miaka ya 50s na mwanzoni miaka ya 60s yalisita kuendelea kuchapishwa mara baada ya Mapinduzi ya mwaka 1964. Sababu kubwa ni kwamba wengi miongoni mwa wahariri na wamiliki wa magazeti hayo walipata nafasi ya kutumikia Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar akiwemo Mhe. Mtoro Rehani Kingo aliyekuwa akimiliki gazeti la "Afrika kwetu".

Mhe. Naibu Spika, magazeti mengine yaliendelea kuchapishwa hadi mwaka 1968 baada ya kutangazwa sera mpya ya kiuchumi iliyoweka hatamu zote za njia kuu za uchumi kuwa mikononi mwa Serikali. Viwanda vya uchapishaji vilitaifishwa na wamiliki na wasomaji wake wengi walihama nchi. Aidha baadhi ya magazeti yalisita kuchapishwa kutokana na kukosa wasomaji wake kwa sababu ya kuhama nchi.

Kuhusu Gazeti la "Kweli ikidhihiri Uwongo Hujitenga" lilisita kuchapishwa mnamo mwaka 1974 kutokana na ukosefu wa watendaji wenye ujuzi na nguvu kazi pamoja na mashine za kuchapia kwa wakati huo. Itakumbukwa kwamba hadi mwaka 1974 mitambo ya kuchapia magazeti humu nchini ilibakia minne iliyokuwa ikimilikiwa na kiwanda cha uchapishaji cha mchapishaji mkuu wa serikali nayo ilikuwa chakavu. Hivyo, ilishindwa kumudu kuendelea na kuchapisha gazeti hilo la kila wiki.

(b) Zipo sababu tatu kubwa za gazeti liliopo la "Zanzibar Leo" kuchapishwa Tanzania Bara licha ya kuwepo kiwanda cha Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali. Sababu hizo ni pamoja na:-

i. Kiwanda cha Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali bado hakina mitambo ya kuchapia magazeti ya kila siku.

ii. Sasa hivi magazeti ni sehemu ya biashara. Hivyo, kwa utaratibu uliopo magazeti ya Serikali yanapaswa kuwa na viwanda vya kuchapishia ikiwa ni sehemu ya kitega uchumi cha magazeti hayo na ndiyo maana kutokana na sababu hizo, Wizara hivi sasa inatafuta uwezekano wa Zanzibar Leo kama shirika la gazeti kuwa na Mitambo yake.

**Mhe. Salim Abdalla Hamad:** Mhe. Naibu Spika, kwanza nimpongeze Mhe. Waziri kwa majibu yake mazuri. Lakini tendo la kupata habari ni la muhimu kwa kila raia wa nchi yoyote na habari kutoka sehemu tofauti za mtazamo ni muhimu sana ili wasomaji na wasikilizaji waweze kufafanua. Kwa sababu hiyo wenzetu wa Tanzania Bara wanayo aina nyingi tafauti kubwa sana ya magazeti na hapa kwa vile kulikuwa na baadhi ya magazeti yakafungiwa.

a) Swali langu liko hapa. Je, ni kweli hapa Zanzibar baada ya gazeti hili moja la serikali liliopo hakuna watu ambao wanaweze wakatengeneza haya magazeti kwa gharama zao, watu binafsi kama ilivyo katika nchi nyengine, ili Wazanzibari wakaweza kupata mtazamo kutoka sehemu tofauti.

b) Nakumbuka kulikwua na gazeti moja hapa zuri sana la Dira na likafungiwa na serikali bila ya aliyekuwa akilihudumikia kupelekwa Mahakamani kama alifanya kosa.

Swali, je, kwa nini serikali ikawa inashadidia kufunga magazeti mengine ili ibakie na lake tu la kiserikali, wakati nchi hii ni nchi yenye mfumo wa vyama vingi.

**Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo:** Mhe. Naibu Spika, serikali inawakaribisha Wazanzibari wakati wowote ule na hata miongoni mwao Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi wakiwa na uwazo wa kifedha waje wafuate utaratibu, waombe kibali kwa mujibu wa sheria wataweza kuanzisha gazeti wakati wowote ili Wazanzibari wapate uhuru wa kusoma magazeti.

Kwa hivyo, uhuru huo bado upo, Mheshimiwa Mwakilishi mwenyewe akiwana na uwazo basi ajikusanye na wengine atafute wahariri na waandishi wazuri, anzishe gazeti lake wakati wowote tunakaribisha, atafuata uratibu, atapewa masharti kwa mujibu wa sheria ataanzisha. Kwa hivyo, hili halina tatizo na sisi tunarekebisha hilo.

Kuhusu suala la gazeti la Dira ni kweli lilifungiwa wakati huo na bado nafasi ipo kwa waliofungiwa gazeti wakati huo. Waangalie walifanya makosa gani kama wamejirekebisha basi bado nafasi ipo, wafuate utaratibu, waje wizarani au tutawepeleka katika taasisi inayohusika Idara ya Habari Maelezo, atafuata utaratibu ama watafungua gazeti kwa jina la Dira au kwa jina jengine ruhusa ipo.

Mhe. Naibu Spika, hayo ndio majibu yetu.

**Nam. 31**

**Safari za Mafunzo kwa Viongozi na Watendaji China.**

**Mhe. Jaku Hashim Ayoub:** Aliuliza:-

Viongozi na watendaji wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar wamekuwa na ziara za mafunzo kwa muda mrefu nchini China kwa nia ya kuwajengea uwezo na uwajibikaji, matarajio ya safari hizo ni kuona kuwa watendaji na viongozi wanaorudi wanaleta tija ya mafunzo wanayoyapata huko kwa kuongeza ufanisi na uwajibikaji pamoja na kutoa huduma bora kwa wananchi.

(a) Ni viongozi na watendaji wangapi ambao wamenufaika hadi sasa na safari hizo za mafunzo tangu kuanza kufanyika nchini humo.

(b) Vigezo gani vinatumika katika kuwapatia watendaji na viongozi wanaotakiwa kwenda kwenye mafunzo nchini China.

(c) Je, gharama za usafiri na fedha za kujikimu zinagharamiwa na nani na kama ni serikali, kiasi gani cha fedha kimeshatumika tangu kuanza kwa mpango huo.

**Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Kazi na Utumishi wa Umma –** Alijibu:-

Mhe. Naibu Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mheshimiwa Mwakilishi swali lake nambari 31 kama ifuatavyo:-

Mhe. Naibu Spika, kabla ya kujibu swali hilo, naomba kwanza kutoa maelezo yafuatayo:-

Mhe. Naibu Spika, ni kweli kwamba viongozi na watendaji wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar wamekuwa wakishiriki ziara za mafunzo ya muda mfupi na muda mrefu nchini China, kwa nia ya kuwajengea uwezo wa kiutendaji. Kwa jumla, Programu hizi za mafunzo nchini China zimekuwa zikiratibiwa na Wizara zetu mbili za

Serikali ya Mapinduzi Zanzibar na Wizara ya Fedha ambayo inaratibu Mpango Maalum wa Mafunzo nchini China kwa Viongozi na Ofisi ya Rais, Kazi na Utumishi wa Umma ambayo inashughulikia mafunzo mengine mbali mbali ya watendaji.

Mhe. Naibu Spika, miongoni mwa matarajio ya safari hizo ni kuona kwamba watendaji na viongozi hao wanaongeza tija katika Taasisi zao kutokana na mafunzo waliyoyapata, kwa kuongeza ufanisi na uwajibikaji katika kutoa huduma bora kwa wananchi.

Mhe. Naibu Spika, baada ya maelezo hayo naomba sasa nimjibu Mheshimiwa Mwakilishi swali lake kama ifuatavyo:-

a) Mhe. Naibu Spika, kama nilivyoeleza kabla, Ofisi ya Rais, Kazi na Utumishi wa Umma inajukumu la kuratibu mafunzo kwa watumishi wote wa umma katika ngazi mbali mbali. Kwa upande wa mafunzo ya muda mfupi na muda mrefu nchini China, watumishi mbali mbali wamenufaika kama inavyoonekana hapo chini nitapoeleza.

| MWAKA | MAFUNZO MAFUPI | MAFUNZO MAREFU |
|---|---|---|
| 2011/2012 | 12 | 5 |
| 2012/2013 | 72 | 2 |
| 2013/2014 | 79 | 2 |
| 2014/2015 | 40 | 0 |
| SUBTOTAL | 203 | 9 |
| GRAND TOTAL | | 212 |

b) Mhe. Naibu Spika, miongoni mwa vigezo vinavyotumika katika kuwapata watendaji na viongozi wanaotakiwa kwenda kwenye mafunzo nchini China ni pamoja na sifa za uzoefu wa kazi. Kiwango cha elimu, uhusiano wa kazi anazofanya na mafunzo anayoomba pamoja na uwezo wa kuzungumza Kiingereza. Kiutaratibu ili ombi la muombaji liweze kushughulikiwa, basi lazima lifuate taratibu za kiofisi ambazo ni pamoja na kuwasilisha barua ya ruhusa kutoka kwa muajiri wake.

c) Mhe. Naibu Spika, kwa ujumla gharama zote za kuendesha mafunzo hayo hugharamiwa na Serikali ya Watu wa China, kwani huu ni Mpango Maalum wa Kusaidia na kujenga mahusiano mazuri kati ya nchi za Afrika na China. Kwa upande wa Taasisi husika, hutakiwa kumpatia mhusika posho kwa mujibu wa taratibu na Kanuni za Utumishi wa Umma kwa mwaka 2014.

Mhe. Naibu Spika, katika hali hiyo haitakuwa rahisi kwa haraka kujua gharama halisi za fedha za Serikali zilizotumika, kwa vile kila Taasisi inasimamia bajeti yake ya mafunzo. Kwa ufafanuzi zaidi kuhusu Takwimu za Mafunzo nchini China, tafadhali rejea vitabu vya bajeti ya Ofisi ya Rais, kazi na Utumishi wa Umma kwa mwaka 2011/2012 – 2014/2015.

**Mhe. Jaku Hashim Ayoub:** Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, pamoja na majibu ya Mhe. Waziri naomba kuuliza swali dogo sana la nyongeza.

Mafunzo hayo lengo lake kubwa ni kuleta ufanisi na tija katika mamabo ya uwajibikaji kwa wandaji wakuu na watumishi wa umma. Ni tija gani imepatikana hadi hivi sasa tokea kuanza kwa programu hizo.

**Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Kazi na Utumishi wa Umma:** Naomba kidogo Mhe. Naibu Spika, arejee swali lake.

**Mhe. Naibu Spika:** Anasema hivi, kutokana na hayo mafunzo waliyopata huko kwa hao waliokwenda China, je, kuna tija gani iliyopatikana na serikali.

**Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Kazi na Utumishi wa Umma:** Mhe. Naibu Spika, lengo ni kuleta ufanisi katika utendaji wa kazi. Sasa ni mapema mno kutoa tathmini sasa hivi, hili jambo linataka lifanyiwe tathmini ya kutosha. Lakini pia, ni vizuri kila Mkuu wa taasisi akafanya tathmini kwa watendaji waliokwenda huko, je, wamebadilika au wako vile vile.

Kwa sababu wakati mwengine nilikuwa namtania, simtanii namwambia kwamba kuna dereva fulani alikwenda mafunzo ya kuendesha gari Dar-es-Salaam, basi aliporudi naona ana mambo ya kiajabu ajabu. Nikamuuliza haya ndiyo mafunzo uliopata kule Dar-es-Salaam, umefundishwa hivi. Akasema sikufundishwa hivi. Nikamuuliza sasa kwa nini unafanya hivi? Akasema imetokezea tu bahati mbaya.

Kwa hivyo, wakati mwengine yale mafunzo nafikiri yanasaidia, wakati mwengine nadhani yanawa-*confuse* baadhi. Sasa ni vizuri tukafanya tathmini sisi wenyewe kwenye taasisi zetu ili sisi Wizara yetu ya Kazi na Utumishi wa Umma tukapata *feedback* na kuweza kurekebisha zile kasoro. Pale ambapo panahitajiwa kuchukuliwa hatuwa tukachukua hatua za kufaa. Ahsante.

**Mhe. Hija Hassan Hija:** Mhe. Naibu Spika, baada ya majibu mazuri sana ya Mhe. Waziri naomba nimuulize maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo:-

Mhe. Naibu Spika, Mhe. Waziri amekiri kwamba wafanyakazi au watumishi wa umma 212 kwa ujumla wake wamepata mafunzo mbali mbali nchini Chini. Pia, amekiri kwamba sehemu ya safari hizo ni mchango wa serikali na sehemu ni mchango wa nchi ya China.

a) Naomba kutaka kujua, je, kama nitahitaji ripoti ya mafunzo hayo Wizara yake watakuwa nayo kwa kila mfanyakazi.

b) Hivyo mabadiliko ya utendaji kazi wa miaka miwili ya nyuma kabla ya mafunzo hayo na utendaji kazi wa leo, hauonekani kama umebadilika. Haoni kwamba kuwapeleka wafanyakazi nchini Chini ni sehemu ya matembezi sio kusoma.

**Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Kazi na Utumishi wa Umma:** Mhe. Naibu Spika, mimi naamini kabisa kwamba hakuna mafunzo ambayo hayasaidii na Mhe. Hija Hassan Hija, labda yeye anavyo vigezo vya kuona tathmini ya kazi hizo na kama anavyo basi atusaidie ili tuvifanyie kazi na sisi. Lakini kwa kiasi fulani ninachosema watendaji wetu waliopata mafunzo kwenda China kwa asilimia kubwa basi wameleta mabadiliko makubwa katika utendaji wa kazi katika maeneo yao na hili wala tusiwe na machaka nalo.

Mhe. Naibu Spika, kiwango cha utendaji kazi katika mawizara yetu kwa kiasi fulani nasema, siwezi kusema asilimia 100, lakini kwa kweli kuna mabadiliko ya hali ya juu hivi sasa ukilinganisha na huko nyuma. Mafunzo haya yamesaidia, hawendi kutembea, wala hawendi kutalii kule China, bali wamekwenda kwa ajili ya mafunzo. Mimi nina imani kwamba fursa kama hizi sote tunapozipata basi tunakwende kwa lengo la kujifunza.

Nadhani hata sisi Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi tulipata fursa ya kwenda China vile vile. Sasa sidhani kama tulikwenda kutalii kule, tulikwenda kwenye mafunzo yake na nadhani yametusaidia tuliporudi wote tumeneemeka. Ahsante Mheshimiwa.

**Mhe. Naibu Spika:** Ahsante Mhe. Waziri maswali yamemalizika Katibu tuendelee.

**HOJA ZA SERIKALI**

**Mswada wa Kuanzisha Sheria ya Kupunguza na Kukabiliana na Maafa Zanzibar na Mambomengine Yanayohusiana na Hayo**

*(Majadiliano Yanaendelea)*

**Mhe. Naibu Spika:** Ahsante, Mhe. Waziri kwa kuwa michangio ilimalizika jana, kwa hivyo, tunaomba uje utoe majumuisho.

**Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais:** Mhe. Naibu Spika, kwanza naomba kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kutujaalia tena kukutana asubuhi ya leo tukiendeleza shughuli zetu za kawaida za Baraza letu tukufu nimshukuru yeye mola kutupa uwezo huo. Aidha, nichukuwe fursa hii Mhe. Naibu

Spika, nikushukuru wewe kwa kunipa nafasi ya kusimama mbele ya Baraza hili tukufu asubuhi hii hasa siku ya Ijumaa ya leo.

Aidha niwashukuru sana sana wajumbe wa Kamati ya Viongozi Wakuu wa Kitaifa kwa ushauri na maelekezo yao katika kufanikisha sheria hii. Aidha niwashukuru wajumbe wote waliochangia na wajumbe wote wa Baraza la hili kwa michango yao adhimu yenye nia ya kujenga kwa maana ya kuimarisha sheria hii ili tuwe na sheria bora na nzuri.

Aidha nimshukuru Mhe. Makamu wa Pili wa Rais kwa busara, hekima na uongozi wake katika Wizara yetu ambao kwa kiasi kikubwa umetuwezesha kufanikisha majukumu yetu na kuadimika ipasavyo. Mheshimiwa baada ya maelezo hayo kwa ruhusa yako naomba pia sasa niwatambue waheshimiwa wajumbe waliouchangia mswada huu.

Nianze na Mhe. Shadya Mohammed kwa niaba ya Mwenayekiti wa Kamati
Mhe. Makame Mshimba
Mhe. Ali Salum
Mhe. Fatma Mbarouk
Mhe. Mohammed Haji Khalid
Mhe. Abdalla Juma
Mhe. Abdalla Mohammed
Mhe. Salma Mohammed Ali
Mhe. Ismail Jussa Ladhu
Mhe. Suleiman Hemed
Mhe. Mgeni Hassan Juma
Mhe. Hija Hassan Hija
Mhe. Bikame Hamad Yussuf na
Mhe. Saleh Nassor Juma

Mhe. Naibu Spika, hao ndio waheshimiwa ambao wameichangia kwa umakini mkubwa mswada huu wa sheria ya kukabiliana na maafa. Mheshimiwa michango yao na ushauri wao kwa ujumla tumeupokea kwa sababu nilijua ni mchango ambao msingi wake ni kujenga na kuifanya sheria iwe nzuri zaidi.

Aidha niwapongeze sana wale waliofanya baadhi ya marekebisho kwa nia ya kuiboresha sheria hii na hasa hasa niipongeze sana Kamati kwa kufanya marekebisho na amewasilisha jadueli ambalo alilonalo kufanya marekebisho katika Sehemu ya Kwanza, Sehemu ya Pili ya kuanzishwa kwa Kamisheni, vile vile katika Sehemu ya Tatu kuanzishwa kwa Kamati inayofanya marekebisho ambayo sio makubwa sana vile vile katika Sehemu ya Nane.

Lakini rekebisho kubwa ambalo kamati hii ililifanya lilitokana na lile kosa ambalo lilifanyika katika uchapishaji kwa maana ya kuongeza kifungu cha 48 ambacho kinasomeka kama ifuatavyo.

Mhe. Naibu Spika, naomba kusoma;

"Sheria ya Usimamizi wa Maafa namba 2 ya mwaka 2003 inafutwa".

Kifungu cha 2;"Bila ya kujali sheria iliyofutwa, kwa mujibu wa kifungu kidogo cha kwanza cha kifungu hiki, jambo lililofanywa au lilichukuliwa hatua kwa mujibu wa sheria iliyofutwa litakuwa limefanywa kwa mujibu wa masharti ya sheria hii".

Mhe. Naibu Spika, hii ni hoja ilizungumziwa sana na Mhe. Jussa, lakini majibu yake ni kwamba licha ya kwamba katika ile Rasimu ya kiingereza neno hili lilikuwemo, lakini kutokana na makosa yaliyofanyika katika Rasimu ya kiswahili katika Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali la kutokuingiza kifungu hiki, bahati nzuri Kamati ya Viongozi Wakuu wa Taifa waliingiza na tunakubaliana na hiki kifungu kama alivyorekebisha.

Mhe. Naibu Spika, kuhusu hoja ya tarehe, ni kweli mswada wetu huu ulionesha tarehe 30 Disemba, lakini hii ilitokana kwamba katika Gazeti Rasmi la Serikali lilichanganywa miswada ya aina mbili. Ile miswada iliyokuja kwa hati ya dharura na ile miswada iliyotakiwa kutimizwa kwa masharti ya Kanuni ya 79 ya kutangazwa kwa siku 21.

Kwa hivyo, ndio maana ikaja kwenye tarehe zile kutokana na suala zima la kuchukua miswada yote miwili kwa pamoja.

Mheshimiwa, mswada wenyewe ulikuwa unajieleza kuhusu madhumuni ya kukabiliana na maafa hapa Zanzibar. Ukitizama sheria hii nia yake na madhumuni yake ni kutokana na hali halisi ya kukabiliana na maafa hapa Zanzibar, lakini pia, kutokana na michango ya siku nyingi, mashauri na maelekezo mbali mbali tuliyopata kutokana na Baraza hili tukufu. Kwa hivyo, ndio maana sheria tukawa tunaifatilia iweze kuwepo kama sheria na iweze kufanya kazi.

Kwa hivyo, madhumuni makubwa ya mswada huu ni kuondoa mapungufu yaliyojitokeza katika sheria ile namba 2 ya mwaka 2003. Na moja kubwa ilikuwa ni suala zima la kuleta uwiano wa sera na sheria yenewe. Maana tulikuja sera mpya ambayo ilikwenda na wakati, kwa hivyo, ilibidi sasa sheria yetu irekebishwe ili iendane na sera...

**Mhe. Naibu Spika:** Waheshimiwa, mnaotoka msichelewe tunataka tupitishe vifungu. Endelea.

**Mhe. Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais:** Lakini vile vile ulikuwepo umuhimu wa kuweka muundo mzuri wa usimamizi wa shughuli za maafa ulihitajika kabisa urekebishwe kutokana na sheria ilivyokuwa na hasa hasa kuanzia ngazi ya shehia na Wilaya pamoja na Taifa ili kuweka mpango mzuri wa kujikinga, kujiandaa na kurejesha hali baada ya maafa, ndio msingi mkubwa. Kwa sababu ile tuliyokuwa nayo ilikuwa sana imeelekeza zaidi katika uokozi.

Sasa sheria hii imebidi iaone masuala mazima ya kujiandaa ambao ulikuwa ni ushauri mkubwa wa Baraza hili, kujikinga na kurejesha hali baada maafa, mambo makubwa kwa msingi wa *preparedness, motivation and post desaster recoverage.* Kwa hivyo, huo hasa ndio ulikuwa sheria hii imezidisha kuweka msingi.

Lakini moja likiwa limezungumzwa sana na Baraza hili ni suala la kushirikisha sekta binafsi, kwa hivyo, hii sheria sasa ya ushiriki wa sekta binafsi utakuwepo katika suala la sheria na kilio kikubwa cha Baraza na wananchi kwa jumla ilikuwa suala la kuanzisha mfuko wa maafa. Sasa japokuwa katika sheria iliyopita ilikuwa inaelezea neno "mfuko" lakini halikuwekwa vizuri kisheria na utekelezaji wake.

Leo katika sheria hii sasa kutaanzishwa mfuko wa maafa ili kusaidia kukabiliana na maafa na kwa msingi huo basi ili kuweko na mfuko ambao wajumbe wengi katika michango yao walieleza nia yake itazidisha suala zima la uokozi, itaimarisha kuwa na vifaa vya kisasa, taaluma na vile vile kuelimisha na mafunzo mbali mbali.

Kwa hivyo, msingi huo pia utasaidia yale mawazo makubwa ambayo waheshimiwa walikuwa wanazungumzia hapa kuhusu suala zima la misaada ya dharura kwa binaadamu. Kwa hivyo, unapokuwa na mfuko maana yake unatuwezesha kwa wakati wowote kuweza kutoa misaada mbali mbali. Kwa hivyo, kwa ujumla dhamira ya mfuko kama walivyoeleza waheshimiwa imejieleza ndani ya sheria hii na nia yetu ni hiyo ili kuimarisha kwa sababu tunajua kabisa uwezo wa nchi peke yake kwa kutumainia bajeti haukidhi haja halisi ya mahitaji ya mambo yanayohusu mambo ya masuala ya maafa.

Kwa hivyo, mfuko tunategemea utasaidia zaidi katika kuimarisha yale mengi ambayo leo yamekuwa ni changamoto kwa upande wetu.

Mhe. Naibu Spika, katika maelezo ya wajumbe moja ambalo lilikuwa limezungumzwa sana hapa lilionesha sura sura ya posho, wajumbe wengi walidhani Kamisheni, Kamati za Kitaifa, Wilaya na Kishehia, wakidhani zinapokaa kuna masuala ya posho. Hakuna posho katika vikao vyote hivi, hivi ni vikao vya kujitolea ni vikao vinavyohusu kunusuru maisha yetu wananchi, ni vikao vinavyokaa kujadili mambo ya kukabiliana na tatizo lililo mbele yetu la dharura.

Kwa hivyo, ukubwa wake na udogo wake si dhana kwamba watu wanataka kupeana posho tukafanya ile kubwa, ukubwa tumeweka kwa sababu maalum ambazo mimi nitazieleza. Lakini kwenye vikao hivi havina posho, hakuna kikao hata kimoja chenye posho hapa. Hapa ni vikao muhimu vya kuhakikisha kwamba tunanusuru au tunajinusuru maisha yetu, maana hujui nani atakumbwa na maafa ama na tatizo linalotokana na maafa.

Kwa hivyo, cha msingi hapa ningependa Baraza hili lielewe kwamba vikao hivi ni vya kujitolea havina posho na hata hapo nyuma tulipokuwa tukikaa kwenye ukubwa wa namna hiyo hiyo hakukuwa na posho na watu walikuwa *commited* na walikuwa *serious* kutafuta ufumbuzi wa tatizo linalokuwa mbele yetu.

Kwa hivyo, ile hoja iliyojitokeza kwamba muundo wa Kamisheni ni mkubwa sana, watu wengine wakasema watu wanajitafutia miradi, hakuna mradi hapa hakuna hela unayoipata, hapa kuna kazi ya kuja kufanya ya kushauri linapotokea tatizo kulitatua tatizo.

Kwa hivyo, kwa nini muundo unakuwa mkubwa, kwa sababu suala la maafa ni suala la MTAMBUKA linagusa sekta zote, kwa hivyo, msingi wake ni kushirikisha wahusika wote ili tukabiliane jambo hili kwa pamoja, watu wamesema mawaziri wote ndio, wana wajibu jambo kubwa limekuta nchi, lazima mawaziri wawajibike na wale wote wahusika wanaohitajika kuwepo wawepo kwenye ile Kamisheni na lilitokea suala hii Kamisheni itakaa mara ngapi.

Hii Kamisheni haina vikao maalum vya kukaa kwa mwaka, Kamisheni hasa inatakiwa ikae pale wakati wa dharura imetokea, lakini itakutana kama kuna uhitaji wa kukutana wa kuitishwa na Mwenyekiti ama tukiamua kufanya hivyo kwa sababu Kamisheni ndio inayotoa *policy* na miongozo ya namna ya kukabiliana na maafa. Sasa kwenye masuala ya kujiandaa inaweza kuitishwa kikao hiki tukakutana kujadili namna nzuri ya kukabiliana na maafa.

Kwa hivyo, hakuna vikao maalum vilivyowekwa kwamba Kamisheni itakutana mara ngapi kwa mwakza au nini, ni suala ambalo tutakutana kwa sababu tunajua tunao wajibu wa kufanya hivyo wa kunusuru maisha ya watu kunusuru mali na kadhalika. Kwa hivyo, ndio suala zima la kukutana.

Na kuwepo kwa ukubwa wa muundo hii inaonesha sasa *commitment* na *seriousness* ya Serikali katika kushughulikia masuala ya maafa kwa nia ya kila muhusika awajibike katika kufanya jambo hili na tayari tuna uzoefu kama nilivyosema kwamba vikao hivi tumefanya kabla ya hapo kwenye idadi hiyo hiyo. Sasa msingi mkubwa ni kuwahusisha wote wanaohusika ili kufanyakazi ya kunusuru maisha ya watu, kunusuru mali zetu, kufanya kila litakalowezekana ikiwezekana kujiandaa vizuri ili kama kuna tatizo lisiweze kutokea ama kulipunguza.

Lakini kubwa ni kwamba Kamisheni itakaa kwa maana ya kutoa ushauri kwa namna ya kujikinga, namna ya kujiandaa, namna ya kurejesha hali baada ya maafa na namna nzima ya uokozi pale ambapo tatizo limetokea.

Kwa hivyo, baadhi vile vile ya wajumbe walizungumzia suala la kuimarisha zana vifaa na maghala, kutoa elimu, mafunzo na kadhalika. Nia yetu mfuko usaidie katika shughuli kwa sababu tunaelewa kama walivyosema wajumbe kwamba ule uwezo wa kibajeti hauwezi kutosheleza mahitaji yote. Kwa hivyo, Mhe. Abdalla, hata lile suala la *fund* maalum ni huo mfuko wenyewe, nia yetu tuwe na mfuko usaidie tuepukane na matatizo ambayo yangeweza kutokea.

Na kuna wenzetu wengine hapa walizungumzia sana suala la kuwa na magari ya zimamoto haya kwa msingi wake ni kwamba pale inapotokea maana ajali zetu za mara kwa mara Zanzibar zilizotokea za zimamoto, kwa hivyo, msingi wake walitaka magari ya zimamoto yawepo na yawe na maji na wengine wakashauri vile vituo vya maji vya ile mifereji ya kusimama viweze kutoka maji na maji yawepo. Ushauri huo tunaupokea tutaufanyia kazi kwa kushirikiana ndani ya Serikali ili kila kasoro ambayo inajitokeza tuweze kuipatia ufumbuzi, nia ni kuwa na uwezo mzuri wa kuweza kukabiliana na matatizo hayo ya maafa.

Lilijitokeza suala la kwamba kwa nini baadhi ya vikosi vyetu vya SMZ wakuu wake hawakushirikishwa katika Kamisheni. Nataka nitamke kwamba ushauri ule tumeupokea na sasa katika vifungu vyote vile tutawaongeza wale ambao hawakuingizwa pale mwanzo, kwa maana ya Mkuu wa Kikosi cha Valantia sasa atakuwa mjumbe, Mkuu wa Kikosi cha Mafunzo sasa atakuwa mjumbe na vile vile Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la bandari naye atakuwa mjumbe kwenye Kamisheni.

Kwa hivyo, utaratibu huo sasa utafanya ule ushauri ambao ulitolewa na Waheshimiwa Wajumbe tunakubaliana nao ili uwemo kwenye sheria kwa msingi ya kile kifungu cha 4(3) kutakuwa na (k), (j), (l) na (m) ili kuhakikisha kwamba wale wote ambao tumewazungumza basi wanakuwemo katika sheria kwa kuhakikisha kwamba na wao wamo kama ilivyoshauriwa. Kwa hivyo, ushauri tumeupokea na tumeufanyia kazi.

Vile vile, kwa upande wa Kamati za Wataalam, kwa upande wa Kamati za Wataalam wale maafisa wa utawala Vikosi vya Valantia na Afisa Mkuu wa Utawala katika kikosi cha kujenga uchumi pamoja na Afisa Mkuu wa Kikosi cha Mafunzo na Naibu Mkurugenzi wa Mamlaka ya Hali ya Hewa, sasa na wao wataingia kwenye ile Kamati ya wataalam pamoja na Kamanda wa Wilaya na Naibu Mkugenzi wa Mamlaka ya Hali ya Hewa, hao sasa wataingia katika ule utaratibu wa *composition* ya Kamati ya Wataalam katika ngazi ya Taifa kama ambavyo ilishauriwa.

Lakini vile vile tunakubaliana na lile shauri la kuongeza wale makamanda katika Wilaya kwa maana Kamanda wa Jeshi la Kujenga Uchumi, Kamanda wa Kikosi cha Mafunzo, Mwakilishi wa Kikosi cha KMKM na Mwakilishi wa Afisa wa Utawala wa JKU hao nao sasa kwenye ile ngazi ya Wilaya watakuwa ni wajumbe wale Wakuu wa Vikosi katika Wilaya watakuwa ni wajumbe katika ile Kamati ya Wilaya inayoongozwa na Mkuu wa Wilaya, lakini vile vile watakuwa wale wahusika wengine kwenye Kamati ya Wataalam kama walivyo wenzao watakuwa wanaingia kule kwenye Kamati ya wataalam katika ngazi ya Wilaya. Kwa hivyo, msingi wake ule ushauri ambao ulitolewa hapa na wajumbe tumeupokea.

Lakini vile vile suali la Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi na Wabunge wasiwemo katika ngazi ya shehia na badala yake wabakie kule ngazi ya Wilaya, ushauri ule pia tunaupokea na sasa basi katika ngazi ya shehia watakuwemo Madiwani. Kwa hivyo, yale yote ambayo waheshimiwa mlitaka yafanyiwe marekebisho tumefanya hivyo na bahati nzuri mkipata hii taarifa ambayo waliwasilisha Kamati yetu ina maelezo ya kutosha kwenye suala hili na wakati tukihitajika masuala mengine tutatoa ufafanuzi wakati tukipitisha kifungu kwa kifungu.

Mheshimiwa kwa ujumla yale mashauri ambayo Baraza hili Tukufu lilitushauri tumekubaliana nayo.Vile vile, kuna kile kifungu cha 43 ambacho kinahusu suala la mtu ambaye kukataa kutoa taarifa, sasa kile tunakifanyia marekebisho ili ionekane mtu ambaye anakataa kwa makusudi kutoa taarifa, nafikiri sasa kifungu hicho kitakuwa kinasomeka vizuri ili kusikiliza ushauri wa wajumbe kwa msingi wa kuondosha ile dhana ya mtu ambaye asije kutiwa hatiani wakati hakukusudia kutenda kosa.

Kwa hivyo, ni kwa wale ambao ukiongoza neno hili "kwa makusudi" nina hakika itakuwa tumeweka usawa katika sentensi ile na msingi huo utasababisha kifungu hicho kiwe kizuri zaidi.

Sasa lipo moja lilizungumzwa sana, kifungu cha 6 (f) cha suala la kukataa kupokea huduma zinazotolewa, hili liliulizwa sana.

Mhe. Naibu Spika, tunapofanya haya nia yetu ni kunusuru maisha ya watu wetu pamoja na sisi sote hapa. Ziko huduma nyengine lazima zitolewe ili kusiathiri maisha ya mtu mwengine. Kwa mfano, Mwenyezi Mungu atunusuru sana isitokee Ebola nchini kwetu, lakini huko kwa wenzetu kuna watu wanakataa hata ule utaratibu wa kupulizia dawa katika eneo lililoathirika. Sasa ikitokea jambo kama hilo hapa kwetu ni tatizo, ikitokea masuala ya kipindupindu watu walikuwa wanakataa katika maeneo yao vile vile kuchukuliwa zile hatua zinazofaa ili maradhi yale yasisambae kwa mwengine. Kwa hivyo, utaratibu ule tukiukatalia maana yake kunaweza kutupa athari kwa maisha ya watu wengine.

Lakini vile vile kukataa kutoa huduma inawezekana unamuona mwenzako amezama na wewe ni mtaalamu wa mambo yaku-*dive* na ukakataa kwenda kumuokoa au una vyombo; *life jackets* na mambo mengine vitakavyoweza kusaidia kuokoa maisha ya mtu na ukakataa kufanya hivyo. Sasa kibinadamu hapa Zanzibar watu hawa sio kuambiwa, kwa utaratibu wao, utu wao, na ubinadamu wa nchi yetu mara nyingi hujitokeza wenyewe na kusaidia vitu hivi. Lakini pale inapotokea kukataa na vitu vya dharura hivi,hii ni ule wakati wa dharura yanapotangazwa yale maafa yenyewe katika nchi, nchi inakuwa katika hali nyengine.

Kwa hiyo, yanapotokea wakati huo, ndiyo maana tukasema suala hili liwepo, kwa hiyo msingi wake ni huo na hauna maana nyengine; kwamba watu walazimishwe jambo wasiloliweza, aah, ni kwa mambo haya yafanyike kutokana na uwezo na ile hali halisi inayojitokeza wakati huo.

Mhe. Naibu Spika, suala jengine ambalo Waheshimiwa Wajumbe walilizungumzia ni ukaguzi wa fedha. Hii ni taasisi ya serikali itakaguliwa kama zinavyokaguliwa taasisi zote za umma, kwa hivyo utaratibu ni ule ule hakuna kificho, utaratibu utakuwa wazi, utakaguliwa kwa mujibu wa sheria zile za fedha na sheria zote za matumizi ya fedha. Kwa hiyo, hilo si tatizo.

Mhe. Naibu Spika, wengine waliulizia kwa nini hii Kamati ya Wataalamu isiwe kwa wataalamu wa maafa tu. Kamati ya Wataalamu hii msingi wake kama nilivyosema mwanzo mambo haya ni mambo mtambuka inawahusu watu wote. Sasa wakati Kamati ya Wataalamu hasa pale ukitizama kwa kiasi kikubwa inawashirikisha sana Makatibu Wakuu, maana yake Makatibu Wakuu wa Wizara hizi zote ni wajumbe kwenye kamati hii.

Msingi wake ni kwamba utampata mtu wa mawasiliano, mtu wa afya, mtu wa mazingira na wote wahusika wa jambo hili. Kwa hiyo, ukisema ni mtu mwenye *qualification* tu za maafa pengine kuna mawasiliano *qualification* yake ni mambo ya miundombinu. Sasa naye unamuhitajia au Mkurugenzi wa Bandari yeye *field* yake haijambo ni ya bandari, sasa ukimwambia lazima awe na utaalamu wa maafa ndio aende pale msingi wa dhana yenyewe haitopatikana, na badala ya kupunguza hayo maafa sasa wewe unakuwa chanzo cha kuongeza maafa. Kwa hivyo, huu ndio msingi wenyewe.

Vile vile iliuliziwa hapa Sekretarieti, sekretarieti ipo katika kifungu cha 8 na muundo wake ukitizama kifungu cha 9 unaeleza vizuri, na majukumu yake unayapata katika kifungu cha 10. Kwa hiyo, sheria yenyewe inaelezea suala zima la sekretarieti.

Vile vile tulishauriwa suala zima la *land use plan.* Kiukweli hili ni jambo la msingi sana,maana suala la mipango miji, kupanga miji yetu katika mazingira mazuri tukayaweka vizuri ni moja ambalo litasababisha kupunguza athari za maafa. Ni kweli mahala ambapo yamejengwa bila ya mipango, magari hayafiki moto ukitokea ni shida, magari ya *fire* hayafiki na kadhalika. Kwa hiyo, suala la kuheshimu *land use plan* ni jambo zuri na ushauri huo tunaupokea, lakini kwa kuwa kifungu cha 10 (f) kinatoa ushirikiano na taasisi nyengine katika sheria hii maana yake kinatuwezesha sasa kukaa na wenzetu ili kulifikiria zaidi suala hili muhimu la *land use plan* kwa maana ya mahitaji ya mipango miji.

Wenzetu wengine waliulizia hapa kuhusu suala la semina. Mhe. Naibu Spika, semina zilifanyika kwenye Baraza hili zinazohusu mpango ule wa kukabiliana na maafa. Tumefanya semina pale *Fisherman's Resort*, tukafanya semina nyengine mkakati wa mawasiliano wa maafa pale. Lakini sheria hii pia ilifanyiwa semina kwa wataalamu mbali mbali wakiwemo wataalamu wanafunzi wale wa vyuo vikuu, wana habari, asasi za kiraia, mashirika ya kimataifa yakiwemo ya *UNDP*, *UNICEF* yalikuwepo hapa Zanzibar, *WHO*, *WFP*, *Red Cross*, *Save the Children* na kamati mbali mbali za maafa za Wilaya na Shehia wamefanyiwa semina ya sheria hii.

Kwa bahati hatukuwahi kufanya kwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi, lakini kwa sababu msingi huko nyuma tulifanya semina inayohusu sera ya maafa katika Baraza hili, mpango kama nilivyosema wa kukabiliana na maafa, mpango wa mawasiliano ambao ukitizama mawazo yale ndiyo chanzo cha sheria hii, na baadaye nitaeleza kwa nini ilikuja kwa utaratibu huu wa hati ya dharura.

Mhe. Naibu Spika, sasa licha ya kufanya semina lakini na kabla ya sheria hii bado nilikuwa nina mpango maalum wa kutoa taaluma na mafunzo ya shehia mbali mbali. Hivi sasa tumefikia asilimia 70 ya shehia zilizopata mafunzo ya mpango wa kukabiliana na maafa, na tunaendelea kutoa taaluma kwenye vipindi mbali mbali vya redio na vile vile tumejaribu kukutana na wadau mbali mbali hasa asasi za kiraia kwa msingi wa kuelezana namna ya kukabiliana na maafa. Kwa hivyo, naamini kabisa jamii kwa kiasi kikubwa ina uelewa wa jambo hili na ina uelewa wa sheria iliyopo.

Wajumbe hapa walizungumzia sana suala la vifaa vya kukabiliana na maafa. Ushauri huo tunaupokea, kwa sababu ni kweli vifaa vya kisasa, vifaa bora kama vile boti, *helicopter* na vyengine ni jambo la msingi lakini linategemea sana na uwezo wa nchi, lakini ushauri ni wa maana na tunaupokea.

Mhe. Naibu Spika, kuhusu daraja za maafa ni kweli maafa yanatokana na majanga ya aina mbili. Moja ni majanga ya kimaumbile lakini mengine ni yale majanga ambayo yanasababishwa na binadamu. Lakini tukitaka tujue vizuri ukisoma kifungu cha 29 (1), 29 (2), 30-31 kinaeleza vizuri hizo *classification* za maaafa na naamini Waheshimiwa mumepitia na mumezielewa kwa kina. Lakini nikumbushe tu kwamba bado mfuko huu utakuwa na haja ya kutizama sana misaada ya kibinadamu itakayotokea wakati dharura mbali mbali, kwa hiyo suala hili tumeanza kulifanya na tutaendelea kulifanya.

Mhe. Naibu Spika, pia liliuliziwa suala la utetezi, maana yake hii nilikusudia *advocacy*, ni suala muhimu sana kufahamisha uma kuelewa masuala ya maafa. Ni suala zima la kutaalamishwa na asasi zetu za kiraia zinafanyia kazi

sana jambo hilo na baadhi ya wataalamu wetu na umuhimu wa kuwepo pale ni vyema ikaendelea kuwepo. Msingi wake ni kutetea umuhimu wa watu kuelewa dhana nzima ya kukabiliana na maafa, na hasa hasa kwa utaratibu wa sasa wa kujikinga na kujiandaa ili maafa yenyewe yasitokee.

Mhe. Naibu Spika, pia Wajumbe walionesha wasi wasi wakasema eeh hii Kamisheni inataka kwenda vitani mbona vikosi vingi, maaskari wengi. Siyo vitani, tunayo mifano hai kwamba kazi kubwa ya kukabiliana na maafa wanaifanya ndugu zetu askari, na wao wanazo zana na vyombo vya kutusaidia kufanya hivyo. Kwa hiyo, wao wanapokabidhiwa jukumu hilo wanatusaidia sana kwenye masuala ya uokozi na saa nyengine hutokea madaraja pia yakavunjika ikawa hakupitiki upande huu na huu wao ndio wanazo hizo zana kama za madaraja na kadhalika.

Kwa hivyo, jambo hili na nchi nyingi hasa ukizitizama moja kwa moja zinaongozwa na vikosi hivi mbali mbali katika kupambana na masuala ya kukabiliana na maafa. Ni jambo kubwa sana, kwa hiyo wenzetu hawa ndio hasa *commanding post* ya utekelezaji wakati wa dharura hiyo kubwa ya maafa.

Mhe. Naibu Spika, kwa nini Katibu Mkuu Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais anakuwa Katibu wa Kamisheni? Kwa sababu yeye ndiye mtendaji mkuu katika Ofisi ya Makamu wa Pili ya Rais, na Ofisi ya Makamu ya Pili wa Rais ndio yenye dhamana ya kuratibu shughuli hizi za maafa. Kwa hivyo, ile namna ya kuwa kiungo cha kuwasiliana *Commission*, Kamati ya Wataalamu, Sekretarieti yale maamuzi namna ya kuyafikisha kwa njia moja ama nyengine. Katibu huyu kuwa Katibu wa Kamisheni ina umuhimu wake katika utekelezaji wa yale maamuzi yatakayotolewa na zile *policy* zenyewe namna ya kuzitafsiri na kuziandika kuwapelekea wahusika wengine. Kwa hiyo ndio sababu hasa ya kwa nini tukawa nae Katibu Mkuu anayekuwepo pale ili kusimamia yale maamuzi na zile sera zitakazoamuliwa ili zifike kwa walengwa kwa utaratibu ulio mzuri.

Nini maana ya kusalimisha mali? Maana ya kusalimisha nia yetu ni mtu mwenye hiyo mali yake aweze kusaidia au awajibike kusaidia. Unaweza ukawa na chombo kama nilivyosema mwanzo gari ama boti na kadhalika ili uweze kusaidia. Pengine gari saa hiyo wako watu wameokolewa hapa katika hali kama ile ya maafa wanatakiwa wapelekwe hospitali uaghirishe ghafla wewe una gari yako umekataa. Sasa kumsalimisha kwake msingi wake ni huo kwamba kwenye wakati ule inapotangazwa nchi, sasa tuelewane wakati nchi inapotangazwa kuwa sasa imo katika hali ya maafa ndio kazi hii inafanyika, usije ukadhani kwamba kumetokea ajali hapo ni vizuri kufanya uungwana ukawasaidia, sasa hivi bado sheria haijatumika, ni pale ambapo nchi imekuwa *declared* kwamba sasa tuko katika hali ya maafa.

Kwa hiyo, ni vizuri kujenga imani na moyo wa kusaidiana, kwa hiyo hapa kikubwa ni namna gani tutawajibika kumsaidia mwengine. Kwa mfano hata madaktari kuna madaktari waliogopa kutoa matibabu kwa wagonjwa fulani fulani, lakini wakati kama huu ukifika huwezi kukataa lazima utafanya hiyo kazi. Kwa hiyo, ni mambo lazima yaongozwe na sheria.

Nini adhabu ya wale ambao wanasababisha majanga na maafa? Mhe. Naibu Spika, ziko sheria mbali mbali lakini hata ile sheria ya adhabu inaeleza mambo hayo lakini ziko sheria nyingi tu. Kuna sheria ya usafiri wa baharini inaeleza adhabu, sheria ya usalama barabarani, sheria za mazingira, sheria za misitu zote zimo ambazo zinaweka adhabu, lakini na hizo sheria za *penal code* ambayo inatoa adhabu kwa wale ambao watakuwa wamekataa kufanya hivyo.

Yuko mmoja alisema hatuoni tofauti kati ya serikali na kamisheni. Mhe. Naibu Spika, ni kwamba serikali mbali na kamisheni mbali, *of course* kamisheni ni chombo cha serikali kinachosimamia shughuli za maafa.

Tumeshauriwa suala zima la usimamizi wa sheria, ni kweli ipo *laxity* kwenye masuala ya usimamizi wa sheria. Naunga mkono kwamba suala hili ushauri tuupokee tuwe na namna nzuri wa utekelezaji wa sheria yenyewe, kwa sababu umuhimu wa sheria hii sote tunauelewa.

Sheria iweke mpango mzuri wa mawasiliano, upo mpango mzuri na mkakati wa mawasiliano katika suala zima la kukabiliana na maafa.

Mhe. Naibu Spika, bajeti bora kama nilivyosema nia ni kuwa na bajeti nzuri lakini itategemea sana uwezo wa serikali, lakini mfuko kwa kiasi fulani lengo lake kubwa ni kumudu hiyo *deficit* ambayo inaweza kutokea ili kusaidia kwa shughuli hizo.

Uteuzi wa wale wanaotokana na asasi zisizo za kiserikali ufanywe na wenyewe wahusika. Nia na dhamira siku zote inakuwa hivi; kwamba asasi zenyewe ndio zitapendekeza kwa Waziri majina hayo, naye Waziri baadaye ndio atatamka nani na nani awe mjumbe, lakini Waziri hawezi kujiripukia akafanya yake kichwani mwake, siku zote atakachofanya ni kuwasiliana na asasi hizo wamletee, na wamesaidia sana kwenye suala zima la *advocacy,* kwa hiyo ni wenzetu na tutaunga mkono ushauri wao.

Kuhusu suala la *gender.* Serikali imesikia na hatua mbali mbali zinachukuliwa kwenye kuleta uwiano katika *gender* na karibuni hivi mtakuwa *fifty fifty* (50-50), pitisheni Katiba Mpya tu. Serikali lazima iwe na umakini katika kuangalia mambo ya kukabiliana na maafa na ndio maana hata kwa ukubwa wa hiyo Kamisheni yote inatokana na umakini wa serikali katika suala zima la kukabiliana na maafa.

Suala la kuwa na kituo maalum cha utafiti wa mambo ya maafa. Ushauri huu lazima tuufanyie kazi kwa sababu viko vituo vya hali ya hewa na kadhalika na kadhalika. Sasa kiutaalamu hii tupate ushauri ukoje lakini kila ushauri mzuri ambao utatusaidia sio vibaya kuufanyia kazi na kuona namna gani utasaidia.
Kuhusu maisha ya vijana wetu katika masuala ya maafa ni jambo zuri jambo ambalo tunalipokea.

Mhe. Naibu Spika, kuhusu sifa ya Mkurugenzi tungekuwa tunahitaji awe na sifa zaidi ya hapo. Sheria inasema zile ni *minimum qualifications,* kwa hiyo tunaanzia hapo kila tukipata mzuri zaidi, ana uwezo zaidi ndio huyo atakuwa tunayemtaka ili atusaidie katika mapambano haya ya kukabiliana na maafa.

Mhe. Naibu Spika, nchi tulizopata uzoefu ni Oman, Seychelles, Mauritius, Tanzania Bara, Israel na hasa kwenye mikutano hii ya kimataifa mingi tunapata uzoefu wao. Kwa hiyo, tumepata uzoefu huo ili kujiimarisha zaidi. Sasa suala kwa nini tunaleta mswada huu kwenye hati ya dharura?

Mhe. Naibu Spika, ni kwamba tunazo sababu tatu kubwa.

Kwanza mswada wenyewe wa kukabiliana na maafa, wenyewe maafa hujui yatatutokea lini, kwa hiyo kadiri unapokuwa tayari ni vizuri kuleta mswada wenyewe.
Pili, katika Jumuiya ya Afrika Mashariki sasa hivi inaandaa sheria ya mambo haya ya kukabiliana na maafa na jumuiya inatutaka nchi wanachama tuharakishe suala la kupeleka hizi sheria katika Jumuiya ya Afrika Mashariki ili zile sheria zetu ziweze kuzingatiwa ndani ya Jumuiya ya Afrika Mashariki. Kwa hiyo, tumetakiwa kuharakisha jambo hili.

mwisho, kubwa zaidi ni agizo la Umoja wa Mataifa. Kuna mkutano ambao utafanyika kule Japan agizo hili linatutaka tutoe taarifa kwa mkutano huo namna ambavyo tumeweka mifumo ya kukabiliana na maafa.

Kwa hiyo, inatakiwa uwasilishe taarifa zako, utekelezaji wako katika kikao ambacho kitafanyika mwezi wa tatu nchini Japan. Na kwa sababu sisi tulikuwa nayo sera tayari tunapaswa kuwa na sheria, na ukitazama umuhimu wa kuileta sasa sheria hii upo umuhimu sana. Na kwa sababu hiyo wajumbe mambo haya ya maafa leo miaka minne kwenye Baraza hili tunayazungumza chini chini, juu wanayajua ukoko na utandu kuliko hata sisi tuliokuwa serikalini, na ukiyatizama yote haya yametokana na mashauri ya Baraza hili Tukufu.

Kwa hivyo, tunapotekeleza wajibu huu tusiwe kila mara tunalaumiwa kwa nia njema, tunapofanya jambo jema tupongezwe tunafanya jambo jema. Kuvunja moyo mtu mwenye nia njema si jambo zuri hata kidogo, lazima utaratibu huo tuwe nao.

Na halafu mambo kama haya mengine tukianza kila jambo kuchanganya na mambo ya siasa humu ndani hatuwezi kufika mbali sana, hebu jamani tubadilikeni, tujenge umoja wetu, tuwe na mikakati ya kuwa na dhamira njema ya kusaidiana ili nchi yetu ibadilike na ipige hatua. Kila mara kulaumiana, kushutumiana, kutafuta kasoro ndogo ndogo sio kwenda mbele, lazima tufike mahala sisi viongozi tuwe mfano wa kuzungumza mambo mema; upendo na kushirikiana zaidi ndio tutakapofanikiwa. Lakini asubuhi tukiwa hapa tunakuja tukisutana tu, tukileta hili na lile sioni kama tunajenga msingi wa manufaa ya maendeleo ya nchi yetu.

Tukizungumzia kweli umoja lazima sisi viongozi tuwe *serious* kusimamia umoja, ndio wananchi wetu huko chini watafahamu, tukianza sisi hapa kuvutana wenyewe kwa wenyewe cheche ndogo hapa inafika chini matokeo yake matatizo yanakuwa makubwa zaidi.

Mhe. Naibu Spika, baada ya maelezo hayo naomba kutoa hoja ili sheria yetu ipite, ahsante sana.

**Mhe. Waziri wa Afya:** Mhe. Naibu Spika, naafiki.

**Mhe. Naibu Spika:** Ahsante, Waheshimiwa hoja imeungwa mkono. Sasa niwahoji Waheshimiwa wale wanaounga mkono hoja ya Mhe. Waziri wanyooshe mkono. Waliokataa, waliokubali wameshinda.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

*(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)*

**Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais:** Mhe. Naibu Spika, sasa naomba kutoa taarifa kwamba Baraza lako Tukufu likae kama Kamati ya Kutunga Sheria ili kuupitia mswada huu kifungu baada ya kifungu na marekebisho yake. Mhe. Naibu Spika, naomba kuwasilisha.

## KAMATI YA KUTUNGA SHERIA

### Mswada wa Sheria ya Kukabiliana na Maafa Zanzibar, 2015

### Sehemu ya Kwanza

### Masharti ya Utangulizi

Kifungu 1 Jina fupi na kuanza kutumika
Kifungu 2 Kusomwa pamoja na marekebisho yake

### Sehemu ya Pili

### Kuanzishwa Kamisheni

Kifungu 3 Kuanzishwa kwa Kamisheni vifungu vipya 8(a), 8(b) na 8(c) pamoja na marekebisho yake.
Kifungu 4 Muundo wa Kamisheni pamoja na marekebisho yake.
Kifungu 5 Kazi za Kamisheni pamoja na marekebisho yake.
Kifungu 6 Uwezo wa Kamisheni pamoja na marekebisho yake.
Kifungu 7 Uteuzi wa Mkurugenzi Mtendaji.
Kifungu 8 Sekretarieti ya Kamisheni pamoja na marekebisho yake.
Kifungu 9 Vitengo vya Sekretarieti.
Kifungu 10 Kazi za Sekretarieti.

### Sehemu ya Tatu

### Kuanzishwa kwa Kamati na Marekebisho yake

Kifungu 11 Kamati ya Kitaalamu pamoja na marekebisho yake.
Kifungu 12 Kazi za Kamati ya Kitaalamu.
Kifungu 13 Kamati ya Kukabiliana na Maafa ya Wilaya.
Kifungu 14 Muundo wa Kamati ya Kukabiliana na Maafa ya Wilaya pamoja na marekebisho yake.
Kifungu 15 Kazi ya Kamati ya Kukabiliana na Maafa ya Wilaya pamoja na marekebisho yake.
Kifungu 16 Kamati ya Kitaalamu ya Kukabiliana na Maafa ya Wilaya.
Kifungu 17 Muundo wa Kamati ya Kitaalamu ya Kukabiliana na maafa ya wilaya pamoja na marekebisho yake.
Kifungu 18 Kazi za Kamati ya Kitaalamu ya Kukabiliana na Maafa ya Wilaya.

| | |
|---|---|
| Kifungu 19 | Kamati ya Kukabiliana na Maafa ya Shehia. |
| Kifungu 20 | Muundo wa Kamati ya Kukabiliana na Maafa ya Shehia pamoja na marekebisho yake. |
| Kifungu 21 | Kazi za Kamati ya Kukabiliana na Maafa ya Shehia pamoja na marekebisho yake. |
| Kifungu 22 | Vikao vya Kamati |
| Kifungu 23 | Maamuzi ya Kamati |
| Kifungu 24 | Akidi ya vikao |

**Sehemu ya Nne**

**Mipango ya Kupunguza na Kukabiliana na Maafa**

Kifungu 25 Mpango wa Kukabiliana na Maafa Zanzibar.

**Mhe. Hija Hassan Hija:** Mhe. Mwenyekiti, nimemsikiliza kwa makini Mhe. Waziri lakini naomba nitumie kifungu hiki hasa kifungu cha 25(g) kujenga hoja yangu kwamba, nilimuomba Mhe. Waziri sheria hii ilazimishe kuwepo kwa ofisi maalum ya kukusanya taarifa za maafa na utafiti wa stori za maafa. Mhe. Waziri akasema kwamba ni jambo la kufanyiwa kazi kwa sababu sijui ziko taarifa za hali ya hewa na nini.

Mimi nadhani hata juzi hali ya hewa walitangaza kwamba itanyesha mvua kubwa siku tatu wala haikunyesha. Kwa hivyo, tuwe na ofisi ya kitaalamu Zanzibar ili wataalamu wetu wafanye utafiti wa kina kujua athari sio mvua tu, kuna athari za kimazingira na athari za kilimo. Nadhani madhali Mfuko huu unaanzishwa utakuwa na fedha nyingi. Sasa kwa hiyo tuwe na ofisi maalum ya kukusanya taarifa za kitafiti kuhusu majanga na maafa katika nchi yetu.

**Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais:** Mhe. Naibu Spika, nimemuelewa sana ndugu yangu Mhe. Hija Hassan Hija, anachokitafuta ni mkakati utakaosaidia katika kukabiliana na maafa. Kama nilivyosema ushauri aliotoa sio mbaya ni ushauri mzuri, lakini unahitaji kufanyiwa kazi vizuri tupate mashauri na majukumu huko yameshaondoka. Hapa kwenye kifungu hiki hata ukitizama ni mipango ya kupunguza na kukabiliana na maafa.

Kwa hiyo, hapa ni kuandaa mipango yenyewe, hivyo kuweka taasisi nafikiri sio jambo sahihi, lakini ushauri wake ni mzuri. Sisi kama serikali ushauri huo tuupokee, tuufanyie kazi tuone namna gani tunafanya jambo hili. Kwa sababu kuwa na vituo vya namna hiyo na taasisi za namna hiyo si jambo baya, lakini je, *capacity* ya kufanya hayo mambo kwa sasa yapo? Kwa hivyo, tukiweka kwenye sheria hapa sidhani kama itatusaidia sana.

Ninachosema ni kwamba, suala hili ushauri mwema tuuchukue, tuufanyie kazi katika ngazi mbali mbali za kiserikali tuone basi ni wapi uta-*fit* tufanye hilo jambo ili litusaidie. Kwa sababu ni jambo zuri, kufanya tafiti kuona vipi tutapungukiwa na mazingira na uharibifu wa mazingira na mambo mengine sio vibaya. Lakini je, tuufanye kwenye taasisi zetu tulizonazo, taasisi za kilimo kule Kizimbani au wapi. Basi hili suala angetuachia tufanye kazi, mule kwenye sheria linaweza kutupa tabu kupata majibu yake hasa hapa, hapa tunazungumzia mipango hakuna suala la taasisi.

Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana.

**Mhe. Hija Hassan Hija:** Mhe. Mwenyekiti, mipango ndio nyenzo muhimu ya kuendesha taasisi, kwa hiyo kwanza huanza mpango ndio baadae ikaja hiyo taasisi.

Hoja yangu ni kwamba tukiweka ofisi ya kupokea taarifa za kitafiti ndio itatuwezesha sisi kama nchi kuwa na mpango maalum wa kusomesha wataalamu wetu, bila ya kuwa na ofisi ambayo itatusukuma kwa wale wataalamu hatutakuwa na umuhimu wa kufunza wataalamu, ndio maana mwanzo walifikiria wao kwamba Kamati za Wataalam za Shehia; Mwakilishi, Diwani, Sheha na Wajumbe kumi. Kwa hivyo, hawakuzingatia utaalamu wa hili jambo. Sasa tuwe na ofisi na ofisi hii ndio itusukume sasa kusukuma wataalamu kuelekeza nguvu zetu. *Main power* kwa vijana wetu kwamba tuwasomeshe ili ofisi ifanye kazi, bila ya kuwa na ofisi hili jambo litakuwa ni historia.

Kwa hiyo, kama ni hapa, kama ni wapi, lakini kuwe na ofisi ili Wazanzibari wenyewe na wenzetu wageni waende kituo maalum kutafuta tafiti za kitaalamu kujua nini mwelekeo ujao wa hali ya kimazingira, mwelekeo ujao wa hali ya hewa, mwelekeo ujao wa hali nyengine yoyote ile, lakini tukiacha hivi Mhe. Mwenyekiti, itakuwa hatujafanya kazi.

**Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais:** Mhe. Mwenyekiti, nimeyafahamu sana maelezo ya Mhe. Hija Hassan na tukisoma pale namba 10, Kazi za Sekretarieti zitakuwa zifuatazo: Ukisoma 10(n) inasema kukusanya na kuchambua takwimu za majanga na maafa na kusambaza kwa wizara zote, idara, wakala na watu binafsi. Nafikiri hili linaweza kusaidia kama ilivyo hapa. Na hata huku kwenyewe ukitizama kwenye mipango hiyo 25(d), vipaumbele vya kupunguza na kukabiliana na maafa kwa visiwa vyote vya Zanzibar ikijumuisha na eneo lake la bahari. Kwa hiyo yote haya yanaendana, kwa hiyo mwisho wa siku utatafuta vitu hivyo anavyozungumzia Mhe. Hija Hassan Hija. Nashukuru.

**Mhe. Hija Hassan Hija:** Mhe. Mwenyekiti, sitaki niwe mbishi kwa sababu lengo ni ufanisi, lakini kifungu cha (n) hakijatupa nguvu, ni kazi ile ile ya Katibu, ya Mkurugenzi Mtendaji au Sekretarieti itafanya kazi. Hoja yangu nadhani nimalizie kusema kwamba serikali waizingatie, bila ya kuwa na ofisi kama hizi za kitaalamu maana yake hatutakuwa na mpango wa kujipangia kutafuta wataalamu.

Kwa hiyo, naomba tuendelee, lakini ni hoja muhimu sana kuangalia kuwa na ofisi za kukusanya taarifa sio utegemee mpaka utangaziwe Kenya, utangaziwe nchi nyengine ndio na wewe ujipange hapa ndani, hatuna *main power* yoyote ile. Kwa hiyo ni jambo la kuzingatiwa sana katika nchi.

Mhe. Mwenyekiti tuendelee.

**Mhe. Fatma Mbarouk Said:** Mhe. Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa fursa hii. Nilipochangia kwenye Sehemu hii ya Nne nilieleza kwamba kuna utata wa hii sentensi ya juu kabisa, Mipango ya Kupunguza na Kukabiliana na Maafa. Hii inaonesha kwamba mipango ya kupunguza na kukabiliana na maafa nikasema inaweza ikawa maafa yameshatokea lakini ukasema kwamba unapunguza. Sasa nikapendekeza kuwa atapokuja Mhe. Waziri basi anijibu au anifahamishe zaidi namna ya hii sentensi inavyosema, angalau ingekuwa basi mipango ya kupunguza maafa.

Kwa hivyo, Mhe. Waziri hakunifafanulia juu ya suala hili angalau na mimi nikajua, maana yake kama kuna utata ndani yake. Mipango ya kupunguza na kukabiliana na maafa.

**Mhe Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais:** Mhe. Mwenyekiti, moja katika jambo kubwa tunalolifanya kwenye sheria hii ni suala zima la kujiandaa, ikiwezekana sio kupunguza, ikiwezekana yasitokee hayo maafa yenyewe. Kwa hiyo, mipango ya kupunguza ndio hesabu iliyo kubwa zaidi, yakitokea uyakabili na ukitaka kuyakabili urudishe hali katika ukawaida wake.

Kwa hivyo, madhumuni ni kujiandaa ndio maana kutakuwa na kujiandaa, kujikinga na kadhalika kusudi kusitokee hayo maafa yenyewe. Hivyo ushauri wake anaozungumza Mhe. Fatma Mbarouk na mimi tunazungumza lugha moja, ila tukiwa na mipango ya kupunguza ndio mizuri zaidi yasitokee na ndio maana tukaja na sheria hii kwa maana ya kujiandaa, kujikinga na mwishowe tukishashindwa yote tuyakabili yanapokuwa yashatokea. Kwa hiyo nafikiri tunazungumza lugha moja sijui kama kuna zaidi ya hapo anataka Mheshimiwa, ahsante sana.

**Mhe. Fatma Mbarouk Said:** Ahsante Mhe. Mwenyekiti, mimi nakuwa si mkaidi sana kwa sababu sheria zenyewe ndio najifunza funza kuwa mwanasheria na mimi kama wenzangu humu. Kwa hiyo tuendelee.

**Mhe. Naibu Spika:** Tunakushukuru tunaendelea.

| | |
|---|---|
| Kifungu 25 | Mpango wa Kukabiliana na Maafa Zanzibar. |
| Kifungu 26 | Mipango ya Kukabiliana na Maafa ya Wilaya. |
| Kifungu 27 | Mipango ya Kisekta ya kukabiliana na Maafa. |
| Kifungu 28 | Miongozo. |

**Sehemu ya Tano**

**Ngazi za Maafa, Tamko na Mawasiliano**

| | |
|---|---|
| Kifungu 29 | Ngazi za Maafa. |
| Kifungu 30 | Kutangaza Hali ya Maafa Katika ngazi ya Wilaya na Shehia. |
| Kifungu 31 | Kutangaza Hali ya Maafa ya Kitaifa. |
| Kifungu 32 | Kipindi cha Kutangaza Hali ya Maafa ya Kitaifa. |
| Kifungu 33 | Mawasiliano na Utaratibu wa Utoaji Maelezo. |
| Kifungu 34 | Upatikanaji wa Rasilimali wakati wa maafa. |
| Kifungu 35 | Uwezo katika hali ya dharura au maafa. |

**Sehemu ya Sita**

**Masharti ya Fedha**

| | |
|---|---|
| Kifungu 36 | Fedha za Kamisheni. |
| Kifungu 37 | Vyanzo vya Fedha. |
| Kifungu 38 | Makadirio. |
| Kifungu 39 | Ukaguzi wa Hesabu pamoja na marekebisho yake. |
| Kifungu 40 | Mfuko wa Kukabiliana na Maafa |
| Kifungu 41 | Malengo ya Mfuko |

**Sehemu ya Saba**

**Makosa na Adhabu**

| | |
|---|---|
| Kifungu 42 | Makosa na Adhabu. |
| Kifungu 43 | Makosa yanayohusu kukataa kutoa taarifa pamoja na marekebisho yake. |
| Kifungu 44 | Makosa yanayohusiana na kutoa tahadhari za uongo. |

**Sehemu ya Nane**

**Masharti Mengineyo**

| | |
|---|---|
| Kifungu 45 | Kulindwa kwa kitendo kilichofanywa kwa nia njema. |
| Kifungu 46 | Ripoti ya Maafa. |
| Kifungu 47 | Kanuni pamoja na marekebisho yake. |
| Kifungu 48 | Kilichopendekezwa na Kamati kufuta na kubakiza. |

*(Baraza lilirudia)*

**Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais:** Mhe. Naibu Spika, ilivyokuwa Kamati ya Kutunga Sheria imeupitia Mswada wangu kifungu kwa kifungu na kukubali marekebisho yake, sasa naomba Baraza lako Tukufu liukubali mswada huu. Naomba kutoa hoja.

**Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais:** Mhe. Naibu Spika, naafiki.

**Mhe. Naibu Spika:** Waheshimiwa Wajumbe niwahoji wale wanaokubaliana na mswada huu wanyooshe mikono. Waliokataa, waliokubali wameshinda.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

*(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)*

**Mswada wa Sheria ya Kukabiliana na Maafa Zanzibar, 2015**

*(Kusomwa kwa mara ya tatu)*

**Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais:** Mhe. Naibu Spika, naomba kutoa hoja kuwa Mswada wa Sheria ya Kukabiliana na Maafa Zanzibar mwaka 2015 usomwe kwa mara ya tatu. Naomba kutoa hoja.

**Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko:** Mhe. Naibu Spika, naafiki.

**Mhe. Naibu Spika:** Waheshimiwa Wajumbe Mswada umesomwa kwa mara ya tatu waliounga mkono wanyooshe mkono. Waliokataa, waliokubali wameshinda.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

*(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)*

*(Mswada wa Sheria ya Serikali ulisomwa mara ya tatu na kupitishwa)*

**Mhe. Naibu Spika:** Waheshimiwa Wajumbe kwanza niwashukuru kwa ushirikiano na kuweza kupitisha Mswada wetu huu na leo ni siku ya Ijumaa, siku muhimu na kila tukienda mapema msikitini tunapata ng'ombe, tukichelewa kidogo mbuzi, basi naomba leo tuondoke mapema ili tukapate huyo mbuzi. Kwa maana hiyo naakhirisha kikao hiki hadi saa 11:00 jioni ili tuje kuendelea na ratiba yetu.

*(Saa 5:22 asubuhi Baraza liliakhirishwa hadi saa 11:00 jioni)*

*(Saa 11:00 Jioni Baraza lilirudia)*

*(Majadiliano Yanaendelea)*

**Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ:** Mhe. Naibu kwa idhini yako naomba kuwasilisha Mswada wa Sheria ya kuanzisha Wakala wa Ulinzi wa Jeshi la Kujenga Uchumi Zanzibar.

Mhe. Naibu Spika, awali ya yote nachukua fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu mtukufu kwa kutujaalia afya njema na nguvu zilizotuwezesha kukutana tena leo katika Baraza lako hili Tukufu ili kuendelea na kazi ya kuwatumikia wananchi.

Mhe. Naibu Spika, nachukua fursa hii kukushukuru wewe binafsi kwa kukubali kunipa fursa ya kuwasilisha katika Baraza lako Tukufu Mswada wa Sheria ya kuanzisha Chombo cha Ulinzi ambacho kitakuwa ni wakala wa Jeshi la Kujenga Uchumi Zanzibar.

Mhe. Naibu Spika, namshukuru Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dr. Ali Mohd Shein kwa maelekezo na miongozo yake iliyowezesha kufanikisha kukamilika kwa Mswada huu na leo kuweza kuuwasilisha katika Baraza lako Tukufu.

Mhe. Naibu Spika, Mswada huu umejadiliwa na Kamati ya Katiba Sheria na Utawala chini ya Mwenyekiti wake Mhe. Ussi Jecha Simai Mwakilishi wa Wananchi wa Jimbo cha Chaani, kamati imefanya kazi kubwa ya kupitia Mswada huu na kufanyia marekebisho maeneo ambayo yalikuwa yana upungufu na kwa sasa nina furaha ya kuliarifu Baraza lako kuwa uko katika hali nzuri.

Nawashukuru sana kwa michango yao ambayo imetokana na uzoefu, uelewa na umahiri wao.

Aidha namshukuru Mhe. Mwanasheria Mkuu wa Zanzibar Mhe. Said Hassan na wanasheria wenzake kwa kazi kubwa waliyoifanya pamoja na kamati na kufanikisha kukubalika kwa mswada huu na kuruhusu kuwasilishwa katika Baraza zima.

Mhe. Naibu Spika, vile vile napenda kutoa shukurani na pongezi kwa kamati ya uongozi ya ofisi yangu na Katibu Mkuu wa Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ, Mkuu wa Jeshi la Kujenga Uchumi na Maafisa mbali mbali wa Idara Maalum ambao walifanya kazi ya kuandaa rasimu ya awali ya mswada na kuendelea kuratibu maoni mbali mbali yaliyokuwa yanatolewa katika ngazi mbali mbali kwa utaratibu wa maandalizi ya mswada kabla ya kufikishwa katika Baraza hili Tukufu.

Pia nawashukuru watendaji wote wa Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ kwani ushirikiano wao kwangu ndio chanzo cha mafanikio haya.

Mwisho lakini niwashukuru wafanyakazi wa Idara ya Upigaji Chapa iliyo chini ya Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais wafanyakazi wa Baraza la Wawakilishi kwa kazi kubwa walioifanya ya kuweza kukamilisha kazi ya upigaji chapa ya mswada huu na kuwapatia Waheshimwa Wajumbe nakla zao nawashukuru sana kwa hilo.

Chimbuko la mswada Mhe. Naibu Spika, ni haja ya kuwa na sheria itakayoanzisha na kusimamia chombo cha kutoa huduma za ulinzi kwa wawekezaji wa Utalii na watalii pamoja na wawekezaji wengine ili kuondosha vitendo vya uhalifu na hujuma mbali mbali zinazoonekana kuongezeka kila siku katika visiwa vyetu vya Unguja na Pemba.

Mhe. Naibu Spika, madhumuni ya mswada huu ni kuwasilisha mapendekezo ya kutungwa sheria itakayoanzisha chombo cha kutoa ulinzi kwa biashara ya Utalii na wawekezaji kwa ujumla dhidi ya tishio la wizi na hujuma mbali mbali.

Muundo wa Mswada, Mhe. Naibu Spika, mswada wa sheria wa Wawakala wa Ulinzi umegawika katika sehemu nne na vifungu arubaini kama ifuatavyo.

(1) Sehemu ya kwanza hii ina vifungu vitatu ambavyo ni jina fupi la sheria, tarehe ya kuanza kutumika, matumizi ya tafsiri ya maneno muhimu.

(2) Sehemu hii ina vifungu 25 ambacho ni kifungu cha 4 hadi cha 28 vinavyoelezea uanzishwaji wa wakala na uwezo wake, uteuzi wa viongozi; majukumu yao, bodi na uwezo wake.

(3) Sehemu hii ina jumla ya vifungu 6 kuanzia kifungu cha 29 hadi 34 ambavyo vinaelezea mapato na matumuzi, usimamizi wa fedha uendeshaji wa *Account* ya Benki, Ukaguzi wa Hesabu pamoja na masharti ya kutoa taarifa za kila mwaka.

(4) Sehemu ina jumla ya vifungu 6 kuanzia kifungu cha 35 hadi 40 ambavyo vinaelezea masharti mengineyo yakiwemo makosa na adhabu, kinga kwa watumishi na uwezo wa Waziri kutunga kanuni.

Hitimisho.

Mhe. Naibu Spika, naomba kuwasilisha kwenye Baraza lako Tukufu mswada huu kwa kufuata taratibu za kisheria na kanuni za Baraza la Wawakilishi ili muupitie, muujadili, mtoe ushauri wenu na hatimae muidhinishe mswada huu na kuwa sheria.

Mhe. Naibu Spika, naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

**Mhe. Ussi Jecha Simai (Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala):** Ahsante Mhe. Naibu Spika, kwa kunipa nafasi ya kuwasilisha Hotuba ya Maoni ya Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala ya Baraza la Wawakilishi kuhusu Mswada wa Sheria ya kuanzisha Wakala wa Ulinzi wa Jeshi la Kujenga Uchumi (JKU) mwaka 2015.

Mhe. Naibu Spika, awali ya yote naomba kuchukua fursa hii adhimu kumshukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu, kwa kutujaalia neema ya uhai pamoja na afya njema miongoni mwetu na kutuwezesha kukutana asubuhi hii ya leo na kujadili Mswada huu muhimu wa kuanzisha Wakala wa Ulinzi wa Jeshi la Kujenga Uchumi (JKU) wa mwaka 2015.

Mhe. Naibu Spika, Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala inawasilisha muhtasari huu mbele ya Baraza lako Tukufu huku ikitambua kazi kubwa ingawa ya haraka iliyofanywa na Wajumbe wa Kamati kwa kushirikiana na watendaji wa Baraza na Afisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

Naomba kuchukua fursa hii kutambua juhudi za Wajumbe wako kwenye Kamati hii kama ifuatavyo:-

| | | |
|---|---|---|
| 1. | Mhe. Ussi Jecha Simai | Mwenyekiti |
| 2. | Mhe. Abdalla Juma Abdalla | Makamo Mwenyekiti |
| 3. | Mhe. Wanu Hafidh Ameir | Mjumbe |
| 4. | Mhe. Bikame Yussuf Hamad | Mjumbe |
| 5. | Mhe. Nassor Salim Ali | Mjumbe |
| 6. | Mhe. Suleiman Hemed Khamis | Mjumbe |
| 7. | Ndg. Aziza Waziri Kheir | Katibu |
| 8. | Ndg. Khamis Hamad Haji | Katibu |

Mhe.Naibu Spika, naomba upokee shukurani za Kamati yangu kwako na kwa Katibu wa Baraza kwa kutengeneza mazingira ya kuiwezesha Kamati hii kufanya kazi ya kuchunguza Mswada huu ingawa katika hali ya dharura na kwa Kamati ilikuwa kazi ya haraka.

Mhe. Naibu Spika, baada ya utangulizi huo naomba sasa kwa niaba ya Waheshimiwa Wajumbe wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala, ambao nimetangulia kuwataja hapo juu, kuwasilisha muhtasari wa maoni ya Kamati kuhusu Mswada wa Sheria ya Kuanzisha Wakala wa Ulinzi wa Jeshi la Kujenga Uchumi (JKU) ambao upo mbele yetu.

Mhe. Naibu Spika, tunashuhudia kwa mara nyengine tena Baraza lako linapokea Miswada mengine kutoka Serikalini ikifika hapa kwa hati ya dharura ya Mhe. Rais. Kutokana na dharura yenyewe uliyoieleza wakati wa kufungua Mkutano huu siku ya Jumatano ya tarehe 21/01/2014, kamati yangu haina tatizo na dharura hii isipokuwa naomba nitahadharishe mambo yafuatayo kabla ya kueleza kazi ya Kamati ya kuchunguza Mswada kwa mujibu wa Kanuni:-

- Mhe. Naibu Spika, Baraza lako liwe na hadhari kuwa fursa hii isitumike vibaya kwa kuletewa Miswada kwa namna ya haraka kama hii. Sote tunakumbuka kuwa huu ni mkutano wa pili mfululizo inaletwa Miswada ya dharura.

- Wajumbe wako watendewe haki kwa kupatiwa Miswada mapema, hata kama Miswada italetwa kwa hati ya dharura, ni vyema Wajumbe wakapatiwa nakala hizo mapema iwezekanavyo ili wapate muda wa kutosha wa kupitia na kufanya utafiti au kufanya mawasiliano na wananchi wao. Utaratibu wa sasa wa kuwapatia Miswada leo kwa kesho ni wa usumbufu na hatari ambapo kuna uwezekano mkubwa wa Baraza lako Tukufu hili kupitisha sheria ambazo kiwango chake ni kidogo na sheria zisizo na ubora na kasoro nyingi ndani yake.

- Aidha, mtindo huu wa kuleta Miswada kwa hati ya dharura usitumike kama njia ya mkato kwa taasisi zetu kuchelewa kukamilisha kuandaa Miswada mapema na kuiwasilisha Barazani.

Mhe. Naibu Spika, Kamati yangu kwa muda ilioupata imejitahidi kuchunguza Mswada huu kama Kanuni ya 83 (4) ya Kanuni za kudumu za Baraza la Wawakilishi inavyoeleza na katika kuchunguza huko Kamati imeona imshauri Mhe. Waziri kwenye maeneo mbali mbali ya Mswada ili Mswada huo utakapopitishwa na Baraza hili kuwa sheria uweze kutekelezeka vizuri.

Mhe.Naibu Spika, Eneo la kwanza ambalo Kamati imechunguza na kujadiliana sana kuhusu Mswada huu ni kuhusu kitu gani hasa Mswada huu unakusudia kuanzisha, Kamati imeona kwenye vifungu mbali mbali mgongano wa chombo kinachotaka kuanzishwa. Vipo vifungu vinaeleza kinachoanzishwa ni "Taasisi ya Ulinzi", vifungu vyengine vinaonesha kinachoanzishwa ni "Wakala" na vipo vifungu vinaonesha kinachoanzishwa ni "Shirika".

Mhe. Naibu Spika, katika mkanganyiko huu Kamati ilielezwa kuwa kinachoanzishwa ni Wakala wa Ulinzi wa Jeshi la Kujenga Uchumi. Maoni ya Kamati yangu katika hili ni kuwa kama kinachoanzishwa ni Wakala basi yazingatiwe masharti ya kifungu cha 55 cha Sheria ya Utumishi wa Umma, Namba 2 ya mwaka 2011 ambacho kimeweka wazi kuwa Wakala wa Serikali haitakuwa na kazi za kibiashara.

Mhe. Naibu Spika, Kamati imeshauri kuwa vifungu vya Mswada huu ambavyo vinaonesha kwenda kinyume na dhana ya kuanzishwa wakala wa Serikali virekebishwe kwenda sambamba na dhana yenyewe au vifutwe na baadhi

ya vifungu hivyo ni kifungu cha 4 (2) (a), 6 (a), 29 (1) (d) na kifungu cha 33 na vifungu vyengine kadhaa kama vinavyooneshwa katika waraka wa marekebisho ya Kamati uliogawanywa kwa Wajumbe.

Mhe. Naibu Spika, **e**neo jengine ambalo Kamati inashauri Mhe. Waziri kulirekebisha kabla ya Mswada huu kuwa Sheria ni kwenye Kifungu cha 1, ambacho kinaelezea jina fupi na kuanza kutumika kwa sheria hii. Katika kifungu hiki Kamati inashauri jina fupi liwekwe vizuri kwa kusomeka " sheria hii itajulikana kama Sheria ya Kuanzisha Wakala wa Ulinzi wa JKU ya mwaka 2015".

Mhe. Naibu Spika, **k**atika kifungu cha 4 cha Mswada huu imewekwa kuwa Wakala wa Ulinzi wa JKU itakuwa chini ya Mkuu wa Jeshi la Kujenga Uchumi, ni maoni ya Kamati yangu kuwa kifungu hiki kinaleta mgongano na watendaji wakuu wa Wakala kwani Mkurugenzi Mkuu anachaguliwa na Rais, kadhalika na Mwenyekiti wa Bodi kama ilivyowekwa kwenye vifungu vya 9 na 14 vya Mswada.

Mhe. Naibu Spika, mbali na uwezo na kazi alizopewa Mkurugenzi na Mwenyekiti wa bodi ambazo zitakuwa kwa mujibu wa sheria hii, Kamati imeshindwa kuona Mkuu wa JKU ambaye taasisi hii itakuwa chini yake anaingia wapi katika utendaji kazi wa Wakala unaoanzishwa na Mswada huu wa sheria.

Mhe. Naibu Spika, Kamati inashauri marekebisho yafanyike kwa aidha Mkuu wa JKU kuwa ndiye Mkurugenzi Mkuu au Mwenyekiti wa Bodi, kwa kufanya hivi kunaweza kuondoa mgongano wa kiutendaji wakati wa utekelezaji wa Sheria hii.

Mhe. Naibu Spika, kama inavyooneshwa katika waraka wa marekebisho yanayoshauriwa na Kamati kwa Mheshimiwa Waziri, Kamati imeshauri kurekebisha mpangilio wa vifungu katika kifungu cha 12 kubadilishwa na kuwa kifungu cha 11 (2) na vifungu vinavyofuata kubadilika kwa kifungu cha 13 kuwa cha 12 na kuendelea kwa vifungu vyengine.

Mhe. Naibu Spika, mapendekezo hayo yana nia ya kuunganisha dhana moja ya Mkurugenzi kupendekeza kuanzishwa vitengo mbali mbali katika uwakala pamoja na wakuu wa vitengo hivyo kati ya kifungu cha 11 na kile cha 12 cha mswada huu.

Mhe. Naibu Spika, Katika kifungu cha 18 cha Mswada huu kuhusu muda wa Mwenyekiti kushika wadhifa wake, imewekwa kipindi cha miaka minne, mwaka mmoja zaidi ya muda wa kumaliza kipindi cha Wajumbe wa bodi.

Kamati inashauri kufanyika marekebisho katika sheria zinazoelekeza miundo ya bodi kwa muda wa Mwenyekiti kuwa sambamba na wajumbe au wajumbe wamalize sawa na Mwenyekiti. Aidha, Bodi zisipewe zaidi ya vipindi viwili mfululizo.

Mhe. Naibu Spika, Pamoja na muhtasari huu, naomba nimalizie kwa kueleza kuwa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala imepitia Mswada huu kwa kirefu na imetoa ushauri kwa Mhe. Waziri kama unavyoonekana kwenye waraka wa marekebisho.

Mhe.Naibu Spika, namuomba Mhe. Waziri apokee ushauri wa Kamati na kutolea maelezo ya ufafanuzi, panapostahiki pafanyiwe marekebisho kwa nia ya kuimarisha vifungu vya Mswada huu.

Mhe. Naibu Spika, Kwa vile Kamati ilishajiridhisha katika Mswada huu na kutoa maoni na ushauri wake, nawaomba Wajumbe wa Baraza lako nao watoe mchango wao wa kuimarisha Mswada huu na kwa pale ambapo jicho la Kamati yetu halikufika, tunaomba watumie fursa hii kuona na kushauri ili tuweke vizuri Mswada huu kabla ya kupitisha kuwa sheria.

Mhe. Naibu Spika, nikushukuru tena kwa kunipa nafasi ya kuwasilisha hotuba hii kwa muda huu mfupi na naomba nimalizie ili Wajumbe nao wapate fursa pana ya kuchangia.

Mhe. Naibu Spika, naomba kuwasilisha. (*Makofi*)

**Mhe. Makame Mshimba Mbarouk:** Mhe. Naibu Spika, kwanza nikushukuru wewe Ijumaa ya leo kwa sasa hivi kuwa ungali hai na *inshaallah* Mwenyezi Mungu atakupa uhai wenye kheri na wewe. *Inshaallah* na mimi

niwaombee dua Wajumbe wote wa Baraza hili tukufu Mwenyezi Mungu awajaalie waendelee kuwa hai kwenye uendelevu wenye kheri na wao, na *inshaallah* nimshukuru na yeye Mhe. Waziri na yeye tumuombee dua na tuupitishe mswada wake wenye kheri na sisi na katika ulinzi wa nchi yetu.

Mhe. Naibu Spika, Sheria hii imekuja wakati mzuri sana leo hakuna mtu asiyejua nini kilitokea ndani ya Zanzibar. Mhe. Naibu Spika, leo kumetokea jambo kubwa sana huko Darajani, majambazi wamevamia risasi zimelia kama tuko *South Africa* au nchi gani nyengine yenye matatizo na kama aliotea, alisema Mhe. Waziri kuwa alete kitu ambacho kitaweza kuwasaidia wawekezaji na hata watu binafsi mmoja mmoja wenye uwezo wa kuweza kuwaita hii kampuni au wakala hawa kuweza kuwalinda.

Mhe. Waziri nikushukuru sana tena sana, shukurani zangu Mwenyezi Mungu anazipokea Ijumaa hii ya leo na sisi wengine ni masharifu.

Mhe. Naibu Spika, mimi bado sijapata jibu safi sikufichi. Kule wenzetu wale walijisema Suma Kampuni ya ulinzi kama hivi kama sijasahau. Mhe. Waziri hebu utakapokuja nitafutie usahihi wa wale wenzetu walitumia neno gani la moja kwa moja. Hebu naomba sana walisema kwamba JKT *security guard* au ilikuwa vipi nimesahau kidogo, naomba unisaidie kwa sababu ili niweke sawa.

Huu mswada mimi nimeukubali wala sina tatizo lolote, ningeomba sana unikubalie hilo, kwa sababu hapa *spelling* hii inanipa tabu katika haya masuala ya ulipaji hapa. Kulipa ada na malipo mengineo kwa ajili ya huduma hiyo. Sasa mimi nikajiuliza mtu au taasisi au kampuni yoyote inayopata huduma za shirika, ina maana watu waliokwenda kutaka huduma ndio kwenye wakala au kwenye shirika, ndio hapo mimi kidogo inanitatiza. Ndio maana hapa Mhe. Mwenyekiti wangu mtaalamu zaidi akaingia mashaka yako hapa sasa.

Mhe. Naibu Spika, kwa kuwa yuko kijana wangu anataka kuja, niweze kumalizia. Lakini acha kidogo nimpe raha ili aweze kuweka sawa na apate *point* kwangu mimi. Mhe. Naibu Spika, ameambiwa mtu ataweza kuteuliwa kuwa Mwenyekiti, isipokuwa awe na sifa zifuatazo. Awe ni afisa wa juu mwenye cheo cha Kanali au aendelee.

Sasa Mhe. Naibu Spika, hapa nataka niulize swali. Je, wale makanali ambao walikuwa wamestaafu kutokana na umri, lakini bado wanaweza kufanya kazi. Je, sheria itaweza kuwapa nguvu ya kuweza kuajiriwa, kwa sababu bado wapo makanali wazuri tu wa JKU waliostaafu, tena wapo sana Mhe. Waziri, wana nguvu na wamesoma. Je, sheria hii Mhe. Naibu Spika, ikiwa Rais au mwenyewe waziri itakuwa na uwezo wa kuweza kuwarejesha hapa kwa mujibu wa utaratibu huu kumuweka Mwenyekiti kwa sababu Mwenyekiti.

Mhe. Naibu Spika, mara nyingi sana tunakuwa hatutii umri wa yule mtu aliyechaguliwa tunatoa tu, hatimaye tunakwenda kumtafuta mtu ambaye ameshazeeka, halafu ukimshauri bado ana yale mambo ya kizamani. Kwa hivyo, Mhe. Naibu Spika, mimi ningeomba na umri nao uhusike, tukubaliane nao wakati unachaguliwa Mwenyekiti, tuuzingatie sana umri ili tuweze kuwaweka hawa, kwa sababu utakuta Kanali amemaliza mapema sana, lakini bado ana uwezo wa kuweza kuzifanya hizi kazi kwa mujibu wa utaratibu unaokubalika.

Mhe. Naibu Spika, mswada huu kama nilivyosema mimi sina tatizo nao, ninautolea baraka zote Ijumaa ya leo na ninaukubali kwa asilimia mia kwa mia, hauna doa lolote.

Niwaombe sana Waheshimiwa Wajumbe tuukubalie kwa asilimia hiyo na tuupitishe kwa nguvu zote, naomba sana Waheshimiwa Wajumbe. Kwa hayo machache Mhe. Naibu Spika, nashukuru sana, ahsante sana.

**Mhe. Ali Salim Haji:** Mhe. Naibu Spika, na mimi nishukuru kwa kupata fursa hii kuweza kuchangia mswada huu wa kuanzisha Sheria ya Taasisi ya Ulinzi ya JKU.

Mhe. Naibu Spika, kabla sijaanza chochote na mimi nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijaalia afya njema, lakini na mimi pia nitoe pongezi za dhati kwa Mhe. Waziri kwa kutuletea mswada huu.

Kwa kweli mswada huu utatusaidia sana Wazanzibari katika maeneo mbali mbali, kwa muda mrefu tumekuwa tukisikia na tunasikitika sana tunaposikia matukio ya kuvamiwa kwa watalii, vitendo ambavyo vinapelekea kurudisha nyuma maendeleo ya nchi hii na kushusha uwezo wa serikali katika upatikanaji wa mapato, kwani

tunafahamu kwamba suala la utalii Zanzibar, ndio suala ambalo limekuwa tegemeo katika nchi yetu katika kujiongezea mapato.

Sasa imani yangu ni kwamba mswada huu tukishaupitisha na kuwa sheria basi yale matendo ambayo walikuwa wakifanyiwa ndugu zetu, ambapo wakati mwengine yalikuwa yanapelekea kuondosha uhusiano mzuri baina ya taifa jengine na taifa letu, basi yataweza kutoweka na kujenga imani katika kuja kwa wageni wetu mara kwa mara.

Mhe. Naibu Spika, pamoja na faida ya ulinzi kwa wageni na wawekezaji wa nchi hii katika maeneo mbali mbali, pia tuna imani kwamba mswada huu utakapopita na kuwa sheria, basi unaweza kusaidia kwa asilimia kubwa sana kuondosha manung'uniko au vile kasoro za vijana wetu katika suala zima la kujiajiri katika eneo hili la ulinzi. Kwa muda mrefu tulikuwa tukipiga makelele sana hapa Barazani, kwamba tumeanzisha maeneo haya ya uwekezaji na masuala ya utalii, lakini kumekuwa kukijitokeza tabia kwa makampuni kutoka nje ya Tanzania, Kenya na nchi nyengine kuja hapa kufanya kazi za ulinzi na vijana wetu kufika pahala wakakosa ile ajira ambayo tulitegemea kwamba ingeweza kuwasaidia.

Mhe. Naibu Spika, najua kulikuwa kuna sababu nyingi za kupelekea vijana wetu kutoajiriwa, yakiwemo kutopata mafunzo ya uhakika. Lakini pia kutokuwa na vitengo ambavyo vilikuwa na sheria madhubuti ya kuweza kufika pahala kuanzisha hivyo vitengo vya ulinzi. Imani yangu ni kwamba mswada tukiupitisha na kuwa sheria, basi suala la ajira kwa vijana wetu linaweza likawasaidia kwa asilimia kubwa.

Mhe. Naibu Spika, mimi nilitaka niseme tu na nimejaribu kuuangalia sana mswada huu, lakini baadhi ya maeneo kila ukiangalia unaona zaidi kwamba kutakuwa na nguvu kubwa ya bodi katika suala la uajiri na suala la utendaji kazi. Sasa Mhe. Waziri atakapokuja anisaidie namna alivyojifunza kwa wenzetu Tanzania Bara, namna walivyoanzisha kitengo kama hiki, wenzetu kule wanaita Suma JKT.

Mhe. Naibu Spika, sasa nataka kuona labda tumekwenda sambamba vipi baina ya sheria yao na sheria yetu, ili kuweka mambo mepesi katika utendaji wa kazi. Kwa sababu shirika litakapokuwa linaanza kazi na kama sheria ya mswada inavyozungumza, kwamba hawa watu watakuwa wakitumia silaha na suala la kutumia silaha ni suala ambalo linahitaji mafunzo na uadilifu wa kutosha, vyenginevyo badala ya kuwa tunakwenda kulinda tunaweza kufika pahala tukakuta kwamba vijana wale wanaweza wakatumia vifaa vile kwa dhamira nyengine, hatutegemei kufanya hivyo, lakini nasema kwamba tuangalie namna wenzetu walivyojikita.

Lakini kwa ufahamu wangu Mhe. Naibu Spika, wenzetu Tanzania Bara Suma JKT walichokifanya wao kwamba kile kitengo waajiriwa wake wanakuwa ni vijana ambao wamepata mafunzo ya uaskari kupitia JKT, lakini wale ambao hawakubahatika kuajiriwa na taasisi za majeshi, ndio ambao wanawachukua kwenda kufanyakazi katika kitengo kama hiki cha ulinzi wa sekta binafsi.

Sasa na kwetu hilo ndio litakalokuwa linafuata, kwa sababu baadhi ya maeneo nimeona kuwa sheria imetiwa nguvu pia ya kuajiri mtu ambaye sio kutoka JKU, sasa nilikuwa napata mashaka kwa wale ambao hawatokuwa wamepitia JKU na kuwapeleka katika kitengo ambacho kitakuwa kinatumia masuala ya silaha. Sasa wenzetu wao naona zaidi wamejikita kwamba moja kwa moja mtu amepata mafunzo ya JKT, na baada ya kupata mafunzo ya JKT lakini hakuwa na sifa za kwenda jeshi, labda kwa sababu ya elimu ndogo au kwa sababu ya umri, kwa sababu umri upo sio zaidi ya miaka 25. Kwa hivyo, wale ndio wanawachukua na kuwaingiza katika suala la ulinzi huu mwengine.

Sasa suala hili Mhe. Waziri atakapokuja anisaidie kuona namna gani wao walivyojipanga katika kuwatumia vijana wetu ambao watakwenda JKU. Pia nimuombe Mhe. Waziri, wakati tunajiandaa kupitisha sheria hii basi ni vyema tukaanzisha kama walivyoanzisha wenzetu, huwa tunakuwa tunachukua awamu maalum yaani kila mwaka kuwaingiza vijana kwa wingi kupata mafunzo ya JKU, ili baadae kuwa na akiba ya kuweza kuwachukua kuwapeleka katika hilo shirika la ulinzi kwa wale ambao watakuwa hawana sifa. Sasa hilo nimuombe, lakini nimuombe pia tuangalie zaidi na sifa zile ambazo tunahisi wanaweza wakazitumikia kama JKU.

Mhe. Naibu Spika, vile vile nataka nimuombe Mhe. Waziri, kwamba wakati tunaandaa mswada huu na kutegemea kuwa sheria ya nchi hii. Namuomba Mhe. Waziri akaandaa mikakati ya kutosha kwa wale ambao tayari kama wako JKU, au tayari ambao tunawategemea kuanza kazi baada tu sheria hii kupitishwa, tukaandaa kitengo maalum cha elimu. Kwa sababu kama utauangalia mswada huu Mhe. Naibu Spika, umelenga zaidi kufanyakazi kwa wawekezaji na watalii, hawa watu wanatumia lugha za kigeni. Sasa kama hatukujiandaa kutoa mafunzo na elimu, suala la

*communication* litakuwa gumu baina ya watumishi na watalii. Sasa litakuwa ni gumu kwa mtu kupata taarifa halisi kutoka kwa mgeni kumuelezea namna tukio lilivyotokezea na mlinzi akaweza kutoa huduma kwa haraka kwa yule mgeni ambaye ameathirika kwa namna moja au nyengine.

Kwa hivyo, ningemuomba wakati tunajiandaa na tumo ndani ya *process* ya kuandaa sheria, basi na yeye Mhe.Waziri akajiandaa kuanza kuwaandaa vijana maalum, ambao yeye labda ni tegemezi wa kuanzia na sheria hii kuanza kutoa mafunzo ya lugha mbali mbali, na hususan kuzingatia labda yale maeneo ambayo watalii wengi Zanzibar wanapenda kuingia ili kujenga wepesi wa shughuli zao.

Mhe. Naibu Spika, baada ya hayo. Hili nimelizungumza Mhe. Naibu Spika, la elimu baada ya kuangalia kazi za shirika zilizoelezwa katika ukurasa wa 270, kifungu cha 6(c).

Mhe. Naibu Spika, kifungu hiki naomba nikinukuu kinasema kwamba moja ya kazi zake itakuwa ni kutoa ushauri wa kiulinzi na kiusalama kwa watalii, wadau wa utalii na taasisi nyenginezo. Sasa kama itakuwa hatuna watu wenye taaluma kutoa ushauri, unampa ushauri mtu ambaye mawasiliano yenu ni magumu basi linaweza likaathiri kwa namna moja au nyengine. Ndio maana suala la kujiandaa na suala la kutoa taaluma nikajaribu kulizungumza kwa undani sana Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Naibu Spika, jengine ambalo nataka kulizungumzia katika mswada huu, katika ukurasa huo huo 270 kifungu cha 6(j), kinasema kuweka viwango vya ada ambavyo vitapasa kulipiwa na wawekezaji kuhusiana na mambo yanayohusiana na huduma ya ulinzi.

Sasa hapa nimeona zaidi viwango vimewekwa kwa wawekezaji kwamba shirika ndio litakuwa linapanga, lakini tegemeo langu na nafikiri mswada huu umezungumza katika maeneo mengine, kuwa pamoja na kuweka ulinzi kwa wawekezaji na watalii, lakini pia wanaweza kutoa huduma za utalii kwa mtu mmoja mmoja kwa yule ambaye atakuwa anahitaji kupata. Sasa viwango vimewekwa katika eneo moja. Mimi ningeomba labda ingejaribu kurekebishwa kama itakuwa inawezekana, kuweka viwango vya ada ambavyo vitapaswa kulipiwa na wawekezaji na maeneo mengine yatakayotoa huduma ya ulinzi. Kwa hivyo, ingeingia kitu chengine, kwa sababu viwango hapo vimeelekezwa katika eneo moja.
Kuna jambo jengine Mhe. Naibu Spika, nilitaka labda Mhe. Waziri atakapokuja anisaidie kuja kunipa maelezo, kwamba tunataka kuanzisha sheria hii ya ulinzi, lakini kwa bahati nzuri tayari hapa Zanzibar, kuna makampuni mengi sana ambayo yako kisheria, na tayari nimesha- *organise* kutoa ulinzi katika maeneo mbali mbali, maeneo ya wawekezaji, maeneo ya utalii na maeneo mengine.

Mhe. Naibu Spika, nilipokuwa nikiangalia kwa kweli nilijaribu kwenda *deep* katika huu mswada, sikuona pahala ambapo tunaweza tukazibana zile taasisi binafsi ambazo zinatoa ulinzi. Tutakuwa tayari tumeshakuwa na sheria, kwa sababu unajua mara nyingi na hususan Zanzibar wawekezaji wengi au wafanyabiashara wengi wamekuwa wanajaribu kukimbilia katika maeneo ambayo yana unafuu wa bei, hawaangalii unafuu wa ulinzi na usalama wao, wanachoangalia wao ni *benefit* ya unafuu wa bei. Inawezekana bei yetu sisi iko juu katika kutoa huduma za ulinzi, lakini kumbe pamoja na bei ya juu, lakini zaidi tunazingatia kwamba sisi walinzi wetu watakuwa wanapewa huduma bora ya ulinzi. Nina wasi wasi watu wakaacha kuangalia huduma bora ya ulinzi wakaenda kukimbilia katika maeneo ya urahisi wa bei kwa makampuni ya ulinzi.

Sasa nafikiri tungejaribu kuangalia kuweka kitu ambacho kitakuwa ni kizito kwa wale wawekezaji, kwa namna gani wanapotaka kuwekeza labda ni taasisi gani ambayo itakuwa iko kisheria katika masuala mazima ya kutoa ulinzi. Vyenginevyo, taasisi inawezekana ikakaa lakini tukakosa kuja kutoa huduma, kutokana na wawekezaji kutokukimbilia katika maeneo yaliyokuwa ni mepesi zaidi kibei.

Jengine Mhe. Naibu Spika, katika kifungu cha Saba kwenye ukurasa huo wa 270(d). Mswada umezungumza kwamba wataanzisha ofisi ndogo ndogo au uwakilishi ndani ya Visiwa vya Unguja na Pemba, kama itakavyoamuliwa na bodi. Mheshimiwa mimi nafikiri tungejaribu kulisaidia kuweka wazi, usibane zaidi kwamba bodi itakapotaka kuamua kuanzisha hizo kesi ndogo ndogo ndio iamue, lakini wasipoona kuna haja wasiamue.

Mhe. Naibu Spika, mimi nafikiri tungekwenda moja kwa moja. Kama jana tulivyokuwa tukipitisha ule mswada wa mazingira, ulielezea wazi kwamba pamoja na *Head Office,* lakini pia watakuwa na *office* ndogo ndogo za kiwilaya, ambazo zimeelezewa kwamba zitakuwa zinaongozwa na nani. Kwa hivyo, nafikiri na hii ilikuwa kuna haja ya

kusema aa! kutakuwa na *office* za Kimkoa au Kiwilaya ambazo zitaongozwa labda na *level* gani ya waajiriwa wake.Kwa mfano, labda kama kutakuwa kuna wajumbe wa bodi maalum. Sasa nafikiri tungetafuta namna, lakini kuna haja ya kwamba tuweke *base* katika maeneo na sheria itamke wazi, kwa sababu unaposema kwamba bodi inapohisi kuna haja, haja ipo. Kwa sababu unajua mnapokuwa na *head quarter* ndogo ndogo katika maeneo mbali mbali, yanapotokezea matokeo inakuwa ni rahisi mtu kuweza kufikisha suala lake wapi, au taasisi ile kuweza kutoa ripoti katika maeneo yale, kuliko kuipa bodi moja kwa moja kwamba itakavyoamuliwa, kama hawakuamua basi twende tu.

Mhe. Naibu Spika, nafikiri hilo lingeangaliwa kwa undani zaidi kuona namna gani tunaweza kuanzisha hizo *office* kisheria zikawepo katika wilaya zetu, na tukajua tukapanga kama *office* za wilaya zitaongozwa na maafisa kuanzia ngazi gani na mpaka kumalizikia ngazi gani na zitawajibika vipi ofisi za wilaya kwa Ofisi Kuu.

Mhe. Naibu Spika, eneo jengine ambalo nataka nilizungumzie ni eneo la ukurasa wa 272, kifungu cha 13(2) na (3) kidogo mimi vinanikwaza sana, kwa sababu kimoja kinatoa *rule* nyengine na chengine kinatoa *rule* nyengine ya kisheria. Sasa kifungu cha 13(2) Mhe.Naibu Spika, kinatamka kwamba hakuna mtumishi wa JKU atakayeshikizwa katika taasisi isipokuwa baada ya kutimiza vigezo na masharti yaliyowekwa na bodi na kuidhinishwa na Mkuu wa JKU.

Sasa mimi hapa napata mashaka Mhe. Naibu Spika, kwamba masharti yaliyowekwa na bodi, sasa kutakuwa kuna masharti mengine, yaani bodi haitofuata masharti ya JKU, yaani katika zile sheria zake za kibodi yaani ule utaratibu wao. Kwa sababu mimi nilihisi labda bodi itakuwa inafuata masharti na sheria za JKU, wao ndio wanajaribu kuzifanyia kazi kisheria kama bodi, kwa sababu tukiweka hivi maana yake bodi itakuwa na vitu vyengine. Sasa na vigezo zaidi vya uajiri wa humu tunaangalia zaidi sifa za mtu ambaye amepata sifa za JKU, za kiulinzi na kiusalama. Sasa na sifa za uaskari tunazijua, askari hana sifa mbaya, vyenginevyo labda itokezee kufanya sifa mbaya ndipo unaweza askari yule ukamuondosha. Lakini mtu yeyote ambaye amepitia JKU na amepata sifa za JKU, maana yake tayari mtu huyo ana sifa za kiuaskari, sasa kama kuna sifa nyengine za ziada za bodi ukiachilia sifa hizi, mimi kidogo zinanipa mashaka.

Katika kifungu cha 3 Mhe. Naibu Spika, wao wameelezea kwamba hakuna mtumishi mpya atakayeajiriwa kuitumikia taasisi, isipokuwa awe ametimiza vigezo na masharti yaliyowekwa na bodi na ametimiza sifa zinazohitajika. Hakuna mashaka kwa sababu tayari huyu ni mtumishi mpya, lakini yule wa mwanzo ni mtumishi ambaye aliyeshikizwa, maana yake ametoka JKU anakuja katika suala la uajiri katika hii taasisi. Kwa hivyo, lile ndio linanipa mashaka, kwa sababu tayari huyu keshatoka JKU sifa anazo. Mimi nafikiri kwa huyu mpya ndio tungekiweka hiki kifungu, kwamba lazima afuate masharti ya bodi na masharti ya vikosi vya SMZ, kwa sababu yeye ni mpya na hakupata mafunzo ya aina yoyote, lakini tayari mtu ana mafunzo, tayari mtu ni muajiriwa sasa bodi sijui itakuwa na masharti gani mengine ya ziada katika masuala ya kiulinzi ili kuweza kuelewa.

Mhe. Naibu Spika, mimi nafikiri Mhe. Waziri hiki kifungu angekiangalia zaidi kuona, *otherwise* itakuwa nina wasi wasi bodi ikajakuwa ina mambo ya vigezo, kukawa kuna mambo ya upendeleo katika masuala ya ajira kukatafutwa sifa ambazo alimuradi kumkosesha mtu haki yake ya msingi ya kuajiriwa. Tunajuana kwamba mtu tayari ameshakuwa JKU lakini tayari unamuwekea pingamizi ya masharti ya bodi, mimi sioni kama kutakuwa kuna ulazima huo kwa yule mtu ambaye tayari amefikiwa, labda kwa yule mtu ambaye tayari ni mtumishi mpya anataka kuajiriwa ndio tunaweza kumuwekea masharti hayo ya JKU na masharti ya bodi.

Mhe. Naibu Spika, kwa kumalizia katika ukurasa wa 273 kwenye kifungu cha 18 na kifungu cha 20 kidogo vina tofauti, baina ya Mwenyekiti na Mjumbe, hapa tayari tunasema Mwenyekiti wa bodi atatumika na kushika nafasi hiyo kwa kipindi cha miaka minne na anaweza kuteuliwa tena kwa kipindi kingine kimoja cha ziada, lakini kwa Wajumbe kinasema kwamba katika kifungu cha 20 kwamba Wajumbe wa bodi ya taasisi ya ulinzi watafanya kazi kwa kipindi cha miaka mitatu. Sasa sioni kama hii itakuwa vyema kwa sababu *experience* imejengeka katika mabodi, kwamba Mwenyekiti na Wajumbe wanakuwa wanakwenda sambamba.

Mhe. Rais anamteua Mwenyekiti, Mwenyekiti yeye tayari akishateuliwa na kuapishwa na Waziri naye ndio anateua Wajumbe wa bodi kwamba watu hawa kazi zao zinakwenda sambamba. Nahisi haitakaa vizuri na sio vyema kwamba Mwenyekiti aende miaka minne, lakini Wajumbe waende miaka mitatu. Maana yake Mwenyekiti atakuwa amebakiwa na mwaka mmoja lakini Wajumbe wake wameshaondoka.

Sasa nafikiri tungeliliangalia hili tukatafuta namna wote wakenda sambamba ama wote waende miaka mitatu au wote wende miaka minne sambamba na watakavyomaliza wamalize sambamba.

Mhe. Naibu Spika, baada ya hayo machache kwa niaba yangu na kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Kwahani naunga mkono hoja, nakushukuru Mheshimiwa. (*Makofi*)

**Mhe. Mussa Ali Hassan:** Ahsante Mhe. Naibu Spika, kwa kunipatia nafasi ya kuweza kuchangia Mswada huu wa Sheria ya Taasisi ya Ulinzi ya JKU. Kwanza sina budi kumshukuru Mheshimiwa Waziri kwa Mswada wake huu alioutoa wakati mzuri hasa wakati huu ambao Zanzibar imepata maafa kuanzia hivi leo ya kuhusu mambo ya ulinzi.

Kwa hivyo tutakuwa na nafasi kubwa ya kuweza kuchangia nafasi hii kuhusu ulinzi na kuhusu vikosi vyetu ambavyo vitakuwa vinalinda hasa sehemu za utalii, na kikawa na jina maalum la JKU. Hivi sasa tunaelewa kwamba tunavyo vikosi vyetu vya SMZ ambavyo vinalinda sehemu zote za ulinzi, lakini hivi sasa tutakuwa na kikosi maalum ambacho kitaitwa JKU ambacho kitakuwa na mafunzo maalum ya ulinzi ya utalii.

Kwanza nataka kujua atakapokuja Mhe. Waziri atuhakikishie kwamba hiki kikosi maalum cha JKU kitakuwa na mafunzo ya aina yake peke yake kuhusu utalii, au kitaunganisha ulinzi ambao tunao hivi sasa. Kwa kweli hivi sasa tunacho kikosi chetu cha JKU na ndicho kinachukua nafasi ya ulinzi sehemu nyingi katika sehemu zetu za utalii. Lakini kwa hivi sasa kwa alivyotwambia Mhe. Waziri, kwamba kikosi hiki kitakuwa ni kikosi maalum ambacho kwanza kitakuwa na Wakurugenzi na kitakuwa chini ya Mkuu wa JKU, kwa hivyo kinakuwa hiki kikosi ni kikosi kipya ambacho kitakuwa na shughuli zake za utalii hapa nchini.

Mhe. Naibu Spika, kwa kweli hivi sasa tutakapokuwa na kikosi hiki cha JKU ambacho *special* kwa mambo ya utalii ningelipenda kujua kwamba kitakuwa cha muundo gani, kwamba tutapata kushirikishwa ndani ya Serikali na JKU wenyewe au kitakuwa ni *brigade* maalum ya mambo ya ulinzi hasa katika sehemu zetu za utalii, Zanzibar.

Mhe. Naibu Spika, vile vile kuhakikisha kwamba hiki kikosi watu wake wanaweza kwenda kusoma maalum kama vile vikosi ambavyo vya Jeshi sasa hivi vinasoma mambo ya kuongoza mambo ya *specialist* ya mambo ya usalama wa nchi wa kimataifa, na hawa ndugu zetu hawa wa JKU ambao wanategemea kuwa ulinzi mimi naona ni wazi kwamba wasomeshwe masomo maalum, kwa vile wanakwenda kukaa sehemu za utalii na kule utalii inatakiwa kuhakikishwa kwamba watu wake wanalindwa kimataifa, sio kama kulinda kikawaida. Kwa hivyo wahakikishwe kwamba watu hawa wanapata masomo maalum nchi za nje.

Mhe. Naibu Spika, kwa vile kikosi hiki cha JKU kitakuwa cha kisasa kwa hivyo kwanza tuhakikishe kwamba kinapata mafunzo pamoja na zana zote za kisasa ambazo zinahitajika kwenye ulinzi, hasa katika sehemu zetu za utalii, katika sehemu kubwa kubwa hasa mahoteli ambayo yana *grade* kubwa za utalii hapa nchini.

Tuhakikishe kwamba tunapata vyombo ambavyo vinahitajika hasa mambo ya magari ya kisasa kwa ajili ya ulinzi, boti ambazo sehemu nyingi watakazolinda utalii zitakuwa katika maeneo ya bahari. Tuhakikishe kikosi hiki kwanza kinapata vitu vipya kwa ajili ya usafiri wa bahari, kwa hivi sasa tulivyozoea kikosi chetu cha JKU bado hakijakuwa na ulinzi katika bahari na katika ulinzi wa utalii tuhakikishe JKU inapata boti za kisasa, ambazo zitasaidia kuhakikisha wahalifu wanaovunja mahoteli au wanaokamata watalii wanaposafiri katika bahari. JKU wawe na uwezo wa kuhakikisha kwamba wanapambana na watu kama hawa kwa ajili ya usalama wa nchi yetu.

Mhe. Naibu Spika, hivi sasa tunahakikisha kwamba utalii unakua zaidi na ulinzi ndio utakuwa zaidi, tuhakikishe Mheshimiwa Waziri atakapokuja atuhakikishie kwamba vikosi vyake vitakuwa vya muundo gani, vitakuwa na muundo wa *brigade* ya JKU iliyopo sasa au itaongezwa nguvu kwa ajili ya kupata ajira vijana wetu wapya. Kuhakikisha kwamba kuna JKU ya ulinzi maalum kwa ajili ya utalii na hiyo ndio itaweza kuhakikisha kwamba vijana wetu wanapata ajira katika sehemu ya utalii ikiongozwa na mwenyewe Mheshimiwa Waziri.

Mhe. Naibu Spika, kuongeza nguvu katika sehemu ambazo tunahakikisha zinalindwa na vikosi vyetu vya JKU katika utalii, tunaomba kwamba Mheshimiwa Waziri atakapokuja kuhakikisha kutoa maamuzi yake ya kusaidia ulinzi, ahakikishe kwamba vikosi vinaajiriwa na JKU, lakini malipo yake yanakuwa chini ya wakurugenzi ambao wanalipwa na Mkurugenzi maalum wa Utalii. Mbali na vikosi vyetu vile vya ulinzi vya ndani ya SMZ na hivi viwe maalum kwa ajili ya ulinzi wa utalii.

Kwa kweli sitokuwa na mchango mkubwa sana isipokuwa naomba kwamba Mhe. Waziri ahakikishe kwamba analitangazia taifa jinsi vikosi hivi vitakavyoongeza nguvu katika sehemu ya JKU, na vitakuwa na *brigade* ya aina yake ya ulinzi wa utalii.

Mhe. Naibu Spika, hapo ndio mwisho wa mchango wangu sina zaidi isipokuwa tunasubiri maelezo ya Mheshimiwa Mawaziri, ili tuhakikishe utalii unaimarika na usalama unaimarika kwa ajili watalii wetu wanaokuja nchini, kusitokee matatizo kama hivi sasa yanavyotokezea. Ahsante sana. *(Makofi)*

**Mhe. Mohammed Mbwana Hamad:** Mhe. Naibu Spika, awali ya yote na mimi namshukuru Mwenyezi Mungu kunijaalia jioni hii kupata fursa ya kuchangia angalau kwa muhtasari Mswada wa Sheria ya Kuanzisha Uwakala wa Ulinzi wa Jeshi la Kujenga Uchumi na mambo yanayohusiana na hayo. Lakini pia nachukua nafasi ya kukupongeza wewe kunipa nafasi hii. Vile vile nachukua nafasi kumpongeza Mheshimiwa Waziri pamoja na Mwenyekiti wa Kamati inayohusika na Mswada huu na Wajumbe wote kutuwasilishia Mswada huu mbele yetu na hivi tunauchangia.

Mhe. Naibu Spika, kwa kweli kuanzishwa kwa wakala wa ulinzi ni jambo zuri hapa Zanzibar kwa sababu tumeona kwamba Zanzibar ya leo imebadilika sana, sio Zanzibar ile ambayo waliiona wazee wetu na hata sisi katika utoto wetu. Zanzibar ya zamani ilikuwa ni aibu sana kulia milio ya risasi ovyo ovyo katika mitaa, lakini inasikitisha Zanzibar ya leo risasi zinalia kila wakati kwa majambazi kama ni jambo la kawaida, jambo ambalo kwa kweli ni aibu kubwa kwa nchi ya Zanzibar.

Mhe. Naibu Spika, inasikitisha sana muda mchache tu uliopita tumepata taarifa kwamba Darajani wamekamatwa majambazi pale wanarusha risasi, bahati nzuri walinzi wetu wamefanya kazi nzuri wakapambana na majambazi hao, inasemekana kwamba majambazi miongoni mwao wametiwa mikononi na hivi sasa wako hospitali. Hongera sana kwa jeshi la Polisi kwa kuwakamata majambazi hao. Kwa hivyo Serikali kuweka wakala wa ulinzi hapa Zanzibar kwa ajili ya kulinda utalii na mengineyo, si utalii tu, ni jambo ambalo linafaa na limekuja kwa wakati muafaka, kwa mujibu wa mazingira ya Zanzibar ya leo.

Mheshimiwa nikiendelea na mchango wangu niende ukurasa wa 270 kifungu (c) ambacho kinatoka ukurasa wa 269 malengo ya taasisi ya ulinzi.

(c) Inasema; "Kurahisisha upatikanaji wa huduma za ulinzi wa uhakika na ulio bora".

Mhe. Naibu Spika, hili ni jambo zuri lakini namuomba Mheshimiwa Waziri aangalie kwamba hivi sasa vikosi vyetu vingi vya Zanzibar vina mapungufu mengi ambayo yanadhoofisha shughuli mbali mbali za kiulinzi. Kwa hivyo kurahisisha upatikanaji wa huduma za ulinzi wa uhakika ni jambo zuri. Mheshimiwa Sentensi hii ni fupi lakini ina maana kubwa sana namuomba Mheshimiwa Waziri aone kwamba vikosi vyetu hivi, sasa vina mapungufu ya mambo mbali mbali yakiwemo ya mavazi, njia za mawasiliano, magari na mambo mengine yanayopolekea kuwa na uhakika wa ulinzi.

Kwa hivyo nimuombe Mheshimiwa Waziri hili aliangalie vizuri na atueleze amejipanga vipi kuliboresha jeshi la JKU ili kuweza kupambana na mambo mbali mbali yanayojitokeza hivi sasa kama hayo ambayo tumeyaona hivi leo, na mengineyo ambayo yanatokea katika sehemu za utalii za majambazi kuwavamia watalii. Jeshi linahitaji kuboreshwa kwa kupewa silaha za kisasa, nguo, buti, na mafunzo endelevu ya kuweza kupambana na mambo mbali mbali yanayohusiana na majambazi ambao wanaingia katika nchi yetu ya Zanzibar.

Mhe. Naibu Spika, niendelee na mchango wangu ukurasa wa 271 kifungu cha 9(2) sifa za kuteuliwa Mkurugenzi.

9(2) "Mswada unasema mtu hatoweza kuteuliwa kuwa Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi isipokuwa awe na sifa zifuatazo:

a) Awe Afisa wa Juu kutoka Idara Maalum".

Huyu ndio ambae anaweza kuteuliwa kuwa Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi. Mimi naona kwamba katika Idara Maalum tuna vikosi zaidi ya kimoja hapa tunazungumza uwakala huu kuwepo JKU. Kwa hivyo napendekeza kwamba huyu Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi atoke ndani ya Jeshi hili hili la JKU wala asitoke katika kikosi

chengine. Kwa sababu akitoka katika jeshi hili la JKU itakuwa ni vizuri zaidi kwa vile itakuwa hili Jeshi amelizoea vya kutosha kuliko kutoka katika kikosi chengine cha Idara Maalum.

Mhe. Naibu Spika, nikiendedelea na mchango wangu niende katika ukurasa wa 272 kifungu cha 13(4) kifungu hiki kinasema.

> 13(4) "Watumishi wa taasisi ya ulinzi, lakini nambari 4 watumishi wa Taasisi watalipwa mishahara na maposho mbali mbali kulingana na Sheria ya utumishi".

Hawa watumishi wa taasisi wanahitaji kutokana na ugumu wa kazi zao waangaliwe vizuri sana pamoja na kulipwa maposho, mishahara kwa mujibu wa utumishi wa umma lakini tuone kwamba tunawaongezea kazi na unapomuongezea mtu kazi basi ni vyema umuongezee na lishe. Kwa sababu utakapomuongezea lishe itakuwa ana uwezo wa kuifanya ile kazi kwa ufanisi na kwa uwazi na kwa uadilifu wa hali ya juu. Kwa hivyo kuboreshwa mafao yao ni jambo ambalo linafaa kabisa ili waweze kufanya kazi zao kwa uaminifu na kwa uadilifu.

Mhe. Naibu Spika, mchango huu kwa jioni hii kwa mimi utoshe na nikupongeze kunipa nafasi hii. Ahsante sana Mheshimiwa. *(Makofi)*

**Mhe. Ismail Jussa Ladhu:** Mhe. Naibu Spika, naomba nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia kuendelea kuwa hai, kuwa wazima jioni hii tukiendelea na shughuli zetu katika chombo hiki cha wananchi wa Zanzibar. Nikushukuru na wewe kwa kunipa nafasi vile vile na mimi kuchangia katika Mswada huu.

Mhe. Naibu Spika, vile vile nitumie fursa hii kuwapa pole wananchi wa Jimbo la Mji Mkongwe lakini pia na wananchi wengine wa Zanzibar wanaotumia au kufanya shughuli zao katika Jimbo la Mji Mkongwe hasa maeneo ya Darajani kutokana na kadhia ambayo imetokezea mchana wa leo. Lakini vile vile na mimi niungane na wenzangu kuwashukuru na kuwapongeza Jeshi la Polisi kwa kazi nzuri ambayo wameifanya leo.

Kwa hakika nilikuwepo maeneo ya Mji Mkongwe huko wananchi wengi wamesifu kwa jinsi Jeshi la Polisi lilivyoonesha ustadi na umahiri mkubwa katika kuwafuatilia toka maeneo ya juu huko mpaka kufika Darajani, na wakaweza kuwadhibiti na inasemekana mmoja alipoteza maisha pale pale, lakini na wengine wameweza kukamatwa, nawapongeza sana Jeshi la Polisi.

Mhe. Naibu Spika, kabla ya kuingia katika Mswada naomba vile vile nitumie fursa hii kuna suala moja, nimekuwa nikitafutwa sana na niwaambie waliokuwa wakinitafuta kwamba madhumuni ya kikao hiki ingekuwa tabu sana kulizungumza suala lao, lakini kwa sababu Mswada huu upo ningemuomba Mheshimiwa Waziri atumie fursa hii kama ataweza atakapokuja kufanya majumuisho atusaidie. Tumekuwa tukipata mawasiliano mengi sana kutoka kwa vijana wa Zanzibar waliopelekwa katika mafunzo ya JKT Bara kwa ahadi kwamba hatimae watachukuliwa na kuajiriwa katika Jeshi la Wananchi wa Tanzania.

Mhe. Naibu Spika, sikufichi tumekuwa tukipokea mawasiliano mengi sana wakilalamika kwamba, yale tuliyokuwa tukiyapigia kelele mara kwa mara kwamba mfumo wa Muungano huu sio wa haki na wao wanayaona kule. Wenzao wameshachukuliwa kwa maelfu waliokuwa nao pamoja katika mafunzo yale, lakini Wazanzibar waliochukuliwa pengine hawazidi 20 hadi sasa. Kwa hivyo wanasema suala hili linawatia unyonge na wamekuwa wakisema, maana yake katika kule kuhangaika wanasema mpaka tuwatafutie nambari ya Rais wa Zanzibar.

Hilo nawambia haliwezekani masuala kama hayo, maana hata mimi sina nambari ya Rais wa Zanzibar, sio jambo kama hilo kila mtu anaweza kuwa nalo. Lakini imefikia hali kuwa namna hiyo. Kwa hiyo ningemuomba Mhe. Waziri atakapokuja hebu atusaidie.

Hasa kwa sababu ninavyoamini mimi na kama sivyo atanirekebisha, kwamba mara nyingi vijana hawa huwa wanapitia JKU kwanza halafu ndio wakapelekwa JKT na baadae kuombewa nafasi za uwajiri katika Jeshi la Wananchi. Kwa hivyo ningeomba Mhe. Waziri akija hilo atusaidie kutupa maelezo, kuna nini kwamba tumeshindwa kusimamia haki zetu na vijana wetu wale waliopelekwa kule wakaweza kupata haki zao. Wanasikitika kwamba wamekuwa wakitumikishwa sana, wanafanyishwa kazi ngumu na bado wanafanya kazi wakiamini kwamba kuna matumaini ya kuweza kuajiriwa katika jeshi, lakini kila nafasi zikija wanaachwa wao, wenzao wanachukuliwa na kusogezwa mbele.

Mhe. Naibu Spika, sasa nije katika Mswada wenyewe. Katika hili mimi ufahamu wangu ni kama inavyosomeka tafsiri ya Kiingereza. Ingawa nataka nikiri kwamba kama nilivyosema jana tunapitia haraka haraka kwa sababu ya namna ya muda mfupi tuliopewa Miswada hii. Kwamba neno lililotumika katika Kiingereza ni kuanzisha *Security guard.* Sasa nilikuwa nataka nisaidiwe hilo la jumla kwamba kwa madhumuni hayo.

Samahani Mhe. Naibu Spika, nashangaa maana simu zote nimezima na bado *microphone* inalia. Naomba Mheshimiwa wambie mafundi wako washughukie mitambo yao, maana simu zote nimezima sijui kwa nini inafanya gh'asia *microphone* ndani ya Baraza lako. Ndio nasema ni huko kwao maana nikinyamaza kusema na huko inanyamaza. Lakini haikupi utulivu kuchangia.

Mhe. Naibu Spika, nilikuwa nasema kwamba dhana yenyewe ilivyoelezwa kwamba ni *Security Guard*. Sasa ningeomba hili la jumla kwanza Mhe. Waziri akija atusaidie, kwa madhumuni ya kuanzisha *Security Guard* hii. Je, kutaajiriwa vijana wapya ambao mahsusi watatumika katika *Security Guard* au watakuwa ni vijana wa JKU ambao watatumika kwa shughuli za *Security Guard* ili kuongeza ufanisi, kuongeza ulinzi, kuongeza mapato na masuala mengine kama hayao.

Mhe. Naibu Spika, naliuliza hili kwa sababu nataka kusema, kwamba dhana yenyewe mimi naikubali na naipongeza na kwa sababu hii nampongeza Mhe. Waziri kuleta Mswada huu katika Baraza hili, ni jambo zuri. Lakini nahofia kwamba ikiwa tunazungumzia kuajiri vijana wapya, hasa kwa hali ya Zanzibar ilivyo, inaweza kuchukua muda mrefu mpaka chombo hiki kuja kusimama chenyewe.

Sasa ikiwa vijana waliokuwemo katika Idara Maalum za SMZ sio JKU tu, zote kwa ujumla wake kwa maana ya KVZ, JKU, KMKM, Kikosi cha Mafunzo na Kikosi cha Zimamoto na Uwokozi, wanalalamika kuhusu huduma zao nyingi kwamba bado hazipo, haki zao, stahiki zao, maeneo wanayoishi na mambo mengine, bado yana matatizo mengi sana. Kwamba tunapotaka kuongeza ajira je, hatuoni kwamba kuna haja ya kushughulikia hawa walikuwepo na kuwapatia mahitaji yao kamili halafu ndio twende kwengine. Tunasema hilo ningeomba tusaidiwe kwamba ikiwa waliokuwepo ndio watakaotumika katika wingi maalum ambao itakuwa ni *Security Guard,* basi hilo sina tatizo nalo.

Mhe. Naibu Spika, la pili nataka hilo niwatahadharishe zaidi wenzangu; naona hamasa zimekuwa kubwa kuowanisha kwamba kuja kwa Mswada huu kutapelekea mambo tuliyokuwa tunayaona yamalizike, tusijidaganye Mhe. Naibu Spika. Ni kweli kwamba ukirusu kuwa na *Security Guard*, ukaruhusu na taasisi binafsi kuja kutumia kutapunguza matukio. Lakini sio kama tunavyohimiza siku zote masuala ya ulinzi ni lazima yashirikishwe wananchi wanyewe. Kama wananchi hawajajenga imani na wakatoa mashirikiano kwa ukamilifu, bado tatizo la uhalifu litaendelea kuwepo pale pale.

Mhe. Naibu Spika, Wazanzibari wengi wanaamini kwamba tatizo la kutokuwa na vizuizi katika uingiaji wa watu Zanzibar na kutoka, nalo pia linachangia kwa kiasio kikubwa katika uhalifu wa aina ambayo tunaushuhudia katika miaka ya karibuni. Sasa nasema tunakaribisha dhana hii, lakini naogopa isijeikatujengea hamasa kwamba matatizo haya kama walivyochangia baadhi ya wajumbe kwamba yatakwisha, si kweli Mhe. Naibu Spika. Kuna hatua nyingi nazo zifanyike kwa pamoja ndio tuione Zanzibar inarudi kuwa pahala salama kama ilivyokuwa tumezoea.

Mhe. Naibu Spika, baada ya kusema hayo naomba niingie katika madhumuni ya Mswada na yale maudhui ya Mswada. La kwanza nianze katika kifungu cha 2 cha Mswada kinasema:

> "Bila ya kuathiri masharti ya sheria hii, Sheria hii itasomeka sambamba na Sheria ya JKU".

Nadhani tumezoea kusoma sheria inapotajwa inatajwa na Sheria Nambari yake na mwaka gani ndio utaratibu wetu. Kwa hivyo nadhani hili lingekaa vizuri. Haidhuru kisheria ukitaja kama kuna Sheria inaitwa JKU *Act* kisheria inatambulika. Lakini nadhani kwa uwandishi mzuri ingependeza pia ikatajwa ile Sheria Nambari yake na mwaka wake.

Mhe. Naibu Spika, la pili ni katika kifungu cha 3 ambacho kinatoa tafsiri ya maneno mbali mbali yaliyotumika. Nilikuwa nahisi labda katika huo utaratibu uliotumika wa kuletwa Mswada kwa haraka mambo mengi hayajakaa vizuri. Kwa mfano naomba Mhe. Waziri akija atusaidie kwamba anapotwambia;

"Mtumishi Aliyeshikizwa" maana yake ni mtumishi yeyote ambaye anatumikia Taasisi ya Ulinzi ya JKU kwa njia ya kuazimwa kutoka JKU au katika tasisi nyengine".

Hizi taasisi nyengine bila ya kuzifafanua inaweza kuwa yoyote tu ama ni taasisi nyengine za ulinzi ama ni Idara Maalum za SMZ hebu naomba hili tuweke sawa, tuwe na *drafting* nzuri.

Mhe. Naibu Spika, jengine lipo katika tafsiri ya neno JKU, limeandikwa,

"JKU" maana yake ni Jeshi la Kujenga Uchumi lililoundwa chini ya kifungu cha 3 cha Sheria".

Sheria ipi? Haikutajwa, kwa hivyo nilikuwa nadhani kwamba na hilo vile vile lisawazishwe.

Mhe. Naibu Spika, kuna suala na liko katika tafsiri lakini nililiowanisha na maudhui yaliyokuwemo ndani, tafsiri ya neno Mkurugenzi. Hapa pameandikwa Mkurugenzi katika tafsiri. Lakini ndani katika kifungu kinachotambulisha kinataja Mkurugenzi Mkuu, halafu vifungu vinavyofuata vinaendelea kutumia neno Mkurugenzi, nilikuwa naomba Waziri akija atuweke sawa. Hili hata katika Kamati nimeangalia hawakuliona, inawezekana kwa sababu ya uharaka wenyewe, basi Mhe. Waziri waziri atusaidie je, huyu ni Mkuregenzi Mkuu ama ni Mkurugenzi. Litakalokubaliwa kwamba ndio sahihi basi ndio litumike katika Mswada mzima.

Mhe. Naibu Spika, jengine limeshaelezwa na kamati na mimi naungana nao na namuomba Waziri katika hili akubali kwamba tuwekewe sawa, hawa katika lugha ya kiswahili, kinachoanzishwa ni taasisi, ni wakala au ni shirika. Kwa sababu haya maneno yanatumika kwa pamoja na yanaleta ukakasi kidogo. Kwa hivyo nilikuwa nafikiri ni muhimu angetuwekea sawa. Linaonekana hata katika tafsiri ya neno wakala pale imeandikwa wakala maana yake ni Shirika la Ulinzi lilianzishwa chini ya sheria hii. Kwa hiyo nilikuwa naomba hayo tuwekewe sawa.

Mhe. Naibu Spika, ikiwa hilo limefahamika nadhani tukishaelewana kwamba tunaanzisha Wakala, Taasisi au Shirika, basi hilo hilo ndio lionekane katika sheria nzima tuwe tumekaa vizuri.

Jengine naomba Mhe. Waziri anisaidie katika kifungu cha 4 hasa kifungu kidogo cha (2) hapo kinasema,

4(2)"Taasisi ya Ulinzi itakuwa ni wakala wa Serikali kwa masuala yote ya Ulinzi kwa mujibu wa Sheria hii na itakuwa ni chombo kinachojitegemea, chenye muhuri wake na itakuwa na uwezo wa..."

Ambao umetajwa pale. Sasa hiki chombo kinachojitegemea katika lugha ya Kisheria mara nyingi tumezoea kuona kwamba ni *Board Cooperate.* Lakini nilitaka kujua kwamba kwa madhumuni ya maudhui yaliyotajwa humu ndani, Waziri na Serakali imejiridhisha kwamba inataka chombo hiki kiwe ni *Board Cooperate*. Kwa sababu nilikuwa nadhani kwa maumbili ya shughuli zake yaani *nature* ya kazi zake, napata wasi wasi kukipa *status* kwamba ni chombo kinachojitegemea. Lakini nipo tayari kusikiliza hoja za serikali katika hili zinasemaje.

Mhe. Naibu Spika, lakini naomba vile vile kuridhishwa katika kifungu cha 5. Hiki kifungu kimeandikwa: "Malengo ya Taasisi ya Ulinzi". Sasa katika lugha ya kawaida ya kuanzisha lugha za biashara au taasisi tumezoea kuna vitu vinaitwa *vision* and *mission*. Sasa kama hapa haya ni malengo ya jumla tu, hiyo ndio *mission*. Je, kuna haja ya *mission* kuandikwa ndani ya Sheria. Mimi nilikuwa nadhani kama ni *mission* inapaswa kuwemo katika nyaraka zake nyengine na zinaweza kuonekanwa pale katika taasisi yenyewe. Lakini kuingiza *mission* ndani ya sheria mimi nilikuwa naona si sawa. Mimi nadhani kazi za shirika ambazo zipo katika kifungu cha 6 zingetosheleza kuainisha hayo masuala yaliyokuwa yametajwa.

Mhe. Naibu Spika, kifungu kingine ninachotaka kukitolea maoni ni kifungu cha 6, kazi za shirika. Hapa napata matatizo, kama ningelikuwa nimekiafiki kifungu cha 5 na kukitumia kwa madhumuni ya kukijengea hoja, imetajwa kwamba shughuli za Taasisi ya Ulinzi malengo yake;

(a) "Kusimamia na kuimarisha huduma za ulinzi katika maeneo ya uwekezaji na utalii".

Katika hali ya kawaida ungeamini kwamba hayo ndio maaeneo mawili tu ambayo taasisi hii itahusika nayo. Katika tafsiri kumeelezwa maeneo ya uwekezaji ni nini.

Sasa mimi nilikuwa nadhani kwanza hilo niweke sawa na niwekewe sawa baadae. Kwa sababu katika hali ya kawaida *Security Guard* wanatumika sio katika maeneo ya uwekezaji tu hata kama mimi nina biashara yangu, hata kama nyumba yangu binafsi kama nikiwa na uwezo wa kulipa na nikahitaji nilindwe, kwa nini izuilike? Sasa nilikuwa naomba ufafanuzi. Je, imekusudiwa hiyo kwamba ni maeneo ya uwekezaji kwa mujibu wa tafsiri iliyotolewa ndani ya Mswada na Utalii tu, au ni shughuli ya jumla ya kibiashara ambayo inaweza ikafanyika.

Lakini kama hivyo ndivyo Mhe. Naibu Spika, kifungu cha 6 takriban katika kila kijifungu kidogo kuanzia a - k, vifungu vingi vinataja huduma za ulinzi wa Utalii na nyenginezo, sasa hii nyenginezo ndio inanipa mashaka, kama tumeamua kama inafanya shughuli zote kwa ujumla wake, basi sheria iwe *clear* iseme hivyo. Mswada unatakiwa uje ujifafanue kuliko kutaja hivi.

Mhe. Naibu Spika, kwa madhumuni hayo hayo pia nauliza swali kama nilivyouliza kule mwanzo. Katika kifungu cha 6(c) kinasema:

> "Kazi za Shirika zitakuwa:-
>
> (c) "Kutoa ushauri wa kiulinzi na kiusalama kwa watalii, wadau wa utalii na taasisi nyenginezo"

Ningeomba maelezo, hizi taasisi nyenginezo zimekusudiwa nini na kama tutasema sio nyenginezo maana yake ni zote. Sasa kama ni zote sasa kwa nini tunazitaja maalum. Ningeomba hii tuwekewe vizuri tupate kuelewa.

Mhe. Naibu Spika, mimi kidogo naogopa uandishi wa kifungu cha 6(j) katika "Kazi za Shirika" imesema:

> "6(j)"Kuweka viwango vya ada ambazo zitapaswa kulipiwa na wawekezaji kuhusiana na mambo yanayohusiana na huduma ya ulinzi".

Sasa hapa nikapata swali najiuliza binafsi. Kwamba hawa ni wale wanaopewa huduma baada ya kuzitaka wameingiana mkataba au nikiamua tu kwamba mimi napiga doria kuja kulazimisha na wewe pia unipe ada. Naliuliza hili Mhe. Naibu Spika, kwa sababu tayari katika Sekta ya Utalii kuna malalamiko makubwa sana kwamba wamekuwa wanatozwa kila siku ada mpaka inafanya ushindani wa utalii baina ya Zanzibar na nchi nyengine, inakuwa tabu kwa sababu ya gharama kubwa zilizokuwepo hapa ndani.

Mhe. Naibu Spika, hivi karibuni Chama cha Wawekezaji katika Sekta ya Utalii ZATI, walitoa waraka wakielezea suala hili la malalamiko ya wawekezaji katika sekta ya Utalii. Ningeomba na hilo pia tuliwekewe sawa.

Mhe. Naibu Spika, nikiondoka hapa naomba niingie katika kifungu cha 7. Hapa imesemwa uwe wa taasisi hii ya Ulinzi iliyoanzishwa. Nimepata kidogo mashaka, kwanza kwenye 7(b) inasema:

> 7(b)"Kuratibu shughuli za utoaji huduma za ulinzi wa kampuni au taasisi binafsi".

Sina hakika na lugha lakini kama ndivyo nilivyofahamu kama sivyo Mhe. Waziri atanisaidia. Kwamba tumekusudia Wakala huyu ndiye atakaye kuwa sasa anaratibu shughuli za kampuni kama *Security Guard* na nyenginezo? Au wale bado kwa sababu wanafanya shughuli zao wanajitegemea na wamesajiliwa huko, wana mamlaka yao mengine, ningeomba kuwekewa sawa. Lakini ambapo nimepata mashaka zaidi ni 7(c), Taasisi hii imepewa uwezo wa;

> 7(c)"Kukamata na kupekuwa sehemu au mali yoyote inayoshukiwa au mtu yeyote aliyevunja kifungu chochote cha Sheria hii au sheria nyengine na kumfikisha kwenye mamlaka husika."

Mhe. Naibu Spika, hiki mimi sikiungi mkono, labda kiandikwe vyengine. Kwa sababu kuna mamlaka maalum katika nchi hii na ni ya kipolisi. Polisi imepewa mamlaka yale kwa sababu imefunzwa askari wake kukabiliana na raia. Sasa unapokipa chombo kingine kama taasisi hii inayotaka kuanzishwa, mamlaka ya kukamata na kupekuwa sehemu au mali yoyote inayoshukiwa au hata mtu yeyote aliyevunja kifungu chochote cha sheria hii. Wao wanapewa mamlaka ya kukamata, najiuliza hatuukaribishi mgongano baina yao na polisi. Ningeomba hili pia tuwekewe wazi, kama si hivyo itakuwa tabu kidogo kuunga mkono sehemu hii ya Mswada.

Mhe. Naibu Spika, kuna baadhi ya vifungu nilikuwa nimeshavitolea maoni kwamba vinalingana na vile ada ambazo zinaongezeka kila siku. Lakini jengine nasema hilo hilo la ada limejitokeza katika kifungu cha 8.
Naokoa muda kwa sababu sitaki kusoma kimoja kimoja, lakini na kifungu cha 8 vile vile hasa 8(a) kinazungumzia bado suala hilo hilo. Nikiondoka hapo kifungu cha 10 nimeshakitolea maelezo mapema kwamba lile neno Mkurugenzi Mkuu na Mkurugenzi, tuweke sawa lipi hasa limekusudiwa kutumika.

Mhe. Naibu Spika, jengine nimeomba na hili linahusika zaidi katika kifungu cha 13 kwamba kinasema;

> 13(3)"Hakuna mtumishi mpya atakaeajiriwa kuitumikia Taasisi isipokuwa awe ametimiza vigezo na masharti yaliyowekwa na Bodi na ametimiza sifa za ajira za Idara Maalum za SMZ."

Ndio maana nikasema niweke sawa tusije tukaweka taasisi ambayo bado inaitegemea serikali, haijaweza kusimama wenyewe tukaongeza gharama huku. Hivi sasa wapiganaji wetu tunashindwa kuwahudumia ipasavyo.

Mhe. Naibu Spika, ni kifungu cha 14 (1)(d) kwenye Wajumbe wa Bodi, nilikuwa nataka Waziri anisaidie kwa nini Mjumbe anaetoka Wizara ya Biashara anapelekwa na Waziri wa Biashara, lakini Wajumbe wanaoteuliwa na Waziri kutoka Tasisi ya Shirika la Utalii wateuliwe na Waziri wasipendekezwe na Waziri anaehusika na Sekta ya Utalii kama ilivyokuwa kwa biashara, ningeomba hilo pia anisaidie.

Mhe. Naibu Spika, Kifungu cha 17, nitakisema kwa jumla kwa sababu ya kuokoa muda maana yake nina mambo mengi, nahofia muda nisiwakwaze wenzangu.

Kwanza nimepata tatizo la kuhusu uwajibikaji, nidhamu na utumishi. Hapa kuna vifungu vinatoa mamlaka kwa vyombo vya taasisi hii kushughulikia, lakini pia kuna *reference* huku mwanzo ni ya Tume ya Utumishi ya Idara ya Maalum, hebu Waziri atuwekee wazi. Mamlaka yepi yanaanza kwanza na yanaishia na yanaingia mengine; kusije kukatokezea mgongano hasa kwa wale wafanyakazi ambao watakuwa wanatoka katika taasisi ya JKT. Kuna nidhamu zake za kijeshi tunazijua na vitu vyengine kama hivyo.

Mhe. Naibu Spika, kuna suala ambalo nilikuwa naomba kuliuliza kuhusiana na Mwenyekiti wa Bodi, kifungu cha 15hapa ukitizama kifungu cha 15 ukija ukakilinganisha na kifungu cha 19, 19 kinataja sifa za wajumbe wa bodi.

Sifa za mjumbe wa bodi zimewekwa kubwa zaidi kuliko sifa za mwenyekiti. Sasa nikasema kibinaadamu tu utapokuwa na hali kama hii kweli ile nidhamu na utii itakuwepo kwa Mwenyekiti wa Bodi ambaye kiwango cha elimu na sifa zake nyengine ziko chini sana ukilinganisha na sifa za wajumbe wa bodi, nilikuwa naomba hili pia atusaidie.

Lakini jengine Mhe. Mwenyekiti kifungu cha 20 nadhani kifungu cha 20 (1) na kifungu cha 22(2) kuna maneno yanajirejea yanahitaji yaondoshwe kwamba wajumbe wa bodi watatumia miaka 3, haidhuru yameongezwa maneno katika hii 20 (2) lakini bado kuna maneno nadhani hayahitajiki, tuseme ndani ya kifungu kimoja juu ya suala la muda wa miaka 3.

Halafu Mhe. Naibu Spika, kuna kifungu cha 21 ambacho hata Kamati ninasikitika hawakukiona nao, kifungu cha 21 kimefanya rejea kwamba Waziri anaweza kumkatisha au kumsimamisha mjumbe yoyote aliyemteua chini ya kifungu cha 11(1) (c),(d) na (e) hakuna kifungu cha 11(1) (c), (d) na (e) hiki nadhani kimekusudiwa kifungu cha 14(1) na hivyo vijitoto vyake ambavyo ndio vinavyozungumzia wale wajumbe wa bodi. Kwa hivyo nadhani hilo lirekebishwe.

Mhe. Naibu Spika, kifungu cha 23(2) suala la kwamba Bodi inatakiwa kuweka kumbukumbu ninakubali lakini sheria ya kusema kwamba Bodi kabla kikao kijacho kinatakiwa kupitisha kumbukumbu nadhani si suala la sheria Mhe. Naibu Spika. Suala la kupitisha kumbukumbu ni mambo ya kanuni za ndani za Taasisi, hayapaswi kuwemo ndani ya sheria kwamba kawaida katika kikao kinachofuata tunasoma kumbukumbu kwanza ni jambo la kawaida sidhani kama linapaswa kuingizwa ndani ya sheria. Kwa hivyo 23(2) nadhani kitizamwe upya.

Mhe. Naibu Spika, kifungu cha 24 kinazungumzia maamuzi ya Bodi, kwa jumla sina tatizo nacho, tatizo langu liko katika 24(2) (3) na hii ni mfumo wa kufanya maamuzi kwa kusambaziana nyaraka halafu mkatia saini mkaridhika.

Katika Taasisi nyengine tumezoea inawezekana ni sawa lakini ninajiuliza kwa chombo kinachofanya shughuli za ulinzi kufanya maamuzi kwa njia hii tunaridhika kwamba ni sawa, likija likitokezea tatizo mtu akahoji kwamba kumeghushiwa wakati mumeshafanya maamuzi na pengine yameathiri kitu fulani hasa katika masuala ya ulinzi, mimi nilikuwa ninamuomba Mhe. Waziri hivi avitazame upya 24(2) na (3) kwamba maamuzi bado yafanywe ndani ya Bodi katika vikao kukitokezea suala la dharura Bodi iitishwe ya dharura, lakini kuliko kufanya maamuzi kwa kusambaziana nyaraka.

Halafu Mhe. Naibu Spika, nimalizie haraka haraka naomba vile vile katika kifungu cha 30(1) kwenye matumizi ya bajeti napendekeza ule mstari wa tatu tuongeze meneno na Bodi yaani kwa kuzingatia sheria zinazohusiana na fedha za Serikali. Fedha za Taasisi ya Ulinzi zitatumika kugharamia matumizi yaliyopangwa na kuidhinishwa kabla kuanza katika, na Bodi katika utekelezaji wa shughuli za Taasisi. Nadhani tuipe Mamlaka Bodi ya kuidhinisha hayo kama ilivyotajwa kwa sehemu nyengine.

Halafu Mhe. Naibu Spika, kwenye sehemu ya mwisho sehemu ya nne ambayo kuna mengineyo. Kwanza ninaipongeza Kamati kwamba imeona suala moja la kurekebisha adhabu. Mara nyingi nimekuwa ninasema kwamba bado leo mwaka wa nne tangu tulivyolisema ndani ya Baraza la Wawakilishi, tukaahidiwa na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu kwamba kungekuja sera juu ya adhabu mpaka leo hatujaletewa. Kwamba unaposema miezi 6 jela inawiana na kiasi gani cha thamani ya fedha, kwa sababu kila sheria inayokuja inaweka viwango vyake tu. Kumekuwa hakuna uwiano na hapa leo ndio ilikuwa inahidhirika kabla ya kamati haijarekebisha. Kwamba inasema Chuo cha Mafunzo si chini ya miezi 6 au kulipa faini isiyozidi milioni 6 wakati asubuhi hapa tulipopitisha sheria haioani kabisa na adhabu hizi, nilikuwa naomba liwekwe sawa.

Mhe. Naibu Spika, na katika hii sehemu ya mwisho ya mengineyo naomba pia nimsaidie Waziri ili arekebishe sheria yake ikae vizuri, katika kifungu cha 38 na nitagusa 40 kidogo, nimalizie ndio cha mwisho.

Kifungu cha 38 Mhe. Naibu Spika, pale mwisho kabisa panasema kwa mujibu wa maelekezo yaliyomo katika sheria ya Tume au sheria ya fidia kwa wafanyakazi, sheria ya Tume ipi sheria iko kimya.Tume tunazo tele hapa na sheria ziko hatujaliweka sawa. Lakini vile vile hii sheria ya fidia ya wafanyakazi ninafikiri kama tulivyosema kule kwengine, muhimu ikatajwa na nambari yake na mwaka wake tukajua tunafanya *reference* ya sheria zipi.

Mhe. Naibu Spika, cha mwisho, katika sehemu hii ya Nne ni kifungu cha 40; hapa kidogo naona kuna mgongano katika mamlaka ya Waziri kutunga Kanuni 40(b) inasema kuweka viwango vya ada kwa huduma mbali mbali zinazotolewa na shirika. Sasa haya mamlaka kapewa Waziri hapa, lakini ukija ukisoma 16(i) mamlaka haya pia imepewa Bodi. Sasa ninafikiri Waziri aje atuwekee sawa mamlaka haya tunampa nani ili tupate kufuta sehemu moja. Haiwezekani mamlaka tukaipa Bodi au tuweke kwamba bodi inapendekeza Waziri ndie anaeidhinisha, ninafikiri suala liwekwe baina ya 16(i) na hiki cha 40(b).

Vile vile kwenye 40(d) hapo mstari wa chini ndio narudia ile concern yangu imeandikwa Waziri pia atatunga Kanuni kuhusiana na taratibu zinazohusiana na utumishi wakati huku mwanzo tumeshataja taratibu zake za utumishi. Tumeitaja Tume ya Utumishi Idara Maalum na nidhamu zake, nilikuwa naomba hili tuwekwe sawa Mhe. Naibu Spika, ili tuweze kuwa na sheria ambayo imekaa vizuri.

Baada ya kusema hayo Mhe. Naibu Spika, samahani kuna nukta moja ndogo ya mwisho hicho kifungu cha 40, Kamati katika ukurasa wao wa mwisho kabisa wamependekeza kuongeza kifungu kipya cha 40(1) na (2). Hapa sikukisoma lakini nilitaka kusema tu ile hoja yangu kwamba ukiona nyongeza ya Kamati inapendekeza tena kufanya rejea katika masuala ya utumishi. Sasa nikasema liwekwe *clear* hili utumishi wao unaongozwa na sheria zipi taratibu zipi kusitokezee mgongano, ninafikiri Waziri atapata muda wa kuliwekwa vizuri ili Jumatatu tutakapokuja kupitisha kama kumejitokeza binaadamu kutokuyaona tuweke vizuri.

Sasa Mhe. Naibu Spika, kama nilivyosema awali kabisa pamoja na kwamba ninaendelea kusikitika kama nilivyosema jana pengine tungepata mapema tungepata kuchangia vizuri zaidi. Tungepata kukupeni ushauri mkubwa zaidi kwa wataalam wa mambo haya. Kwa hivyo nasema tena Serikali iache huu mtindo wa kutuletea miswada kwa hati ya dharura namna kama hii lakini baada ya kusema hayo nasema napongeza hatua ya kuleta mswada huu. Napongeza hatua ya kufikiria kuunda chombo kama hiki ni ubunifu wa aina yake katika Taasisi kama hizi. Nimtakie kila la heri Waziri, nasema mswada huu ninauunga mkono mia kwa mia. Ahsante.

**Mhe. Fatma Mbarouk Said:** Ahsante Mhe. Naibu Spika, na mimi kunipa fursa hii ya kuchangia machache katika mwada huu wa sheria ya kuanzisha sheria ya Taasisi ya Ulinzi ya Jeshi la Kujenga Uchumi Zanzibar na mambo mengine yanayohusiana na hayo. Pia nimshukuru Mhe. Waziri kwa kuwasilisha mswada huu mbele yetu. Vile vile niipongeze Kamati kwa kazi kubwa ambayo ameifanya na nakubaliana na yale ambayo Mwenyekiti wa Kamati ile ya Katiba na Sheria imewasilisha vile vile.

Mhe. Naibu Spika, kwa kweli miswada mara nyingi sisi tunaitazama kwenye madhumuni na sababu. Ukitizama kwenye madhumuni unaipata picha nzima ya mswada ule namna ilivyouelezea kwa ufanisi madhumuni na sababu. Lakini Mhe. Naibu Spika, mswada wetu huu umeelezea kwa ufupi ambapo huwezi kupata ile picha yenyewe halisi na napenda ninukuu kwa kusema kwamba sababu na madhumuni ya mswada huu imesema kwamba "mswada huu unapendekeza kuanzisha Shirika la Ulinzi ambalo litakuwa chini ya JKU".Hupati ile picha halisi ya kwamba madhumuni hasa na sababu ya kuanzishwa. Kwa hivyo Mhe. Naibu Spika, kwanza nilikuwa na hilo.

Nikitazama miswada mengine ambayo kwanza nimtake samahani Waziri wa Ardhi, Maji na Nishati labda kuusoma mswada wake kabla ya kuwasilishwa mbele yetu na unasema kwamba kwa mfano Mswada wa Kuanzisha Sheria ya Kamisheni ya Ardhi na naomba Mhe. Naibu Spika, niombe kunukuu huo mswada ambao umesema:

"Madhumuni na sababu ya mswada huu una lengo la Kuanzisha Sheria itakayosimamia masuala ya ardhi katika kujenga uimara wa uongozi na usimamizi wa raslimali ya ardhi kwa ajili ya matumizi bora na maendeleo kwa taifa. Nikiendelea inasema kwa lengo hilo mswada huu unapendekeza kuanzishwa kwa Kamisheni ya Ardhi kwa ajili ya kuongoza na kusimamia utekelezaji wa masharti ya sheria hii na pamoja na sheria nyengine zinazohusiana na masuala ya ardhi".

Kwa hivyo Mhe. Naibu Spika, hapa inaeleza ile hali halisi ya kuanzishwa mswada ule, sasa hapa unasema madhumuni na sababu muswada huu unapendekeza kuanzisha Shirika la Ulinzi ambalo litakuwa chini ya JKU. Lakini vile vile ukenda kwenye mswada wenyewe huku vile vile inajenga kama wenzangu walivyokwisha kusema kwamba sheria ya kuanzisha Taasisi ya Ulinzi ya Jeshi la Kujenga Uchumi Zanzibar na mambo mengine yanayohusiana na hayo.

Sasa huku inasema ni taasisi lakini huku ni shirika. Sasa hapa Mhe. Naibu Spika, kuna utata kidogo wa haya maelezo, huku ni taasisi na huku ni shirika na shirika tunajua kwamba kama ni shirika, basi shirika siku zote linakuwa linajitegemea, linakuwa halipati ruzuku kutoka Serikalini, mara linakuwa linajitegemea na vile vile naona kwamba Taasisi hii bado itakuwa ndio kwanza inaanza kwa kusema kwamba inajiendesha wenyewe kama shirika itakuwa ni tatizo kubwa.

Mhe. Naibu Spika, huu mswada kwa kweli ni mdogo ambao una sehemu nne lakini na vifungu ni vingi sana lakini Mhe. Naibu Spika, mimi naomba nichangie kidogo tu na kwa sababu sina mengi na kama wenzangu walivyosema huu mswada wenyewe ni wa dharura sijui kwa nini Serikali inaleta miswada ya dharura, kwani ninahisi inakuwa kidogo ni tabu kwa ghafla kuchangia na hata semina kama wajumbe tutakuwa hatujapata.

Kwa hivyo tukipata semina vile vile inatujengea uwezo zaidi wa kuweza kuchangia miswada hii lakini vile vile wanasema lisilobudi hutendwa na wamenambia wenzangu kwamba miswada hii tuipitie tuisome vizuri na yale ambayo tunaweza kuyashauri basi tushauri ipasavyo.

Mhe. Naibu Spika, nikienda kwenye sehemu hii ya pili kifungu cha 35 kinasema kujiuzulu kwa mjumbe wa Bodi. Napenda ninukuu:

> "Mjumbe yoyote wa Bodi anaweza kujiuzulu wakati wowote kwa kuandika barua kwa mamlaka ya uteuzi akitaja siku ya kujiuzulu kwake na iwapo itatokea barua hiyo kutokueleza siku ya kujiuzulu kwake, tarehe ya kupokelewa barua hiyo itahesabika ndio siku ya kujiuzulu kwa muhusika".

Mhe. Naibu Spika, niseme tu kwamba mbali ya hili suala la kujiuzulu mwenyewe lakini vile vile kama mjumbe labda ata-*miss* ku-*attend* vikao vile vile kuwe na basi kama ni Mwenyekiti wa Bodi au labda ni Katibu wa Bodi aweze kumuondosha kwenye nafasi hiyo kwa sababu atakuwa hana uajibikaji.

Mhe. Naibu Spika, kifungu 23 vikao vya Bodi sina tatizo nalo, lakini naendelea sehemu ya tatu ambayo inasema kifungu cha 31 Taasisi ya Ulinzi itafungua na kuendesha *account* moja au zaidi katika benki yoyote itakayoidhinishwa na Bodi. Mhe. Naibu Spika, hapa niseme nitilie mkazo kwamba hizi *account* ziwe zaidi ya moja, kwa sababu kutakuwa na mambo mbali mbali, kutakuwa na akiba ambayo ni fedha za akiba ambazo zitakuwa na watu mbali mbali pengine ni mshahara, pengine tuseme labda mfanyakazi wa Taasisi hiyo atakuwa pengine hayupo. Lakini mshahara wake utaweza kuwekwa kwenye *account* ya *deposit* vile vile revenue *account* ni lazima kuwepo kwa kuweka yale mapato na vile vile *capital account* ambayo itakuwa ina-*deal* na kuweka, labda mambo ya labda miradi kama Taasisi hiyo itakuwa na miradi mbali mbali kwa hivyo ni lazima *account* hiyo iwepo.

Vile vile, nikenda kifungu 32 Mhe. Naibu Spika, kinasema ukaguzi wa hesabu, Taasisi ya Ulinzi itafanyiwa ukaguzi wa mahesabu kulingana na taratibu za sheria inayohusika na ukaguzi wa hesabu za Serikali, lakini hapa haijatajwa kwamba ni ukaguzi upi labda au ni nani ambaye atahusika na ukaguzi. Imesema lakini imejificha ficha na si mara nyingi inakuwa inawekwa wazi kwenye sheria mbali mbali kwamba hapa ni Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ambaye atakagua. Hapa ilikuwa vile vile si vibaya kusema kwamba Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa hesabu atakagua.

Vile vile, kinasema kifungu cha 34 taarifa ya kila mwaka kifungu 34 kinasema;

> "Mkurugenzi atawasilisha kwenye Bodi taarifa ya utendaji ya mwaka ndani ya miezi mitatu baada ya kukamilika kwa mwaka wa fedha itakayowasilishwa kwa Mkuu wa JKU ambaye naye ataiwasilisha kwa Waziri ambayo itaelezea pamoja na mambo mengine".

Vile vile, hapa naona kwamba Mkurugenzi atawasilisha kwenye Bodi taarifa ya utendaji ya mwaka ndani ya miezi mitatu baada kukamilisha mwaka wa fedha itakayowasilishwa na Mkuu wa JKU ambaye naye atawasilisha kwa Waziri ambaye atatekeleza pamoja na mambo mengine. Sasa vile vile kuna mahesabu ya mwisho wa mwaka ambayo vile vile yanatakiwa yawasilishwe kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali naona pia sijaiona katika sheria yetu hii.

Mhe. Naibu Spika, baada ya hayo nasema kwamba kwa niaba ya wananchi wa Amani walionituma kuja humu kuwasemea ndio kazi kubwa ambayo nimekuja hapa kuwasemea kwa hivyo nachukua fursa hii kumpongeza Mhe. Waziri na vile vile naunga mkono hoja mia kwa mia.

**Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi:** Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kunipa nafasi hii na mimi kuchangia mswada huu wa Sheria ya Kuanzishwa Taasisi ya Ulinzi ya Jeshi la Kujenga Uchumi Zanzibar na mambo mengine yanayohusiana na hayo. Mhe. Naibu kwanza nimpongeze Mhe. Waziri kwa kutuletea mswada huu katika Baraza letu hili la Wawakilishi. Lakini pia niseme kwamba nitaungana na Mhe. Waziri pale ambapo taratibu zote zilizoletwa hapa zitafuatwa kadri inavyowezekana.

Mhe. Naibu Spika, mimi nije katika kifungu cha 29 katika mswada kinachosema kwamba sehemu ya tatu hiyo mapato na matumizi na usimamizi wa fedha, kifungu cha 29 kinasema;

> "Vyanzo vya Mapato vya Taasisi ya Ulinzi, vyanzo vya mapato ya Shirika vitakuwa ni ruzuku kutoka Serikalini, fedha kutoka kwa wahisani, mikopo kutoka taasisi za fedha kwa ajili ya kuendesha shughuli" na hiyo inaendele.

Mhe. Naibu Spika, niliombe Jeshi lisitegemee vyanzo vya mapato kutoka Serikalini tu na pia mikopo kutoka kwa wahisani, pia niseme kwamba Jeshi lianzishe vyanzo vyao wenyewe vya mapato ambavyo vitawaletea tija katika shughuli zao. Pia vyanzo hivyo serikali nayo isimame kidete ili kuwasimamia au kuwaongezea vyanzo hivyo ili wazidi kuzalisha vizuri zaidi.

Mhe. Naibu Spika, nikija katika kifungu cha 20 ambacho kinasema muda wa Mjumbe wa Bodi. Wajumbe wa Bodi ya Taasisi ya Ulinzi watafanya kazi kwa kipindi cha miaka mitatu. Hapa Mhe. Waziri bado naomba ufafanuzi, Bodi itakuwa ya muda gani? Kwa sababu inasema kwamba kifungu cha 2 kila Mjumbe wa Bodi, isipokuwa anayeingia kwa wadhifa wake atatumikia wadhifa huo kwa kipindi cha miaka mitatu na anaweza kuteuliwa tena kwa kipindi kingine kimoja.

Sasa niseme kwamba hii Bodi hapa anasema kwamba Wajumbe wa Bodi wa Taasisi ya Ulinzi watafanya kazi kwa kipindi cha miaka mitatu, lakini Mjumbe mwingine wa Bodi atateuliwa tena. Naomba nijuulishwe kwamba bodi itakuwa na muda wa miaka mingapi?

Mhe. Naibu Spika, nije katika kifungu cha 22 kinachosema kujiuzulu kwa Wajumbe wa Bodi. Mjumbe yeyote wa Bodi anaweza kujiuzulu wakati wowote kwa kuandika barua kwa mamlaka ya uteuzi akitaja siku ya kujiuzulu kwake na iwapo itatokea barua hiyo kutokueleza siku ya kujiuzulu kwake, tarehe ya kupokelewa barua hiyo itahesabika ndio siku ya kujizulu kwa muhusika.

Mhe. Naibu Spika, niseme pamoja na kupokelewa kwa barua hiyo lakini Bodi ihakikishe kwamba huyo mtu anayejiuzulu anajiuzulu kwa sababu gani? Halafu vile vile ihakikishe Bodi kwamba huyu mtu anayejiuzulu anaondoka katika Bodi yuko salama, hapana tatizo litakalotokea hii Bodi ihakikishe hivyo kwamba huyu mtu anayejiuzulu kaondoka hapa yuko salama.

Mhe. Naibu Spika, pia nije katika kifungu cha 15 kinachosema kwamba sifa za Mwenyekiti wa Bodi. Mtu hatoweza kuteuliwa kuwa Mwenyekiti isipokuwa awe na sifa zifuatazo.

Awe ni Afisa wa juu, mwenye cheo cha Kanali na kuendelea au kinacholingana na hicho au mstaafu kutoka taasisi ya ulinzi na usalama aliyefikia cheo hicho au kinacholingana nacho.

Mhe. Naibu Spika, niseme kwamba ikiwa watu wote watakuwa na elimu hizo na sasa hivi tunao vijana wetu ambao pengine wana sifa zaidi ya hizo na kila siku kuteuliwa mtu huyu aliyekuwa kwenye sehemu ya Kanali na nini, lakini sasa hawa vijana ambao sasa hivi tayari na wao wanahitaji uajiri. Je, Mhe. Naibu Spika, huoni hili litakuwa ni tatizo kwa vijana wetu?

Mhe. Naibu Spika, kwa kuwa wapo wengine wanataka kuchangia niseme baada ya hapo ahsante nashukuru.

**Mhe. Hamza Hassan Juma:** Mhe. Naibu Spika, nakushukuru kunipa nafasi hii na mimi nikatia nyalio katika mswada huu wa Sheria ya Kuanzisha Taasisi ya Ulinzi ya Jeshi la Kujenga Uchumi Zanzibar, pamoja na mambo mengine yanayohusiana na sheria hii.

Mhe. Naibu Spika, mimi kwanza nataka niipongeze serikali kupitia Mhe. Waziri kwa kusikia kilio chetu cha muda mrefu juu ya Jeshi letu la Kujenga Uchumi kuanzisha taasisi ambazo zitakazoweza kusaidia kulinda maendeleo na uchumi wa Zanzibar.

Mhe. Naibu Spika, hili kwa bahati nzuri nikiwa Mwenyekiti wa Kamati ya Kusimamia Afisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa katika awamu ya mwanzo ya serikali hii ya awamu ya saba, nilikuwa Mwenyekiti ambao JKU ilikuwa chini ya Kamati yangu.

Nashukuru sana kwamba malezi mazuri ambayo niliyoyafanya basi Mjumbe wangu wa Kamati sasa hivi amekuwa ndiye Mwenyekiti wa Kamati hii. Kwa hiyo, najaribu kumuangalia hapa amekwenda kuswali, lakini kimsingi kwamba tunashukuru kuwa elimu tuliyokuwa tunaitoa imeweza kuwajenga Waheshimiwa na wao sasa hivi wanaweza kuongoza kamati kwa ufanisi mkubwa. Hii inadhihirishwa jinsi ya marekebisho ya mswada walivyoiyaleta kamati, kwa kiasi fulani maeneo mengi ya marekebisho ya mswada ambayo kamati imependekeza kwa kweli mengi ni maoni ya kitaalamu, lakini vile vile yamejikita zaidi katika masuala ya kisheria.

Kwa hiyo, mswada huu Mhe. Naibu Spika, tulipokuwa kwenye kamati kipindi hicho kabla ya mabadiliko ya wizara, ambayo wizara hii ilikuwa chini ya kamati yangu, tulijenga mahusiano mazuri na wenzetu Jeshi la Kujenga Taifa, Tanzania (JKT). Na tulianzisha mahusiano baina ya Kamati ya Baraza la Wawakilishi kupitia JKU na JKT, tulikwenda Tanzania Bara karibu mara mbili, tukenda tukajifunza mambo mengi kutoka kwao.

Kwa kweli yale ambayo tuliyoyaona mazuri wenzetu waliyoyafanya JKT basi tuliwaomba wawe karibu sana na ndugu zetu au vijana wetu wa JKU ili sasa yale maendeleo ambayo wenzetu waliyofikia, basi waweze kuwarithisha na wenzao ili na sisi tuwe na Jeshi la Kujenga Uchumi ambalo litakuwa na shughuli kama tafsiri ya Jeshi la Kujenga Uchumi linavyosema.

Sasa katika ziara zile tulitembelea makambi mbali mbali, sina haja ya kuyataja kwa sababu ni mengi tuliona wenzetu kwamba wameanzisha Shirika la Uchumi ambalo linaitwa SUMA JKT (Shirika la Uchumi la Jeshi la Kujenga Taifa). Kwa hiyo, katika Shirika lile la Uchumi la Jeshi la Kujenga Taifa ndio zikazaliwa hizi *annex* ikiwemo hili Shirika la SUMA GUARD. Kwa hiyo, SUMA GUARD imetoka ndani ya Shirika la SUMA JKT.

Sasa tulivyojaribu kuangalia namna gani ya muundo kwa ile taasisi yao ya ulinzi, hapa kidogo ndio nimehisi kuna tofauti ndogo baina ya Shirika la Ulinzi na JKT na mfumo wa muundo wa Shirika la Ulinzi letu la JKU. Hapa labda Mhe. Waziri aje anisaidia kidogo namna ya utendaji na utekelezaji wa hizi shughuli zitakavyokuwa. Kwa sababu wenzetu kule tulivyojifunza, wao walitwambia kwa sababu tuliwauliza inakuwaje mnakuwa na shirika ndani ya chombo cha ulinzi, kwa sababu chombo cha ulinzi ni chombo cha kutoa huduma za ulinzi.

Sasa mmeanzisha chombo chengine lakini cha kibiashara, wao ndio wakatwambia kwanza hawakuwanzisha tu SUMA GUARD lakini kwanza walianzisha SUMA JKT. Kwa hiyo, shirika lile wanaweza wakatoa *annexes* tofauti tofauti mfano ndio hiyo moja hii ya ulinzi. Wanaweza wakaanzisha Shirika la Viwanda, wanaweza wakaanzisha Shirika la Kilimo yaani wanaweza wakatengeneza *annex* mbali mbali kupitia lile Shirika la Kiuchumi, kwa sababu linakuwa limeundwa na kazi yake ni kutafuta mambo ambayo ya uzalishaji mali peke yake.

Sasa sisi Shirika letu hili la Ulinzi la JKU au kwa jina jengine lolote kwa sababu hapa imeandikwa taasisi, halafu kuna sehemu imeelezwa kama itakuwa ni wakala kwa vyovyote tutakavyokubaliana lakini kimsingi tuje na maudhui yale ambayo yaliyokusudiwa.

Mimi hofu yangu moja kwamba tukisema tunaanzisha Shirika la Ulinzi au Taasisi ya Ulinzi ina maana JKU ikija ikitaka kuanzisha huduma za viwanda, ina maana tuje na sheria nyengine. Lakini kama tungelifanya kama tulivyojifunza kwa wenzetu JKT kwanza tukaunda Shirika la Kiuchumi halafu haya mengine yakawa yanabuniwa tu katika lile shirika lenyewe, kwa sababu itakuwa kazi yake ndio hiyo. Basi nafkiri ingelikuwa ni jambo jepesi zaidi kuliko pengine hivi tulivyojibana sisi.

Mhe. Naibu Spika, ukiangalia hata muundo wa ile JKT na SUMA JKT na *SUMA GUARD*, kule Mkuu wa SUMA *GUARD* anakuwa ni Mkuu wa JKT. Kwa hiyo, hizi nyengine zinazoundwa hizi *annex* zinakuwa yule msaidizi wake ndio anakuwa yeye ndiye mtendaji mkuu na mratibu mkuu wa shughuli za siku zote za uzalishaji wa SUMA JKT. Kwa hiyo, hata ikianzishwa SUMA GUARD ya ulinzi anakuwa yeye ndiye mratibu, ikianzishwa SUMA *Industry* kwa jina lolote watakaloita linalohusu viwanda na vitu vyengine inakuwa ni kazi rahisi, hakuna haja tena kila siku kurudisha au kutengeneza sheria nyengine. Na haya tuliyaona matunda yake, tumeona vijana wengi ambao wanaochukuliwa kujenga taifa kwenye JKT wengi wao wanachukuliwa serikalini katika vyombo vya ulinzi na usalama, na wale wengine wanaamua wanakwenda kujitegemea.

Lakini kwa wale wengine ambao hawakubahatika kuajiriwa basi wanawaajiri wenyewe JKT kupitia katika haya mashirika yao, wanakuwa sio askari lakini wanakuwa ni jeshi ambalo lilokuwa chini ya SUMA JKT au *SUMA GUARD*.

Sasa hapa ndio maana nikasema Mhe. Waziri hebu aje anisaidie zaidi kwa hili shirika letu, na kwa sababu labda huko mbele nikija katika uteuzi wa Mkurugenzi, Mwenyekiti wa Bodi tutakuja jaribu kuangalia zaidi kusije kukawa na mgongano wa utendaji na kwa sababu hiki chombo chenyewe kinaongozwa kijeshi jeshi. Sasa kutakuwa kuna Mkuu wa JKU, halafu huku kutakuwa na Mkurugenzi wa hii Tasisi yetu sijui tutaita nini kule kuna *SUMA GUARD* huku inaweza kuwa *SUMA GUARD* maana yake inatokana na JKU. Sasa kwa jina lolote litakaloitwa lakini katika mambo ya kiutawala na katika mambo ya amri kusije kukatokezea migongano tofauti tofauti.

Mhe. Naibu Spika, nakuja katika kifungu cha 4 cha sheria hii, kuanzishwa kwa Taasisi ya Ulinzi ya JKU pamoja na kazi zake.

Kifungu hiki cha 4 (1) kinasema kutakuwa na Taasisi ya Ulinzi ya JKU inayojuulikana kama “Taasisi ya Ulinzi ya JKU” ambayo itakuwa chini ya Mkuu wa Jeshi la Kujenga Uchumi. Kwa hiyo, hapa taasisi hii ina maana itakuwa chini ya Mkuu wa JKU. Halafu taasisi yenyewe inasema (2) Taasisi ya Ulinzi itakuwa ni wakala wa serikali kwa masuala yote ya ulinzi kwa mujibu wa sheria hii na itakuwa ni chombo kinachojitegemea, chenye muhuri wake na itakuwa na uwezo wa kushtaki na kushtakiwa kujipatia, kumiliki, kutoa mali, kuingia mikataba ya makubaliano na kufanya mambo kama ilivyoelezwa hapo, kufanya shughuli nyengine yoyote.

Sasa chombo hiki kama inavyoeleza sheria kitakuwa ni chombo ambacho kinachojitegemea, kitakuwa na haki ya kushtaki na kushtakiwa, lakini vile vile na kumiliki mali. Sasa ndio maana pale niliposema kwamba hapa kuna Mkuu wa JKU ambaye yeye ndiye kutakuwa na Taasisi ya Ulinzi kama nilivyosema ambayo mkuu wake atakuwa Mkuu wa Jeshi la Kujenga Taifa. Halafu huku mbele kuna Mkurugenzi ambaye atateuliwa na Rais vile vile, halafu kutakuwa na Mwenyekiti wa Bodi atakayeteuliwa vile vile na Rais.

Sasa ndio hapa nikaona huu utendaji wake, lakini kwa sababu kama ingelikuwa kama ile sheria ya wenzetu kule Tanzania Bara JKT ingelikuwa Mkuu wa JKU yeye ndiye Kiongozi Mkuu wa Shirika la Uchumi la Jeshi la Kujenga Uchumi, halafu zile taasisi nyengine kama hiyo ya ulinzi, ya uchumi, ya viwanda na vitu vyengine ingelikuwa msaidizi wa Mkuu wa JKU yeye *automatic* kwa cheo chake angelikuwa anshika ile nafasi bila ya kutajwa tena Mkurugenzi mwengine.

Mhe. Naibu Spika, kwa sababu hapa hofu yangu anaweza kuwa kuna Mkuu wa JKU, halafu kuna msaidizi wake pengine, halafu akaja akateuliwa mtu mwengine ndiye anakuja kushika hii taasisi kukaja kukawa kuna viswahili sio sawa sawa, nahisi kidogo kunaweza kuleta *conflict.* Lakini kwa kuwa wenzetu kamati walipata na kama alivyosema Mhe. Fatma hapa kutokana na umuhimu wa hii sheria hasa katika masuala sasa hivi ya ulinzi, hasa katika sekta ya utalii imekuja kwa hati ya dharura.

Kwa hiyo, hatukupata muda wa kupata kuuliza maswali mengi kiuhuru kabisa na waziri, ili tunapokuja kupitisha sheria hii yale maswali mengi ya kienyeji tukawa tumeshayapatia jawabu za kimsingi. Sasa lakini pamoja na yote hayo Waswahili wanasema anavyoanguka ndivyo achinjwe hivyo hivyo, lakini sasa kwa Zanzibar tumchinje Kiislamu tusije tukaanza kumkata miguu.

Mhe. Naibu Spika, hizo ni sehemu ya hofu zangu naamini Mhe. Waziri pamoja na Mwanasheria Mkuu wanaweza wakatusaidia sana jawabu ya masuala yetu.

Kifungu cha 5 kinasema malengo ya taasisi ya ulinzi. Anasema Taasisi ya Ulinzi itakuwa na malengo yafuatayo.

Kusimamia na kuimarisha huduma za ulinzi katika maeneo ya uwekezaji na utalii; kusimamia, kuimarisha maeneo ya ulinzi katika kukuza uchumi wa nchi; kurahisisha upatikanaji wa huduma za ulinzi wa uhakika na ulio bora. Sasa mimi nilikuwa nashauri tuongeze neno hapa , hii ya 5(a) iseme, "Kusimamia na kuimarisa huduma za ulinzi katika maeneo ya uwekezaji, biashara na utalii". Kwa sababu hawa walinzi wapya wa JKU watakuwa tofauti na wale ambao kazi yao kubwa itakuwa pengine kwenda kulinda viongozi au taasisi za serikali. Hawa zaidi watatumiwa sana na wafanyabiashara wakubwa, lakini vile vile makampuni ya kitalii na wawekezaji lakini hapa hatukuwataja wafanyabiashara.

Mimi nadhani tukiweka na wafanyabiashara itasaidia sana kwamba wafanyabiashara na wao watakuwa na nguvu zaidi sasa ya uimara wa biashara zao kiulinzi kwa kuchukua hawa watu ambao, kwa mujibu wa sheria watakuwa wanamiliki silaha. Kwa hiyo, ilikuwa ni nyongeza yangu katika eneo hilo.

Mhe. Naibu Spika, nikija kifungu cha sita kazi za taasisi ya ulinzi; hapa (a) inasema, "Kutoa huduma za ulinzi wa kibiashara kwa taasisi zinazoshughulikia huduma za utalii na vyenginevyo". Sasa huku neno "biashara" halikujitokeza lakini huku mbele limejitokeza. Kwa hivyo ndio maana kuna umuhimu lile neno likaanza huku nyuma ili liendane na huku ilivyokusudiwa.

Halafu (b) kufanya doria ya ulinzi katika maeneo ya uwekezaji na mengineyo. Sasa hapa Mheshimiwa unajua kwa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania masuala ya ulinzi na usalama ni masuala ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Hapa kuna swali nilikuwa nataka kuliuliza lakini naona kama jawabu imenijia kabisa kichwani, maana yake nilitaka kujiuliza, unapozungumza kwamba taasisi hii itakuwa na kazi ya doria. Je, tuna sera ya ulinzi ya Zanzibar? Maana yake suala la ulinzi ni jambo la Muungano basi angalau tungekuwa na sera ya ulinzi wa ndani ya Zanzibar.

Sisi sera ya ulinzi kwa kuwa ulinzi ni jambo la Jamhuri ya Muungano hapa Mhe. Mwanasheria Mkuu nitaomba kidogo aje aumize kichwa, atusaidie kututolea ufafanuzi. Ufafanuzi atakaonisaidia mimi atawapa jawabu mpaka na wale wanaosema kwa nini Zanzibar kuna vikosi na vinamiliki silaha. Sasa na hii taasisi yetu itakuwa ni ya JKU

lakini iko *semi private, semi government*. Kwa sababu humu katika hii sheria ya kumiliki silaha mpaka sasa hivi kwa Zanzibar hatuna. Jamhuriya Muungano wa Tanzania wanayo sheria ya raia kumiliki silaha, lakini sisi Zanzibar sheria hiyo hatuna. Lakini kupitia sheria hii ina maana hao walinzi wa JKU, ulinzi binafsi hawa watakuwa wanamiliki silaha? Sasa wanapokuwa wanakuja kufanya doria, ndio maana nikasema kuwe na miongozo ya kutosha kusije kukawa kuna migongano katika masuala mazima ya doria na wenzetu, pengine Jeshi la Polisi.

Hili tusilione dogo kwa sababu sio mifano mizuri kutoa, lakini wakati mwengine huwa kuna majibizano ambayo hayapendezi katika maeneo ya kijamii baina ya askari wa taasisi tofauti, wakati mwengine mpaka kutishiana ngumi. Sasa sitaki kuzitaja taasisi zenyewe nikatengeneza mzizi wa fitina, lakini kwa wale ambao wamebahatika kuona kuna baadhi ya askari wanaovaa *uniform* tofauti walikuwa wanatunishiana misuli kila mmoja yeye ndiye mwenye nchi.

Sasa na hapa kwenye hizi doria na kwa sababu kutakuwa kuna JKU *solder* na JKU *Private Company* au *Security Company* kusije kukatokea migongano. Kwa hivyo, lazima nafikiri huku mbele kuna kanuni ambayo Mhe. Waziri atakuja kuitunga, basi katika eneo moja aje aweke utaratibu mzuri wa hizi doria, lazima kuonekane na zitajwe katika ile kanuni na taasisi nyengine katika ule utaratibu wa doria.

Mhe. Naibu Spika, labda wanapofanya doria lazima kuwe kuna *information* zimepatikana au zimepelekwa kupitia kwa *RPC* wa Jeshi la Polisi. Kwa sababu na yeye inawezekana katika operesheni zake amepanga doria lakini hawa JKU *Private Company* au *Private Security Company* wakaja wakagongana katika utendaji wa shughuli zao.

Chengine (c) imeelezwa hapa kazi yao nyengine itakuwa kutoa ushauri wa kiulinzi na kiusalama kwa watalii, wadau wa utalii na taasisi nyenginezo. Kwa hiyo ina maana ukiacha mambo ya ulinzi lakini watakuwa na kazi nyengine ya ziada ya kutoa taaluma.

Vile vile, (d) inasema, "kutoa mafunzo ya kiulinzi na usalama kwa taasisi zinazojihusisha na utalii na nyenginezo". Kwa hiyo, ina maana hii taasisi ambayo tumeiunda ina maana itakuwa na mamlaka ya kutoa taaluma mpaka kwa *Security Company* nyengine *Private* ambazo zinafanya kazi Zanzibar. Kwa hiyo, ina maana likiwa hilo litafanyika sasa katika masuala ya kuomba kazi, kwa sababu hii pamoja na kuwa ni taasisi ya ulinzi ya serikali lakini itakuwa inafanya shughuli zaidi za kibiashara na katika mambo ya kibiashara, tunajua kuna baadhi ya mahoteli ambayo sasa hivi kuna *Security Company* tofauti; nyengine za ndani na nyengine za nje.

Sasa, je, hakutokujakuwa na *conflict of interest* hapa, ikiwa wao watakuwa na kazi ya kutoa mafunzo pengine wakaja wakafanya wale kampuni nyengine kuwalazimisha baadhi ya mambo, kwa sababu unajua mafunzo unakwenda kupewa maelekezo. Sasa hebu hapa atusaidie Mhe. Waziri, ndio maana nikauliza pale mwanzo kama tungekuwa tuna sera ya ulinzi wa ndani kwa Zanzibar, hili suala lingeelezwa kwenye sera katika suala zima la vigezo vya kampuni kuwa inaitwa Kampuni ya Ulinzi na vigezo mbali mbali. Lakini sasa hapa sisi hatuna hiyo sera, tumekuja moja kwa moja na sheria ambapo hawa JKU tukishapitisha sheria hii inawezekana kuna kampuni zitavutiwa na taasisi hii ya JKU kwa sababu watakuwa wanatumia silaha za moto na wataweza kuyanyima kazi makampuni mengine ambayo yaliyokuwa yakifanya kazi hizi mwanzo.

Je, hakutokuwa na *conflicts* katika sheria hii na haya makampuni mengine yaliyoanzishwa? Vile vile, ukizingatia kwamba haya makampuni mengine ya ulinzi sijui kulikuwa kuna sera gani ambayo ilikuwa inaongoza. Sasa hapa kama hakuna kitu kama hicho, basi serikali tuangalie utaratibu wa kuandaa *policy* ya ulinzi wa ndani ili vyombo hivi katika masuala mazima ya ulinzi yasije yakaleta migogoro.

Mhe. Naibu Spika, kwa nini nikasema hivyo? Sasa hivi kumekuwa na vijana wetu wengi ambao wamekosa ajira za moja kwa moja. Kuna *Private Company* nyingi, pengine kuna watu hawa mafunzo ya ulinzi hawana wameanzisha kampuni zao ndogo ndogo kwa ajili ya ulinzi. Tunashukuru kwa sababu vijana wetu wanapata rizki, lakini kumekuwa kuna matatizo mengi sana; wakati mwengine wanatujia mpaka majumbani mwetu, mtu anafanya kazi analinda miezi mitatu hajalipwa mshahara wake.

Wakati mwengine mtu anaambiwa kwamba utaajiriwa utalipwa mshahara pengine shilingi laki moja na nusu mwisho wa mwezi, anakuja kulipwa shilingi laki moja; yaani kumekuwa na mambo mengi ya ujanja ujanja ambayo vijana wetu yanakuwa yanawasumbua.

Unajua mambo ya kazi ukishapata kazi unajua mwisho wa mwezi napata shilingi laki moja na nusu, hamsini elfu kwanza unaikopea, mwisho wa mwezi umetegemea utapata shilingi laki moja na nusu unapata shilingi laki moja.

Mhe. Naibu Spika, haya ninayoyazungumza yameshawakuta sana vijana wetu, wakati mwengine unakuta vijana wako majumbani kwetu usiku foleni utafikiria labda Mhehsimiwa kuna tatizo gani, kumbe vijana wanakuja kulalamikia haki zao. Sasa ndio maana mimi nikasema kwamba hatuna sera ya ulinzi ya ndani, basi serikali iandae kitu kama hicho, ili hawa makampuni ya ulinzi yasiwadhulumu vijana wetu. Kwa sababu mtu leo watu wamelala wakati wa binadamu kupumzika, yeye ndio anakwenda kukaa pale analinda na ulinzi wenyewe pengine umempa gongo ndio analinda. Sio gongo la kunywa; gongo lile la kumpigia mtu au la kutisha mtu, mana jambazi gongo haliogopi. Mwizi gongo analiogopa lakini jambazi haliogopi. Ndio maana nikasema tukishapitisha sheria hii, kampuni nyingi za ulinzi zitakosa kazi.

Mhe. Naibu Spika, ukiangalia hata hao vijana wanaochukuliwa katika hizo kampuni za ulinzi hajawahi kulinda, hata siku moja hajawahi kupata mafunzo, hata mafunzo ya kukwepa kile kibao hajawahi kupata. Lakini unamkuta pale ameshashonewa *uniform,* amepiga kofia yake kubwa, matokeo yake inabidi yeye ndiye alindwe. Kwa sababu kama mtu hajui kujihami inabidi analindwe yeye sasa baada ya yeye kulinda.

Vile vile na mkono mkono pia huwa unatokezea. Kuna kampuni sitaki kuzitaja maana hizo siri za watu; kuna kampuni mpya zimeanzishwa hapa wamechukua wafanyakazi ndani ya miezi miwili watu tayari wako Mazizini pale Kituoni Polisi, sijui huyu kaiba maziwa, huyu kaiba nini. Kwa sababu gani, wale walinzi wanaokwenda kulinda hawana mafunzo ya ulinzi maana yake kwanza kazi ya ulinzi ufundishwe kuheshimu kile unachokwenda kukilinda. Lakini sasa kama wewe uliekwenda kulinda unaanza kukinyemelea kile unachokilinda, sasa inabidi wewe ndio ulindwe. Hiyo inakuja kwa sababu gani, kunakuwa hakuna ukaguzi, na hakuna mchujo.

Kwa hiyo, muhimu sana serikali yetu kuangalia kwamba hata baadae, basi tuangalie kuwe na muongozo au sera ya ulinzi wetu wa ndani. Maana tukisema sera ya ulinzi Zanzibar tutakuwa tumekiuka Katiba ya Jamhuri ya Muungano, lakini tukisema sera ya ulinzi wa ndani, hiyo tutakuwa hakuna matatizo yoyote.

Mhe. Naibu Spika, sasa eneo hilo kidogo tufafanuliwe, najua unanitizama lakini niliseme sana kwa sababu ndio mambo ambayo yaliyokuwepo. Unajua kuna sheria nyingi tunazipitisha hapa ni sheria tu pengine za utekelezaji wa matakwa ya kimataifa, lakini hii ni sheria 100% ya Wazanzibari wenyewe. Wazanzibari wanahitaji kulindwa, ulinzi uliokuwa wa uhakika kabisa.

Mhe. Naibu Spika, nimejaribu kuangalia kifungu (a) mpaka (d) lakini vile vile nimeangalia kifungu (f). Kifungu hiki kinasema: "Kuandaa mfumo mzuri wa uendeshaji na utekelezaji wa huduma za ulinzi wa utalii na nyenginezo". Sasa hii ndio ile niliyozungumza inakuja kama *policy*, unaposema kuandaa mfumo mzuri basi mfumo ina maana ni muongozo. Kwa hiyo, ina maana hii inakuja kama ni *policy*.

Lakini vile vile (g) inasema: "Kukuza, kuendeleza na kuendesha miundombinu ya huduma za ulinzi". Sasa hii je, kwa taasisi zote au kwa wao tu wenye hii taasisi. Maana yake unaposema kukuza, kuendeleza, kuendesha miundombinu ya huduma za kiulinzi, ina maana miundombinu ya huduma za kiulinzi mambo ya *CCTV Camera*, mambo ya *Radio Call* na mengineyo. Je, katika hiyo miongozo wao hawa watakuja kuzitafuta wa-*supply* kwa yale Makampuni mengine, mfano hizi *Radio Call?* Kwa sababu moja katika chombo muhimu sana katika ulinzi ni *radio call*; *radio call* ni ulinzi unachukua sawasawa na ulinzi wa walinzi 20 kwa kutumia *radio call.* Lakini sasa ukiangalia hizi kampuni zetu nyingi za ulinzi anakwenda pale hata hiyo simu haina vocha. Kwa hiyo ina maana akizidiwa sasa ana-*beep*, ushavamiwa una-*beep* vijana wa mjini wanakwambia una-*beep fire*. Unaunguliwa na moto unam-*beep* Kamishna wa *Fire,* sasa huo moto utakuunguza wewe kwanza.

Sasa hii ndio ile niliyoizungumza kwamba kukuza na kuendeleza, kuendesha miundombinu ya huduma za ulinzi, huduma za ulinzi ziko nyingi. Kwa hiyo ina maana hawa watakuwa kama wanasimamia mpaka ile *policy* ya ulinzi katika nchi yetu.

Vile vile, imeelezwa kutoa miongozo mbali mbali ya kiulinzi kwa ajili ya kutumika katika sehemu za maeneo ya uwekezaji na nyenginezo kwa niaba ya serikali. Sasa hii ndio ile niliyokuwa nasema *policy,* sasa mambo haya nafikiri yangelikuwa yameandaliwa na ile JKU yenyewe, halafu hii taasisi ikawa inafuata hii miongozo ya ile JKU yenyewe. Kwa sababu hii ni *Private Company,* inaweza ikaja ikaingia kwenye *tender*.

Mfano mdogo sasa hivi tunamshukuru Mwenyezi Mungu pamoja na makelele tuliyoyapiga Barazani, lakini tunaishukuru serikali limejengwa hoteli kubwa pale Mambo Msiige. Siku hiyo ya ufunguzi ule mstari wa mbele lazima wakae Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi, maana yake hoteli ile imeleta historia kubwa katika nchi, tulisema mpaka tukapasuka lakini chuma ndio kile pale sasa hivi.

Mhe. Naibu Spika, unajua Waswahili wanasema "Ukimuona mtoto analia sana pengine kuna kunguni anamnyukua". Sasa hivi si tushanyamaza, kwa sababu gani kuna hoteli kubwa nafikiri la Kimataifa la mwanzo kwa Zanzibar. Sasa pale wale hawatokwenda kumtafuta mlinzi wa gongo, pale tunategemea sheria hii baada ya kupitishwa hatujajua utaratibu wa wenzetu. Mambo haya mara nyingi yanaendana na *tender*.

Sasa kwa kuwa wao ndio watakuwa wanatoa miongozo na vigezo, kwa hiyo ina maana kutakujakuwa na kazi ya *tender* ndio maana nikasema haya ambayo ninayataja, hizi kazi zao nyingi zilikuwa ziwe ni kazi za JKU yenyewe kutoa miongozo kwa taasisi ya JKU ya ulinzi, pamoja na taasisi nyengine kutoa miongozo ya masuala mazima ya ulinzi.

Mhe. Naibu Spika, (i) inasema: "Kutoa maelekezo kuhusiana na vifaa na mitambo ya kiusalama, kiulinzi katika maeneo ya uwekezaji na mengineyo kwa niaba ya serikali". Sasa hayo wao watakuwa ni kazi yao kuwaelekeza hao wawekezaji. Kama nilivyosema wanaweza wakatoa maelekezo, lakini pale kuna kampuni nyengine ambazo zinafanya kazi kwa muda mrefu ikaja ikaonekana kwamba labda wao wanakwenda kutoa miongozo. Sasa kwa kuwa wale walinzi waliokuwepo mwanzo hawajatoa miongozo ile na pengine hawakuona umuhimu nayo ikaja ikaleta zile *conflict,* ndio maana nikasema kazi hii mengi haya mimi nilikuwa nahisi yaandaliwe na JKU yenyewe, halafu katika hii taasisi itakayoundwa kuwe kuna miongozo na hizo taasisi nyengine ya kukamilisha hayo mambo yanayotakiwa yafanywe.

Mhe. Naibu Spika, Ibara ya Saba au kifungu cha 7. Kifungu hiki kinazungumza uwezo wa taasisi ya ulinzi, (a) "Kumiliki na kutumia silaha katika kutekeleza majukumu yake kama ilivyoelekezwa na sheria hii na kanuni zilizotungwa chini ya sheria hii".

Mhe. Naibu Spika, sheria hii hasa ibara hii ya 7(a) huu ndio muarobaini wa yale ambayo yalikuwa yanatokezea. Tumeshashuhudia kuna askari wetu wa vikosi vyetu vya SMZ wanapewa kazi ya kwenda kulinda katika maeneo tofauti tofauti na wakati mwengine huwa yanatokezea majanga, yanapotokezea majanga yale unajua katika mambo ya ulinzi haya pengine kutokana na uhaba wa askari vikosi vyetu pengine wanawachukua mpaka wale vijana waliokuwa wanajitolea. Sasa inapokuja kutokezea jambazi amekuja na silaha ina maana kijana wetu yule akipata madhara chombo chetu cha ulinzi kinakuwa kimeingia kwenye hatia. Lakini kwa sheria hii sasa hivi suala hili nafikiri litakuwa limepatiwa muarobaini.

Kwa hiyo, hata vijana wetu ambao wanaojitolea JKU sasa hivi kwa wale ambao ajira imechukua muda hawajapata basi wataweza kuajiriwa kama ilivyosemwa, kwamba ajira ya kushikizwa katika JKU angalau wakawa wanapata pesa ya sabuni. Kwa sababu kama tunavyoona vijana wetu wanakwenda kule wanagaragara miezi sita, saba wengine mpaka miaka miwili lakini akirudi nyumbani anakwambia mjomba leo sabuni ya kufulia sina. Lakini kwa sheria hii naamini wale wengi sasa hivi ikishapita basi wataingia katika hii Kampuni, wataweza kupata angalau rizki na watoto wao.

Mhe. Naibu Spika, hapa (b) imeeleza "Kuratibu shughuli za utoaji huduma za ulinzi wa kampuni au taasisi binafsi". Kwa hiyo, ndiyo kama pale nilivyosema kwamba hii ina maana pamoja na kwamba itakuwa inafanya kazi za ulinzi lakini watakuwa wanaratibu na zile shughuli za kampuni nyengine. Sasa ndio pale nilipokuwa naogopa ile *conflict of interest* isije ikatokezea.

Vile vile, hii (c) sina matatizo nayo lakini 7(d) inasema "Kuanzisha ofisi ndogo au uwakilishi ndani ya visiwa vya Unguja na Pemba kama itakavyoamuliwa na bodi". Sijui wamekusudia nini, Mhe. Waziri atakuja kunisaidia hapa. Kwa sababu JKU ipo Unguja na Pemba na ukishaanzisha shirika au taasisi na mimi zaidi neno taasisi sikuliafiki sana, kama ingekuwa shirika hasa ndio ingekuwa mahala pake. Sasa baadae huko sijajua Waheshimiwa tutakavyokubaliana kama mfano itakuwa shirika, JKU iko ndani ya Zanzibar na hii mipaka ya bahari isifanye kutugawa. Kwa hiyo ina maana kama hawa wakishakuwa na ofisi yao makao makuu wanaweza wakaanzisha ofisi sehemu nyengine zozote.

Kwa sababu kama mfano tulivyopitisha sheria ya JKU hatukusema kwamba watakuwa na ofisi Unguja, watakuwa na ofisi Pemba, watakuwa na ofisi wapi, wao wenyewe tu kwa kuwa ni taasisi ambayo ipo kisheria sehemu yoyote wanaweza wakaanzisha ofisi kwa kuendeleza zile shughuli zao.

Mhe. Naibu Spika, Ibara ya 9(1) inasema: "Kutakuwa na Mkurugenzi Mkuu wa taasisi ya ulinzi ambaye atateuliwa na rais". Sasa hapa ndio ile hofu yangu ya mwanzo ndio maana nikajaribu ku-*reflect* na ile sheria ya wenzetu kule Tanzania Bara. Hili vile vile nitamuomba sana Mhe. Waziri kwa kuwa leo tuna siku ya Ijumaa na mida yenyewe hii ya kumalizia hizi shughuli zetu, itakuwa haiko mbali sana kumaliza; ningelimuomba sana atumie muda wake wa Jumamosi na Jumapili kuwasiliana na wenzetu wa Tanzania Bara au hata kuangalia ile sheria yao, tukajaribu kuangalia hii Mkurugenzi ambaye atakuwa anaendesha hii taasisi.

Kwa sababu kule wenzetu mimi nilivyojaribu kuangalia kipindi kile kama nitakuwa na kumbukumbu sahihi kwamba msaidizi wa Mkuu wa JKT anakuwa moja kwa moja yeye ndiye kiongozi wa taasisi hii ya ulinzi.

**Mhe. Naibu Spika:** Mheshimiwa malizia.

**Mhe. Hamza Hassan Juma:** Mhe. Naibu Spika, kwa heshima kubwa naomba dakika zangu 15 zilizobakia nije nimalizie siku ya Jumatatu. Mhe. Naibu Spika, nakushukuru, ahsante sana.

**Mhe. Naibu Spika:** Waheshimiwa Wajumbe kwanza niwashukuru kwa kushirikiana tangu asubuhi hadi sasa hivi, lakini kabla sijaakhirisha kikao chetu pana tangazo nimepewa nitangaze na uongozi wa Baraza, kwamba mnaarifiwa semina ya Mtakwimu Mkuu wa Zanzibar na Mtakwimu Mkuu wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kupitia Wizara ya Fedha ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, itafanyika siku ya tarehe 25/01/2015 yaani siku ya Jumapili saa 8:00 mchana katika jengo letu hili, ukumbi wa juu badala ya tarehe 24.

Kwa hivyo, wale waliokuwa hawapo tukifika huko mitaani tuwaeleze wenzetu kwamba semina badala ya Jumamosi itakuwa Jumapili tena saa 8:00 mchana. Baada ya tangazo hilo sasa naomba niakhirishe kikao chetu hadi tarehe 26/01/2015 siku ya Jumatatu saa 3:00 asubuhi.

*(Saa 1:45 usiku Baraza liliakhirishwa hadi tarehe 26/01/2015 saa 3:00 asubuhi)*